

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Nne – Tarehe 5 Novemba, 2021

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nawaomba tukae. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Mkutano wetu wa Tano, Kikao ni cha Nne.

Katibu!

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na TAMISEMI. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, uliza swali lako tafadhali.

Na. 39

Malipo kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa

MHE. MRISHO S. GAMBO aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanapata malipo kama Madiwani na Wabunge kutohana na majukumu mazito wanayoyafanya ikiwemo ufuatiliaji wa malipo ya Kodi ya Majengo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa, Dkt. Festo John Dugange, tafadhalli.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kwa kuwa ndio wasimamizi wakuu wa shughuli zote za maendeleo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ngazi ya Vijiji na Mitaa za Mwaka 2014 chini ya Tangazo la Serikali Na. 322, mionganoni mwa sifa zinazomwezesha mkazi wa Kijiji, Mtaa au Kitongoji kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti ni pamoja na kuwa na shughuli halali inayomwingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa mwongozo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu malipo ya posho ya viongozi hawa kwa kutumia mapato ya ndani kadri ya uwezo wa Halmashauri. Kwa ujumla, uwezo wa Halmashauri zilizo nyingi bado ni mdogo katika kutekeleza jukumu hili. Hivyo, Serikali imeichukua changamoto hii na itaendelea kufanya tathmini. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mrisho Gambo nimekuona.

MHE. MRISHO S. GAMBO: Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji ndio msingi wa Serikali za Mitaa katika nchi yetu, na kwamba, maelekezo mengi ya Serikali kutoka ngazi ya TAMISEMI, mikoa, wilaya na halmashauri yanapelekwa ngazi za chini na wao ndio wanazisimamia.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, Jiji letu la Arusha limeongoza kwa mapato kwenye hii robo ya kwanza. Na ukizingatia kwamba, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 tulitenga fedha kwa ajili ya kulipa shilingi elfu 50 kwa kila Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na bado halmashauri yetu haifanyi hivyo. Je, ni nini kauli ya Serikali kwa Halmashauri ya Jiji la Arusha kuhusiana na changamoto hii ambayo inawakumba Wenyeviti wa halmashauri?

Mheshimiwa Spika, swalı langu la pili; ukizingatia kwamba, uchaguzi wa Serikali za Mitaa ulifanyika mwaka 2019 na mpaka sasa Wenyeviti wa Serikali za mitaa hawajapatiwa semina, hawapewi *stationaries* zozote, hawajapewa vitambulisho na hata bendera kwenye maeneo yao pia hazijapatikana na hasa ukizingatia pia hawana hata ofisi. Inabidi wachangishe kwa watu waende wakaombe hela kwa wadau, ili mwisho wa siku waweze kulipia ofisi.

Mheshimiwa Spika, hatuoni kwa kufanya namna hiyo tunawaweka kwanye mazingira ya rushwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa? Je, nini kauli ya Serikali kwenye kutoa heshima kwenye ofisi za Serikali za mitaa?

SPIKA: Majibu ya swalı hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Dugange, tafadhalı.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA,
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, viongozi hawa Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji wanafanya kazi kubwa sana katika kusukuma maendeleo ya nchi yetu. Na ndio maana katika jibu la msingi nimeeleza namna ambavyo Serikali imeendelea kutathmini na kuweka njia bora zaidi ya kuhakikisha tunawawezesha Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji kupata posho zao kila mwezi, lakini kwa sababu halmashauri

zetu hazijawa na uwezo wa kutosha tunaendelea kuona namna gani tutaboresha mfumo huu, ili waweze kupata posho hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali ilitoa mwongozo kwamba, kila halmashauri itenye fedha kulingana na uwezo wa mapato yake na iweze kuwalipa posho hizo Wenyeviti wa Mitaa.

Kwa hiyo, naomba nitoe maelekezo kwa Halmashauri ya Arusha na halmashauri nyingi zote nchini, zile ambazo zimetenga bajeti na zina uwezo wa kukusanya fedha hizo ziendelee kuwalipa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji kwa kadiri ya bajeti ambazo wamezitenga.

Mheshimiwa Spika, lakini pili, Serikali imeendelea kutoa fedha ambazo ni fidia ya vyanzo villyofutwa (*GPG*), kwa maana ya asilimia 20 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa ofisi za vijiji na mitaa. Utaratibu huu unaendelea ili kuwezesha kuweza kununua shajara, lakini na matumizi mengine ya kila siku. Ahsante.

SPIKA: Tunaendelea na maswali. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu; Mheshimiwa Kamamba, tafadhali.

Na. 40

Hitaji la Vituo vya Afya - Kakonko

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Zahanati na Vituo vya Afya katika Wilaya ya Kakonko?

SPIKA: Bado tuko kwako Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Dugange.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya vya kimkakati nchini, ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi bilioni 38.15 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 758 kote nchini. Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imetengewa shilingi milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tatu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetoa fedha za makato ya tozo za miamala ya simu shilingi bilioni 55.25 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya 221 kwenye Tarafa zisizo na Vituo vya Afya vyenye uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji, ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko imepokea shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya katika Tarafa ya Nyaronga kata ya Gwalama.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kujenga zahanati na vituo vya afya katika Wilaya ya Kakonko na nchini kote katika maeneo ya kimkakati kulingana na vigezo vilivyowekwa badala ya kila Kijiji na kila Kata. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Buyungu, nimekuona.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Serikali ambayo yametolewa na Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, zimetengwa milioni 150 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati tatu.

Je, Serikali lini itapeleka hizo fedha milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha zahanati hizo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ukamilishaji wa zahanati hizo tatu utasababisha uhitaji mkubwa wa wataalam katika kada ya afya ambapo bado mpaka muda huu tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi katika kada hiyo ya afya.

Je, lini sasa Serikali itapeleka watumishi wa kutosheleza mahitaji ya watumishi wa kada ya afya katika wilaya ya Kakonko? Nashukuru sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri nimekuona.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha hizi ambazo zimetengwa kwenye mwaka huu wa fedha 2021/2022 zitaendelea kupelekwa kwenye majimbo yetu, kwenye kata zetu kadiri zinavyopatikana. Kwa hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka huu wa fedha fedha hizi zitapelekwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati hizi tatu katika Jimbo hili la Kakonko.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la watumishi; ujenzi wa zahanati na vituo vyta afya unaenda sambamba na mipango ya ajira kwa ajili ya watumishi wetu kuhakikisha wanakwenda kutoa huduma katika vituo hivyo. Kwa hivyo, pamoja na ujenzi, lakini pia mipango ya ajira inaendelea kufanywa na vibali katika mwaka huu wa fedha vinaandaliwa kwa ajili ya kuajiri watumishi kwenda kutoa huduma za afya katika vituo hivyo. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba, suala hilo pia litakwenda sambamba na ujenzi wa vituo katika maeneo hayo. Ahsante.

SPIKA: Bado tuko TAMISEMI, Mheshimiwa Ester Bulaya nilikuona.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilihamasisha wananchi mbali ya kujenga shule, lakini waweze kuanza kujenga zahanati na mwisho wa siku Serikali kutoa mchango wake. Sasa wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini walihamasika sana na kwa mfano maeneo ya Zahanati ya Changuge, Mchalo, Gushigwamara, Nyamatoke, maeneo hayo yote wananchi walihamasika na nilichangia kwa kuweka fedha ya Mfuko wa Jimbo.

Je, Serikali ni lini sasa mtamalizia ili wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini kwa maeneo ambayo nimeyataja wawe na uhakika wa kupata huduma ya afya katika maeneo yao? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Dugange, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujali afya za wananchi kwa kuwashemasisha kutoa nguvu zao kujenga zahanati na Serikali kuchangia nguvu za wananchi katika ukamilishaji wa maboma ya zahanati. Na katika jibu langu la msingi nimeeleza jumla ya maboma 758 yatakwenda kujengwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, jitihada zake, lakini pia jitihada za Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini zimeendelea mara kwa mara kuikumbusha Serikali. Na nimhakikishie kwamba, tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunatafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo. ahsante.

SPIKA: Ahsante, tunahamia Wizara ya Maji. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma uliza swali lako.

Na. 42

Tatizo la Maji Katika Mji Mdogo wa Mikumi

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA aliuliza:-

Je, ni lini tatizo la maji litakwisha katika Mji Mdogo wa Mikumi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifauatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa Mji wa Mikumi ni wastani wa asilimia 62.3. Mahitaji ya maji kwa sasa kwa Mji wa Mikumi ni takriban lita milioni 3.4 kwa siku ukilinganisha na uzalishaji wa maji wa lita 900,000 kwa siku. Katika jitihada za kumaliza tatizo la maji, Serikali ina mpango wa muda mfupi na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mfupi, katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, Serikali imepanga kuboresha Mradi wa Maji wa Msimba kwa kufunga pampu mpya, ujenzi wa tangi la ujazo wa lita 90,000 na kuongeza mtandao wenye urefu wa Kilometra 6.5. Maeneo yatakayohudumiwa na mradi huu ni pamoja na Mitaa ya Msufini, Ng'apa, Msimbakati na Miomboni. Vilevile, mpango huu wa muda mfupi unahusisha ujenzi wa Mradi wa Maji Rutwina ambao unahusisha uchimbaji wa kisima kipywa, ufungaji wa pampu na ulazaji wa bomba kuu umbali wa Kilometra 1.5 kutoka kwenye kisima hadi kwenye tanki la kuhifadhi maji eneo la Kidoma Mlimani. Maeneo

yatakayohudumiwa ni pamoja na Kikwalaza, Tambukareli, Kidoma na Chekereni. Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kuanza mwezi Disemba, 2021 na kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2022.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa muda mrefu, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi wa kutumia chanzo cha Mto Madibila. Mradi huo utahudumia maeneo ya Chekereni, Kikwalaza, Kidoma, Tambukareli, Magoma, Mjimpya, Mowlem na Green. Zabuni ya kumpata Mkandarasi wa kujenga mradi huo, imetangazwa tarehe 21 Oktoba, 2021. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2022 na kukamilika mwishoni mwa mwezi Disemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo yote ikikamilika itamaliza changamoto ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Mikumi na kufikia lengo la asilimia 95.

SPIKA: Mheshimiwa Ishengoma nimekuona.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Licha ya majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa Wizara ya Maji inafanya kazi sana kwa jitihada zao, licha ya jitihada hizo, lakini bado watu wanataka maji. Kata ya Ruaha ambayo iko kwenye Jimbo hilohilo la Mikumi, Wilaya ya Kilosa waliahidiwa na Mheshimiwa Rais Awamu ya Tano kupatiwa maji. Kwa hiyo, nauliza ni lini watapatiwa maji? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Kata ya Lukobe ambayo iko Manispaa ya Morogoro tulitembelea kamati yangu na wananchi wakaahidiwa kuwa watapariwa maji kuanzia mwezi wa nane hilo tanki la mguru wa ndege, lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea tanki hilo halijawahi kupata maji na sasa ni mwezi wa 11 na ahadi ilikuwa mwezi wa nane, wananchi wanakunywa maji ya visima ambayo ni maji yasiyo Safi na salama. Na wamenituma wanaauliza ni lini watapatiwa

hayo maji kuititia kwenye tanki hilo la Mguu wa Ndege?
Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, kipekee nipende kumshukuru Mheshimiwa Mama yangu Dkt. Christine Ishengoma kwa namna ambavyo anaendelea kufuatilia suala hili la maji katika maeneo ya Mkoa wa Morogoro na nikushukuru sana Mheshimiwa Christine Ishengoma kwa ushirikiano ambaao umeendelea kutupa sisi Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la kwanza Kata ya Ruaha; tayari *RUWASA* wameshafanya taratibu zote na sasa hivi wametangaza ili tuweze kumpata mkandarasi. Na tunaamini kwa kasi ambayo tunaenda nayo watu wa Ruaha nao watakwenda kunufaika muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa eneo hili la mguru wa ndege wakati wa ziara na mimi nilikuwepo. Mheshimiwa Dkt. Christine kama ambavyo tumekuwa tukiwasiliana kwenye suala hili, lile tanki hata ukipita pale barabarani unaliona kubwa, zuri, lenye ubora kabisa limeshakamilika na sasa hivi tunaingia kwenye awamu sasa ya usambazaji na tayari Wizara tunapeleka fedha kwenye mgawo huu unaokuja kwa lengo la kuona sasa maji yanakwenda kuwafikia wananchi wote wa eneo la Lukobe. Ahsante.

SPIKA: Tunaendelea na swali kinalofuata. Tumalizie lile swali la TAMISEMI, Mheshimiwa Mbunge wa Kishapu, Mheshimiwa Butondo.

Na. 41

Mgogoro wa Mipaka Kati ya Wilaya ya Kishapu na Wilaya ya Iramba

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro uliopo mpakani mwa Wilaya ya Kishapu Kata ya Mwamalasa Kijiji cha Magalata na Wilaya ya Iramba?

SPIKA: Majibu ya Serikali kwa swali hilo. Sijui kuna mgogoro gani hapa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, upo mgogoro wa mipaka kati ya Wilaya ya Kishapu na Wilaya ya Iramba. Mgogoro huo upo katika eneo la Bonde la Mto Manonga katika Kijiji cha Magalata Wilaya ya Kishapu na Kijiji cha Mwasangata Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, Mgogoro huu unatokana na malisho ya mifugo na maji, ambapo kwa upande wa Wilaya ya Kishapu jamii ya wafugaji wanaoishi kijiji cha Magalata hutumia bonde la Mto Manonga kwa ajili ya malisho na maji na upande wa Wilaya ya Iramba jamii ya wafugaji wanaoishi kijiji cha Masangata hutumia pia bonde la mto Manonga kwa ajili ya malisho na maji. Mgogoro huu mara nyingi hutokea wakati wa kiangazi ambapo jamii za pande zote mbili hutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo ambayo hupatikana kwa wingi katika Bonde hilo.

Mheshimiwa Spika, vikao mbalimbali vyatya usuluhishi vimefanyika vikihusisha viongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Uongozi wa Mikoa, Wilaya na Wananchi wa Vijiji vinavyohusika. Aidha, vikao hivyo vimesaidia kurejesha amani, utulivu na usalama kati ya vijiji hivyo hususan Magalata na Mwasangata.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaeendelea na jitihada za kuutatua mgogoro huu kwa njia shirikishi ili kudumisha amani na utulivu katika maeneo hayo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Butondo nimekuona.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Spika, mimi naomba nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza siyo peke yake mgogoro huu umekuwepo nyakati za kiangazi mgogoro huu umekuwepo nyakati zote masika na kiangazi na sasa hivi tunapozungumza habari za shughuli za kilimo maana yake zinapoenda kutekelezwa na wananchi wa maeneo haya kipindi hiki pia mgogoro huu unaweza ukaibuka. Kwa hiyo siyo sahihi kwamba ni nyakati za kiangazi peke yake na hata masika kwa sababu shughuli za kibinadamu zinafanyika nyakati zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu umekuwa ukichangia sehemu kubwa sana uvunjifu wa amani wa wananchi wetu nataka nipate *commitment* ya kutosha ya Serikali kwamba ni lini sasa watakwenda kutatua mgogoro huu ikiwa ni pamoja na kuijumlisha Wizara ya Ardhi kuhakikisha wanaenda kuainisha na kuweka *beacon* ili mipaka ya maeneo ya kiutawala yaweze kuainishwa sawasawa. (*Makofii*)

Swali la pili Wizara ya Ardhi mwaka 2019 walifika katika eneo hili la mgogoro na kwa bahati mbaya kwa sababu walifika nyakati za masika maji yalikuwa yametapakaa katika maeneo hayo ya mipaka na kwa hali hiyo walishindwa kufanya suala zima la kuainisha lakini pia na kuweka *beacon*

na waliahidi wangeweza kutekeleza na kuumaliza mgogoro huu uliokuwepo katika maeneo haya ya Iramba na Kishapu.

Je, ni lini Wizara ya Ardhi watafika na kuhakikisha wanaweka *beacon* kuainisha maeneo ya kiutawala lakini na kuweka *beacon* ili mgogoro huu sasa usiendelee na wananchi waendelee na shughuli zao za maendeleo. (*Makofii*)

SPIKA: Mnagombea nini huko wakati nchi ni moja ya Mama Samia hii nchi? Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naomba nichangie kidogo nyongeza ya swalii hili, nafikiri nilikutana na huyu Mheshimiwa Mbunge naliija hili tatizo lakini mimi sijawahi kushiriki vizuri, lakini niliwaahidi kwamba tungeweza tukakutana na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI tukazungumza kwanza kiutawala kati ya Wakuu wa Mikoa hawa wawili lakini mimi Wizara yangu kazi ya kutafsiri mipaka ndiyo kazi yake kwa *GN* zilizoandikwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo nataka kumuahidi Mheshimiwa Mbunge nitalisimamia mwenyewe hilo la kuweka mipaka ili wananchi wa Wilaya hizi waweze kujua mipaka yao iliyoainishwa na mwenye mamlaka kwa sababu mamlaka ya kugawa mipaka ya utawala ni ya Mheshimiwa Rais, sasa wakati mwingine huwa inatokea wananchi wanasema nilikuwa hapa nilikuwa hapa nawakumbusha tu mwenye mamlaka ya kugawa mipaka ya utawala ni Mheshimiwa Rais na mipaka hii huwa inaandikwa kwenye Kanuni zinaitwa *GN* na *GN* tunazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mbunge wananchi waambie Wizara yangu itakuja kutafsiri ardhini mipaka iliyoainishwa kama nia ya Mheshimiwa Rais ya kupanga na kuunda hizo Wilaya mipaka ya ardhini itakuja kuainishwa na kutafsiriwa na Wizara yangu na jambo hili litafanyika mara moja. (*Makofii*)

SPIKA: Nakushukuru sana kwa majibu mazuri Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Sasa tunahamia Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Dkt. Stephen Lemomo Kiruswa Mbunge wa Longido uliza swali lako.

Na. 43

Kuboresha Miundombinu ya Minada ya Mifugo Nchini

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaboresha Miundombinu ya Minada ya Mifugo kwa kujenga mazizi ya kisasa, vyoo na ofisi za kupokea tozo na kodi za mnada.

SPIKA: Majibu ya swali hilo nimekuona Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa - Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha minada nchini ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara katika bajeti ya maendeleo imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 4.46 kwa ajili ya kukarabati na kujenga miundombinu ya minada 19 ya upili mpakani na ya awali kwa kujenga uazio, ofisi, mazizi ya kisasa ya ng'ombe na mbuzi, vyoo, vipakilio na mabirika ya kunywea maji mifugo katika minada ya Pugu (Dar es Salaam), Mkia (Pwani), Mtukula (Kagera), Horohoro (Tanga), Ndelema (Tanga), Malampaka (Simiyu), Magena (Mara), Igunga-(Tabora), Buhigwe (Kigoma), Ipuli (Tabora), Wasso (Arusha), Gendi (Manyara), Kileo (Kilimanjaro), Meserani (Arusha), Nyanguge (Mwanza), na Nyamatala (Mwanza). Utekelezaji unatarajiwa kuanza mwezi huu wa Novemba, 2021 na utachukua miezi minne kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya minada nchini kulingana na uwezo wa kibajeti. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kiruswa nimekuona

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza, lakini kabla sijaauliza maswali yangu madogo kuna kumbukumbu naomba kuiweka kwa usahihi kuhusiana na suala zima la ushuru na tozo za minada ya mifugo katika Wilaya ya Longido tulipata heshima kubwa ya kutembelewa na Rais kama wiki mbili zilizopita tarehe 18 na kuna Waandishi wa Habari ama wamempa Rais habari ambayo siyo sahihi, baada ya kufungua kiwanda kikubwa cha nyama ambacho kimezinduliwa kilijengwa na wawekezqji kwa zaidi ya shilingi billioni 17 akapata taarifa kwamba inazalisha chini ya kiwango kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Longido inatoza kodi na ushuru mkubwa unaosababisha wafugaji kupeleka mifugo Kenya.

Mheshimiwa Spika, kumbe Halmashauri ya Wilaya ya Longido hajjawahi kuchukua hata shilingi katika kile kiwanda tangu kianze na kodi zinazokusanywa zinaenda Wizarani na taarifa hiyo ilitoka katika taarifa ya lkulu wananchi wa Longido walikereka sana na hiyo kauli, nikaomba sasa basi nitoe hapa wasikie kwamba nimewasema na ndipo sasa niulize maswali yangu mawili madogo ya nyongeza.

SPIKA: Sasa swali.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Swali la kwanza kwa kuwa viwanda hivi vilivyojengwa nchini hivi karibuni vyakisasa ikiweko hicho cha *Eliya Food Products* kilichoko Longido zinapata malighafi pungufu kulingana na uwezo wake.

Je, Serikali imeweka mpango na mkakati gani wa kuhakikisha kwamba malighafi ya kulisha hivyo viwanda inapatikana?

Swali la pili; kwa kuwa Wilaya ya Longido ni Wilaya ya wafugaji kwa asilimia 95 na afya ya mifugo inategemea kwa asilimia kubwa upatikanaji wa maji hasa maji ya mabwawa - malambo yale.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyafufua mabwawa na malambo yaliyofukiwa na udongo kwa miaka mingi katika Wilaya ya Longido na hasa Kiseriani ambapo maji kidogo yaliyobaki mwaka huu yanakwamisha wanyamapori? Juzi nimeweka *post* ya Pofu aliyejekuwa anatolewa na Wamasai amekwama katikati ya lile bwawa pamoja na binadamu, sisi tunatumia maji ya mifugo na binadamu pia.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kiruswa..

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Wizara ya Maji inawahuhsu mtatusaidiaje kufufua mabwawa yaliyofukiwa katika Wilaya ya Longido?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Kwa niaba ya wananchi wa Longido majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvumi, Mheshimiwa Ulega tafadhali. (*Kicheko/Makof!*)

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa Lemomo Mbunge wa Longido kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linahusu mkakati wa Serikali wa kuhakikisha viwanda hivi vinapata rasilimali, tumejipanga juu ya kuhakikisha tunaweka utaratibu wa unenepeshaji kuititia vikundi na kwa watu binafsi. Mkakati wetu ni kuwa na wanenepeshaji wasiopungua 500 nchi nzima ambao mionganoni mwao watakwendwa kuingia mikataba na viwanda, kwa mfano kiwanda cha *Eliya Foods* kimeshaanza utaratibu huo wa kuwa na *suppliers* ambao wanawapa mikataba kwa ajili ya kupeleka ng'ombe pale kiwandani na hii itatusaidia sana hata katika lile jambo la mwanzo

alilolizungumza la tozo kwa kuwa utaratibu tuliuweka wale wote watakaokuwa na mikataba na viwanda vinavyofanya uchakataji kwa ajili ya *export* tutawaondoshea baadhi ya tozo hizo ili kurahisisha vile viwanda viweze kupata malighafi kwa urahisi na kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni hili la maji katika bajeti ya mwaka 2021/2022 tunayo malambo ambayo tunayatengeneza kwenye maeneo mengine ya nchi hii, lakini nafahamu Longido uko mradi mkubwa wa maji ambao unakwenda kuwashudumia wananchi wa Longido. Tumekaa na wenzetu wa Wizara ya Maji na nimpongeze sana yeye Dkt. Kiruswa na timu nzima ya pale Longido Mkoani Arusha kwa kuwashawishi wenzetu wa Wizara ya Maji waweze kutoa matoleo ambayo yatatengeneza mabirika yahudumie mifugo na wakati huo huo yaweze kuhudumia wanadamu na sisi ndani ya Serikali tunaendelea na ushauriano ili kusudi jambo hili liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo mradi ule mkubwa wa maji uliokwenda kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuhakikisha kwamba uweze kuhudumia maji haya yaweze kuhudumia binadamu na mifugo pia. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa, aah! nyongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha tafadhali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyyoatoa nilitaka niongezee jibu sehemu ndogo ili Mheshimiwa Mbunge ambaye anawasemea sana wananchi wa Longido aweze kulibeba hilo jibu. Wizara ya Fedha pia kushirikiana na Wizara ya Mifugo tunaangalia upya sehemu ya tozo ile ambayo tuliuweka ambayo inahusu pia sekta ya mifugo pamoja na maeneo mengine ambayo yamesababisha upande wa huku Serikali Kuu iweze kuongeza hiyo sehemu ambayo ameisemea, kwa hiyo naamini kwenye kikao hiki hiki kinavyoendelea tukiwa tumeshakamilisha Mheshimiwa Mbunge atarudi Longido akiwa na jibu lilirosahihi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu ya kufufua bwawa tayari tumeshakamilisha makubaliano na Waziri wa Maji ambaye anafanyakazi nzuri sana, tumeshatoa fedha za kununua mitambo ya kuchimba mabwawa ambako kila ukanda wa nchi hii utakuwa na mtambo wake wa kuchimba mabwawa. Kwa hiyo kwa wafugaji hata kama wataamua kuchimba bwawa kila baada ya mazizi mawili Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu amesema wachimbe tu na wata-manage wenye kutoa maeneo ya kuchimba hayo mabwawa. (*Makofî*)

SPIKA: Haya wasiwasi wa maji huko Longido sasa unazidi kupungua, tunakwenda Wizara ya Ardhi Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava Mbunge wa Korogwe Vijijini endelea Mheshimiwa nimekuona.

Na. 44

Kulifuta Shamba la *Mwakinyumbi Estate* - Korogwe

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali italifuta shamba la *Mwakinyumbi Estate* lilitolekezwa kwa muda mrefu na kuwapa wananchi wa Hale na maeneo jirani ili waweze kufanya shughuli za kiuchumi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi Mheshimiwa William Lukvi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la *Mwakinyumbi Estate* lilitilikishwa kwa barua ya toleo yenye Kumb Na. TRKF/76/65/AOM kwa muda wa miaka 99 toka tarehe 1 Aprili, 1989

kwa matumizi ya kilimo. Mmiliki alipewa masharti ya umiliki kwa mujibu wa Sheria za Ardhi. Mionganoni mwa masharti hayo ni uendelezaji wa shamba na ulipaji wa kodi ya pango la ardhi kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, ukaguzi uliofanyika wa ndani umebaini kuwa shamba hilo limetelekezwa na hakuna uendelezaji wowote uliofanyika na kwa sasa shamba hilo linadaiwa kiasi cha shilingi millioni 174.73 ikiwa ni kodi pamoja na malimbikizo kwa muda wa miaka 17 kuanzia mwaka 2005 hadi mwaka huu 2021. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilianza kuchukua hatua za kisheria za kubatilisha miliki ya shamba husika kwa kutuma ilani ya kusudio la ubatilisho wa milki kwa siku tisini (90). Mmiliki hakuwasilisha utetezi wowote juu ya ilani ya ubatilisho aliyotumiwa kufuatia uvunjaji wa masharti kama ilivyoainishwa katika barua yake ya toleo. Hivyo, Serikali kwa sasa inaendelea na hatua za ubatilisho hatua zilizobaki mimi naandika barua kwa Mheshimiwa Rais kumshauri shamba hilo afute.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ufutaji wa mashamba yaliyotelekezwa nchini ni zoezi endelevu kwa mujibu wa sheria ikiwa na lengo la kulinda maslahi mapana ya Taifa, wananchi na wawekezaji. Hatua hii inapunguza migogoro ya matumizi ya ardhi ambayo imekuwa ikijitokeza katika maeneo mbalimbali nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Mnzava nimekuona

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Jambo la kwanza jambo hili limekuwa ni la muda mrefu sana na Mheshimiwa Waziri atakuwa shahidi wa jambo hilo pamoja na ahadi hii nzuri ulioitoa Mheshimiwa Waziri ningependa kujua uko tayari baada ya Bunge hili uongozane na mimi kwenda kuzungumza na wananchi wa Hale uwape matumaini ya kuharakisha jambo hili ili wapate ardhi kwa ajili ya kufanya shughuli zao za kilimo?

Mheshimiwa Spika, Swali la pili Wilaya ya Korogwe sehemu kubwa ya ardhi yake ni mashamba makubwa ya wawekezaji wa chai na wawekezaji wa m Konge na maendelezo yake hayaridhishi sana na jambo hili limefanya wananchi wetu kukosa maeneo ya kufanya shughuli za kilimo hasa vijana wamekosa maeneo ya kujajiri. Je, Serikali iko tayari kukaa pamoja na wawekezaji hawa pamoja na umuhimu wa uwekezaji wao kwenye maeneo haya lakini tufanye mazungumzo ya kuona namna gani ya kumega maeneo kwa ajili ya kuwapa vijiji ili wananchi wapate sehemu ya kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo suala la kilimo? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri wa Ardhi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mnzava Mbunge kijana machachari wa Korogwe kama ifuatavyo:

Kuhusu swali la kwanza, kwenda anauzoefu anajua akiniita naenda tulishaenda na nitakuja na huko na nitafanya yale ambayo tulifanya sehemu nyingine ambazo ulinipeleka. Kwa hiyo, wananchi wasiwe na wasiwasi Mheshimiwa Mnzava akinihitaji kwangu mimi ni agizo nakwenda tu na Waheshimiwa Wabunge wote kama kuna matatizo kama haya mkiniambia ndiyo inanisaidia kupata kazi maana mkinituma ndiyo napata uhalali wa kuja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mnzava nakuja. (*Makofii*)

Swali lake la pili; ni kweli una mashamba mengi na ni kweli kwamba kwenye mashamba mengi najua wakati ule wenye mashamba wanapomiliki hasa Kanda hii ya Kaskazini wananchi walikuwa wachache sasa wananchi wameongezeka sana. Kwa hiyo nataka ukitoka hapa muulize Mheshimiwa Mbunge wa Same hapa Mama Kilango akufundishe namna alivyofanya na mpaka na mimi nikaenda kule na moja ya shamba wananchi wakarudishiwa ekari 300. Kwa hiyo uwezekano huo upo kwa sababu mifano tunayo

tutakaa na wenyewe mashamba wanajua kabisa wanataka kuishi vizuri na majirani wao, hawakatai.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge aniorodheshee hao wenyewe mashamba ni watu gani halafu tupange ratiba tuzungumze nao wanajua hali halisi na wenyewe wanataka kuishi vizuri na wananchi wanaowazunguka kwa hiyo hilo tutafanya, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Kule Msekwa kuna swali la nyongeza Mheshimiwa Getere nimekuona.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nilipenda kujua tu kwamba Waziri anayezungumza hapa ndiyo mwenye mamlaka ya kugawa mipaka ilivyo katika wananchi na wanyamapori. Sasa nimuombe Mheshimiwa Lukuvi mpaka wa vijiji kama 11 hivi vya Jimbo la Bunda ukianzia mipaka ile ya Honyali, Maliwanda ukienda Mgeta mpaka Tingirima mpaka wao ni Mto Rubana ndiyo mto asili unaotumiwa na wananchi wa maeneo yale lakini mpaka uko katikati ya Mto Rubana. Ni lini Waziri ataenda pale kutenganisha mita 500 za wanyamapori na mita 500 za wananchi?

SPIKA: Swali linahusu mashamba sasa Mheshimiwa lakini yuko mbali kule Msekwa kwa hiyo naliruhusu Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa William Lukuvi kama umelielewa swali ni lini utaenda Jimboni kwake kule kuona namna gani huo mpaka unakua ukumbuke mpaka wenyewe *actually* ni mto unaotenganisha nafikiri unayajua hayo maeneo.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Getere kwanza nitamuona hapa hapa anipe ufanuzi vizuri zaidi lakini pia ninao uwezo wa kwenda Mkoa wa Mara kwenda kuzungumza nae na viongozi wengine ili tujue hilo kwa sababu hata vijiji huwa

vinaanzishwa kwa mfumo ule ule unaofanywa na Wilaya na Mikoa.

Mapendekezo ya kuanzisha vijiji huwa yanaanza Wilayani yanakuja mkoani mwishoni Ofisi ya Rais, TAMISEMI ndiyo inaidhinisha ambayo iko chini ya Ofisi ya Rais na kutoa *GN* maandishi yanayoainisha kila Kijiji na mipaka yake iko namna gani. Jukumu langu mimi siyo kuanzisha mipaka ya vijiji vipyta Wizara ya Ardhi hatuanzishi mipaka, tunasuluuhisha lakini kwa kutafsiri ardhini *GN* za mipaka zilizoainishwa na mamlaka inayohusika.

Kwa sababu hiyo, nitakwenda huko kwenda kuwasaidia wananchi wa vijiji hivyo kuainisha mipaka iliyopendekezwa au ilioamuliwa kuaanzisha vijiji hivyo kwa mujibu wa mapendekezo ya mamlaka. Lakini pia hiyo migogoro katika *buffer zone* na ardhi za vijiji nitapenda kumsikia lakini tutakwenda huko hivi karibuni tulikwenda Serengeti nako kulikuwa na migogoro ya *buffer zone* vijiji vilivyoanzishwa hifadhi ya Serikali ilichukua mita 500 za ardhi ya vijiji ikafanya *buffer zone*.

Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameagiza ili kuondoa tataruki, ardhi ile ambayo Serengeti walichukua kuanzia Mkoa wa Mara kule Tarime mpaka Serengeti mita 500 kwenye ardhi za vijiji zirudishwe kwenye vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumetekeleza maelekezo hayo mita 500, 500 zilizokuwa kwenye *buffer zone* ya Hifadhi ya Serengeti zimerudishwa kwenye vijiji na hivyo Serengeti sasa kama wanahitaji *buffer zone* watarudi ndani ya hifadhi yao. Lakini zile za vijiji zimerudishwa tayari, kwa hiyo hili nalo tutakwenda kujifunza *nature* ya mgogoro huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ameagiza, ili kuondoa tataruki, ardhi ile ambayo Serengeti walichukua kuanzia Mkoa wa Mara kule Tarime mpaka Serengeti, mita 500, kwenye ardhi za vijiji zirudishwe kwenye vijiji.

Mheshimiwa Spika, tumetekeleza maelekezo hayo, mita mia tano mia tano zilizokuwa kwenye *buffer zone* ya Hifadhi ya Serengeti zimerudishwa kwenye vijiji na hivyo, Serengeti sasa kama wanahitaji *buffer zone* watarudi ndani ya hifadhi yao, lakini zile za vijiji zimerudishwa tayari. Kwa hiyo, hili nalo tutakwenda kujifunza *nature* ya mgogoro huu.

SPIKA: *Actually, swali lake linahusu hiyo hiyo mita 500 ambayo tayari mmesharudisha. Mpaka wa Serengeti ni mto, kwa hiyo, kuurudisha tena ndani wala haitawezekana maana yake wanyama lazima wanywe maji pale. Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Getere ni *trick trick* hivi, lakini kwa kuwa wamesharudishiwa *buffer zone* yao, wako salama.*

Tunakwenda swali la Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, kwa niaba yake, Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Na. 45

Kutatua Mgogoro wa Ardhi Kati ya Kata ya Bendera na Mkomazi

MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro uliopo katika eneo lenye madini ya Jasi kati ya Wananchi wa Kata ya Bendera Mkoani Kilimanjaro na Wananchi wa Kata ya Mkomazi Mkoani Tanga?

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini kuptitia Tume ya Madini, imetoa leseni za uchimbaji mdogo katika maeneo hayo ya Kata ya Bendera iliyopo Mkoani Kilimanjaro na Kata ya Mkomazi iliyopo Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo ya kata hizo mbili, hivi tunavyoongea, hakuna mgogoro wowote unaohusiana na leseni za uchimbaji mdogo wa madini ya Jasi na wachimbaji wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. Nakushukuru. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia ameridhika. Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Same Mashariki.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi. Kwa sababu sehemu hizi mbili; Bendera na Mkomazi jambo kubwa wanalogombea ni mpaka kati ya Bendera na Mkomazi, ndiyo linapokuja suala la madini: Je, Serikali hamuoni ni muhimu sana Mkuu wa Mkoa akafika pale akaweka vizuri mpaka ule ili hili tatizo lilitozungumzwa hapa ndani sasa hivi lisiendelee kutokea? Ahsante.

SPIKA: Haya tulikuwa na migogoro ya mipaka ya Wilaya kwa Wilaya, sasa huu mpaka wa Kata kwa Kata ambapo maana yake kuna vijiji na vijiji.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, ni mpaka wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Tanga, uko kati ya Bendera na Mkomazi.

SPIKA: *Okay!* Ni mipaka ya mikoa!

MHE. ANNE K. MALECELA: Ndiyo.

SPIKA: Haya, Mheshimiwa Lukuvi umeelewa.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Kule kote ambako

kuna migogoro ya tafsiri za mipaka sisi tunahusika. Kwa hiyo, hatutasita kwenda kutafsiri ardhini tafsiri ya mipaka iliyoinishwa na mwenye mamlaka. Tunazo *GN*, tutaifanya kazi hiyo. Nitaomba tu Mheshimiwa Kilango anipe maelezo ya ziada ili tuunde timu yetu ya pamoja ikafanye kazi hiyo. Hiyo ndiyo kazi yetu ya kutafsiri *GN* zilizoainisha mipaka na mwenye mamlaka. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti, Mheshimiwa Mrimi, nilikuona mahali, uliza swali lako.

Na. 46

**Kupunguza Viwanja vya Ndege Ndani ya
Hifadhi ya Serengeti**

MHE. JEREMIAH M. AMSABI aliluliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza Viwanja vya Ndege ndani ya Hifadhi ya Serengeti kwa kujenga Uwanja wa Ndege katika Mji wa Mugumu nje kidogo ya Hifadhi pamoja na kukamilisha ujenzi wa barabara ya lami ya Makutano Sanzate Natta na ile ya Tarime Mugumu Natta?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri na Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa lengo la kujenga Kiwanja cha Ndege cha Serengeti katika eneo la

Mugumu, kitakachotoa huduma za usafiri ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Aidha, kiwanja hicho kitakapojengwa na kukamilika kitapunguza matumizi ya viwanja vya ndege ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwani ndege nyingi zitakuwa zikitumia kiwanja kitakachokuwa kimejengwa nje ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Makutano – Sanzate – Natta yenyе urefu wa kilometra 90, ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea na umegawanyika katika awamu mbili. Sehemu ya kwanza ni Makutano – Sanzate yenyе urefu wa kilometra 50; kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea na hadi Oktoba 2021 ujenzi ulikuwa umefikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2022. Aidha, sehemu ya pili ni Sanzate – Natta yenyе urefu wa kilometra 40; ujenzi kwa kiwango cha lami unaendelea. Hadi Oktoba, 2021 kazi za ujenzi zilikuwa zimefikia 7% na zinatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Barabara ya Tarime – Mugumu – Natta yenyе urefu wa kilometra 122.97 itajengwa kwa awamu. Zabuni kwa ajili ya kupata Mkandarasi wa kujenga sehemu ya Tarime - Nyamwaga yenyе urefu wa kilometra 25 zimefunguliwa mwishoni mwa Oktoba, 2021 na uchambuzi unaendelea ili kumpata Mkandarasi wa ujenzi. Serikali itaendelea na ujenzi wa sehemu iliyobaki kadiri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mrimi.

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni sote tumeona jitihada kubwa sana za Rais Samia za kuvutia watalii katika nchi yetu, lakini pia sasa hivi tayari Mkuu wa Mkoa wa Mara Mheshimiwa Ally Hapi, pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii walianza jitihada za pamoja, wameanza vikao vya kuona namna ya kujenga uwanja ule. Hii ni kuzingatia pia kwamba kuna

ushindani mkubwa kwa wenzetu, watu wa Masai Mara kule Kenya ambao wana-share ikolojia moja na Serengeti.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri nipate nafasi ya kukutana naye kwa mazungumzo maalumu kuona ni namna gani tutapata mwelekeo wa pamoja wa kuweza kujenga uwanja huu kwa viwango vikubwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, barabara hii ya Sanzate mpaka Natta, na ile ya Tarime – Mugumu – Natta, barabara hizi hazi-connect Makao Makuu ya Wilaya ya Serengeti pale Mugumu. Mwaka wa jana, 2020 aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano alitupa ahadi ya ujenzi wa kilometra 30. Kwa hiyo, namwomba sana...

SPIKA: Unasema Tarime – Mugumu – Natta, haifiki Mugumu tena!

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika, Tarime – Mugumu – Natta halafu kuna ile ya Makutano na Sanzate – Natta. Sasa zote hizi kwa jinsi ya ule mpango wa ujenzi, zitachukua muda mrefu kuja kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, tukawa tumemwomba aliyekuwa Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwamba kipande cha Natta – Mugumu kiweze kupewa fedha kijengwe haraka ili barabara ile ya Makutano – Sanzate – Natta sasa itoke pale Natta mpaka Mugumu. Halafu na ile inayotoka kule Tarime – Nyamwaga – Mugumu iweze kuungana nayo mapema zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lini Wizara inaweza kutekeleza mpango huu na ile ahadi ya Rais? Ahsante sana.

SPIKA: Yaani sijakuelewa, lakini wewe ndio Mbunge wa huko. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amsabi Jeremiah, Mbunge wa Serengeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza ameomba tufanye mazungumzo namna bora ya kupata fedha ya kujenga uwanja wa ndege wa Serengeti.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nitumie nafasi hii kusema kwamba kwa sasa pia Mheshimiwa Rais ameshatoa fedha za kutosha za kuanzia ujenzi wa uwanja wa ndege wa Musoma na mkandarasi ameshapatikana, yupo *site* anafanya kazi, lengo ni kuboresha huduma katika Hifadhi ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, tangu anazungumza Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, walifanya kazi nzuri sana pamoja na Wizara ya Maliasili ya kufanya mjadala. Sisi tunaona kwamba uwanja ambao walipendekeza kujenga ni uwanja ambao unamilikiwa na TANAPA na Halmashauri, ambao ni uwanja mdogo. Sisi tunataka tujenge uwanja mkubwa wa Kimataifa ili tushindane na wenzetu wa Kenya ambao wanajenga kule Masai Mara uwanja mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumewaelekeza watu wa Maliasili Uongozi wa Mkoa wa Mara watuletee andiko maalumu, tukae pamoja na Wizara ya Ujenzi, tujenge Uwanja wa Ndege wa Kimataifa ili tusigawane watalii wanaotaka kupata huduma katika mbuga yetu ya Serengeti. (*Makofii*)

SPIKA: Huo uwanja mnataka kujenga wapi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, tunafikiria kujenga uwanja wa ndege Serengeti pale Mugumu, wanalo eneo pale la kutosha.

SPIKA: Haya endelea.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, sawa, ahsante.

Mheshimiwa Spika, swal i pili, ni kweli kwamba barabara ya Sanzatte inajengwa na ameleta ombi la kilometra 30, tumepokea ombi hilo na linafanyiwa kazi. Wakati huo huo, kilometra 25 zinajengwa kutoka eneo la Tarime kwenda Serengeti ili wananchi wa eneo hilo waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, mawazo yote ni mazuri, lakini kupanga ni kuchagua. Kadri tunavyopata fedha za kutosha, barabara hizo zitakamilika kwa wakati ili huduma iweze kipatikana katika eneo la Serengeti. Ahsante. (*Kicheko*)

SPIKA: Ahsante sana. Nafikiri Mheshimiwa Mbunge mkutane na Mheshimiwa Naibu Waziri ili muweke picha zenu pamoja. Mkijenga uwanja wa ndege Mugumu, unaingilia wapi Serengeti?

MHE. JEREMIAH M. AMSABI: Mheshimiwa Spika,...

SPIKA: Aah, wala sisemi ujibu. *At most* uwanja utajengwa *Fort Ikoma* na ukijenga uwanja wa *Fort Ikoma* barabara zenu zote zinatoka Mugumu zinakuja Natta moja kwa moja, ina maana haiunganishi *Fort Ikoma*, mnaiacha katikati. Hebu yawekeni vizuri haya mambo kitalii, siyo vile mnavyoona ninyi. Iwe ni kwa faida ya utalii wa eneo lile, kwa sababu anapokuja mgeni hana haja ya kupoteza muda, inatakiwa *gate* ya Serengeti liwe karibu, anaingia, mambo yanakwenda. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara Mjini kabisa pale. Mheshimiwa Mtenga.

Na. 47

**Wananchi waliojiunga na Pride kwa ajili ya
kupata Mikopo Mmtwara Mjini**

MHE. HASSAN S. MTENGA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itashughulikia urejeshwaji wa Fedha za Wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini ambao walijiunga na *Pride* kwa ajili ya kupata mkopo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo tuko Fedha na Mipango, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Mwigulu Nchomba, tafadhalii.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, Mbunge wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama inavyokumbukwa kuwa kulikuwa na shauri mahakamani liliofunguliwa mwaka 2016 kuhusu umiliki wa Kampuni ya *Pride*; baada ya kukamilika kwa shauri hilo na kutolewa hukumu tarehe 11 Novemba, 2018 kuwa Kampuni ya *Pride Tanzania* ni mali ya Serikali, Serikali ilifanya tathmini ya hali ya kampuni na kufuatiwa kwa ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutambua kuwa mali na madeni ya Kampuni hiyo ambapo taarifa ilionesa kuwa Kampuni hiyo ina madeni makubwa kuliko mali zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa hiyo, Wizara ya Fedha na Mipango imeielekeza Ofisi ya Msajili wa Hazina kusimamia ufilisi wa Kampuni hiyo kwa kufuata taratibu za ufilisi wa Makampuni. Hivyo, kwa sasa Kampuni ya *Pride* ipo katika hatua za ufilisi. Madai yote yanayohusu Kampuni hiyo yatashughulikiwa kwa kufuata taratibu za ufilisi.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge Mtwara Mjini, swalii la nyongeza.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa shauri hili lilizungumzwa toka mwaka 2018 na Ofisi ya Msajili Hazina wakapewa jukumu la kulisimamia tuna miaka zaidi ya mitatu sasa hivi imeshapita: Je, ni lini tutaelezwa kwamba shughuli hii itakuwa imemalizika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Wananchi wa Mtwara ambao wanadai zaidi ya shilingi milioni 250: Ni lini Mheshimiwa Waziri atakuja kuzungumza na wananchi wa Mtwara ili waelewe mustakabali mzima wa fedha zao ambazo zimepotea mpaka sasa hivi haijulikani watalipwaje? (*Makofii*)

SPIKA: Makatibu, baridi hii ya leo ni kali sana. Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mtenga kwa kufuatilia sana masuala ya wananchi wake wa Jimbo la Mtwara. Mara kwa mara akija ofisini anaafuatilia masuala yanayohusu wananchi wa Mtwara katika sekta mbalimbali na anatumia vizuri uzoefu wake wa kuwa Katibu wa Mkoa wa Chama na maeneo tofauti tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza kwamba jambo hili limechukua muda, ni kweli lilichukua muda kwenye hatua za awali kwa sababu lilipokuwa kwenye ngazi za kimahakama, hatua nydingine hizi zisingeweza kufanyika, lakini baada ya kuwa shauri hilo limeshaamuliwa na Mahakama, kwenye hizi hatua nydingine, zinaweza zikafanyika kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie kwamba wananchi wake watapata uhakika haraka tu. Naamini nami nitapata uhakika kutoka kwa Msajili wa Hazina ili niweze kumuarifu makadirio hasa ya muda aliyokuwa anataka aujue kuwa ni lini?

Mheshimiwa Spika, hili la pili kwa ridhaa yako, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tukishamaliza Bunge tutapanga utaratibu ili tuweze kuwaandaa wahusika hao, nami niweze kufanya ziara kuweza kuwaelimisha nikiwa tayari na majibu ya uhakika kutoka kwa Msajili wa Hazina kuhusu kipindi ambacho kitatumika kuweza kuhakikisha kwamba hatua hizo za kiutawala zitakuwa zimekamilika.

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Tunza Malapo, uliza swali lako.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba tu Serikali inieleze, inakuwa wapi mpaka matatizo haya yanatokea? Uizingatia kwamba watu wengi wanaoweka na kukopa kwenye hizo taasisi ni watu wa kipato cha chini; Serikali inakuwepo inaona jambo linaendelea mpaka linakua, wanakuja kunyang'anya ama kuchukua, watu wanaathirika. Kumbuka mambo ya *DEC*, ilikuwa hivi hivi. Leo *PRIDE* iko hivi hivi. Nataka nijue, Serikali inakuwa wapi mpaka inaacha mambo haya yanafikia hapo wananchi wanaathirika ambapo wengi wao ni wakipato cha chini? Nakushukuru. (*Makof*)

SPIKA: Swali la Mheshimiwa Tunza hilo. Mheshimiwa Tunza Malapo, anasema Serikali inakuwaga wapi? Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu tafadhali. (*Kicheko*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kazi ya Serikali kutoa miongozo na kusimamia hizi taasisi. Kwa upande mmoja Serikali ni pamoja na wananchi inapofika masuala ya kifedha kwa sababu taasisi zote za kifedha zinakuwa na mikutano yao ya kila mwaka, lakini mara nyingi sana wananchi wetu wakishaweka fedha kwenye maeneo haya ya kibenki, hawafuatillii sana mienendo ya kifedha kwenye maeneo walikoweka. Wakati Serikali inafanya yale mambo ya kiutawala, ni wajibu wao pia kuangalia mwenendo wa taasisi yao ambako wameingia mkataba na taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, rai yangu, kwanza wananchi watumie taasisi za kifedha ambazo hazina mashaka mashaka. Tuna mabenki yanaendelea kuenea katika maeneo mengi, watumie mabenki ambayo yako *accredited* na Serikali, wasitumie taasisi zile ambazo zina mashaka mashaka, lakini hata taasisi zile ambazo ziko *accredited* kama ambavyo masharti ya kifedha yanasema, wanapokuwa na mikutano ya mwaka ya taasisi hizo,

wachukulie umuhimu kufuatilia mienendo ya taasisi hizo ambazo wameingia mkataba nazo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Tunza Serikali ipo. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, nimekuona.

Na. 48

Kuwezesha Mradi wa Regrow Kuanza – Kihesa

MHE.COSATO D. CHUMI aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatoa *GN* kuwezesha Mradi wa *Regrow* kuanza rasmi katika eneo la Kihesa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utalii Mheshimiwa Mary Francis Masanja, nimekuona.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa tangazo la awali la siku 90 la nia ya kubadilisha matumizi ya sehemu ya eneo la Msitu wa Kihesa Kilolo, tarehe 9 Julai, 2021. Siku 90 tayari zimekwisha, hivyo Serikali imepanga kutoa *GN* ya Msitu wa Kihesa, Kilolo mwezi Novemba, 2021. Naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

SPIKA: Sasa Mheshimiwa Chumi unauliza swali mgongoni kwa Waziri! Basi endelea hapo hapo, nimekuruhusu. (*Kicheko*)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona.

SPIKA: Mheshimiwa Chumi unauliza swali mgongoni kwa Waziri? Basi endelea hapo hapo, nimekuruhusu. (*Kicheko*)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza naishukuru Serikali kwa kuifanya Iringa kuwa kitovu cha utalii kusini, lakini mradi huu ambao *GN*hiyo imetangwazwa Julai, 2021 ulizinduliwa tarehe 12 Februari, 2018 na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassain akiwa Makamu wa Rais. Sasa swali langu ni moja tu kwa Serikali, je, inaridhika na *speed* ya utekelezaji wa mradi huu?

SPIKA: Maswali mengine magumu. Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili hebu jaribu, unaridhika?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu utakamilika kwa wakati. Nasema hivyo kwa sababu mradi huu una-cover maeneo manne ya Kusini mwa Tanzania ambako ndiyo unatekelezwa. Mradi huu kwenye maeneo haya ni pamoja na Hifadhi ya Nyerere, Ruaha, Udzungwa na Mikumi.

Mheshimiwa Spika, eneo analoliongelea Mheshimiwa Chumi ni eneo mojawapo ambalo ni ujenzi wa kituo mahususi kwa ajili ya kutunza *information* za masuala ya utalii. Hivyo, maeneo mengine mradi huu unaendelea ambapo mitambo mbalimbali imeshanunuliwa, magari lakini pia kuna viwanja vyatundege ndani ya hifadhi vimeendelea kukarabatiwa na miundombinu mingine mingi inaendelea kufanyika. Hivyo, eneo hili lilikuwa linasubiri tu *GN*weze kukamilika, lakini wakati huo huo tuna mshauri mwelekezi ambaye tayari ameshaanza zoezi na tumeshaanza kupokea ripoti. Kwa hiyo, nimtoe

wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakamilisha mradi huu kwa wakati bila wasiwasi. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana mtaona muda wetu wa saa moja tumeutumia vizuri na maswali yamekwisha kwa siku ya leo. Sasa niwatambulisse wageni wetu kama ifuatavyo:-

Tulionao kwenye *galleryya* Spika ni pamoja na Katibu Mtendaji wa Taasisi ya Umoja wa Maraisi wa Afrika kwenye mapambano dhidi ya Malaria - ALMA ambaye kiongozi wake tuko naye hapo *gallery* ndugu Joy Phumaphi, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka hii *ALMA* ilianzishwa kwa juhudni kubwa sana za Rais Mstaafu Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Kikwete na inasaidia sana katika kutoa fedha na kukusanya rasillimali fedha kwa ajili ya mapambano dhidi ya *malaria*, kwa hiyo tunashukuru sana ndugu Joy kuwa nasi. Yeye anatokea kule Botswana. (*Makofi*)

Tunaye Mshauri Mwandamizi wa Malaria wa *ALMA*, Dkt. Abraham Mnzava, ahsante na karibu sana. (*Makofi*)

Pia tunaye Meneja katika Ofisi ya *ALMA* hapa Tanzania Dkt. Adiel Mushi. Ahsante sana na karibu sana. (*Makofi*)

Nina wageni vile vile ambaeo ni Viongozi kutoka Benki ya *NBC*. Nianze na *NBC Managing Director*ndugu Theobald Sabi, karibu sana. Huyu ndiyo Mkurugenzi Mkuu wa *NBC* na kama mnavyojua mambo yao siku hizi hata ligi ile ya daraja la kwanza sasa wao ni *sponsor* wakubwa, hongereni sana *NBC*. (*Makofi*)

Wapo *Board Member* Dkt. Kassim Hussein; Ndugu Godfrey Malekano; na Ndugu Felix Mlaki; karibuni sana. (*Makofi*)

Yupo Mkurugenzi wa Biashara za kibenki ndugu Elvis Ndunguru; yuko *Head of Corporate Affairs*, ndugu William

Kallaghe; yupo *Head* wa *Private Banking*, Ashura Waziri; na yuko Meneja wa Branch yetu hapa Dodoma, ndugu Happiness Kizigira. Karibuni sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge ndugu zetu wa *NBC* wameandaa matembezi keshokutwa siku ya Jumapili mapema asubuhi, naamini baadhi yenu mnazo taarifa, wale ambao hamna taarifa, basi mnaweza mkajiandikisha kupitia Ofisi yetu ya Bunge ili tuweze kufanikishiwa kuhusu nyenzo za kufanya matembezi hayo ambayo yataongozwa na Makamu wa Rais Dkt. Mpango.

Naomba sana tushiriki siku hiyo mapema asubuhi, halafu tuweze kuwahi kuja kwenye semina yetu ambayo tutaitangaza baadaye kwamba utaratibu wake utakuwaje. Karibuni sana *NBC Board* na karibuni sana *ALMA*. (*Makof*)

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mwongozo.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Kanuni ya 76 ukiniruhusu nitasoma.

SPIKA: Endelea.

MHE. NUSRAT S. HANJE: "Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba "Mwongozo wa Spika" kuhusu jambo ambalo limejitokeza Bungeni mapema, ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaluhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu na kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye, kadri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 Bunge hili Tukufu lilitunga sheria iliyoitwa Sheria namba 12 ya Baraza la Vijana la Taifa ya mwaka 2015. Imepita miaka sita tangu Bunge hili Tukufu litunge sheria hiyo, lakini pia tarehe 15 Juni mwaka huu Mheshimiwa Rais akiwa anaongea na vijana, Mkoa wa Mwanza alitoa maelekezo kwa Wizara inayoshughulika na

masuala ya vijana kuhusiana na kuangalia kwa upana na umakini suala la uanzishwaji wa Baraza la Vijana la Taifa.

Mheshimiwa Spika, imepita miezi minne tangu Mheshimiwa Rais atoe maelekezo hayo kwa wasaidizi wake, lakini mpaka sasa vijana wa Tanzania wapo kwenye giza nene kwa sababu hawajui imepitaje miaka sita bila kutekeleza sheria ambayo ilitungwa na Bunge hili ambalo linaheshimiwa na nchi hii, lakini bila kutekeleza maelekezo na maagizo ya Mheshimiwa Rais wakati anaongea na vijana wa Mkoa wa Mwanza kwa niaba ya vijana wote wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wako kwa ajili ya kulinda maslahi na heshima ya Bunge hili kwa sababu tunatumia pesa za walipa kodi kukaa kwenye kikao hiki cha Bunge na kutunga sheria ambazo kimsingi zinatakiwa zitekelezwe. Sasa naomba Mwongozo wako pia kuhusiana na kulinda heshima na hadhi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu itakumbukwa jana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, alifanya mkuutano na Waandishi wa Habari kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyoyatoa kuhusiana na watumishi walioondolewa kazini ambao yalitolewa hadharani Mei Mosi kama ambavyo maelekezo ya kuangalia kwa upana suala la Baraza la Vijana yaliyotolewa hadharani mbele ya vijana wa Mwanza kwa niaba ya vijana wa Tanzania. Kwa hiyo naomba Mwongozo wako kwenye jambo hili kwa ajili ya kulinda heshima ya Bunge hili kwa maana ya kutunga sheria, lakini kulinda heshima ya Mheshimiwa Rais. Ahsante.

SPIKA: *Issue ni nini hasa Nusrat kwa kifupi. Issue ni nini?*

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, *issue ni kushindwa kutekelezwa kwa sheria iliyotungwa kwa maana ya kuanzisha Baraza la Vijana la Taifa ambayo imepita miaka sita tangu itungwe na hajatekelezwa, lakini hata Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo hadharani na mpaka leo tupo gizani*

hatujui nini kinaendelea kuhusiana na Baraza la Taifa la Vijana.

SPIKA: Ni Waziri yupi ambaye unamlenga? Suala hilo la vijana.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, ni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Masuala ya Vijana na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Masuala ya Vijana, Bunge na Walemauvu.

SPIKA: Ok! Waziri wa Nchi kama una ufanuzi, tafadhalii.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii fursa. Kwanza nimwamble Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna kiongozi yejote ndani ya Taifa hili ambaye yupo kudhalilisha ama kumuaibisha na kumdhaliilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayupo. Naomba nimhakikishie sana kwamba Viongozi wa Tanzania wanayo heshima kubwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Sita Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Amiri Jeshi Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; taratibu zote za kutekeleza maagizo ya Rais huwa zinasimamiwa kwa misingi pia ya kimfumo ili kuhakikisha utekelezaji wa maagizo yote ya Mheshimiwa Rais yanatekelezwa ipasavyo kwa kuzingatia kwamba matokeo ya utekelezaji wa maagizo hayo yanakuwa kwa manufaa na ustadi mkubwa kwa wanufaika kuhusiana na maelezo hayo...

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, nitakupa nafasi uendelee dakika moja tu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, ndiyo.

SPIKA: Nitakupa nafasi, naomba dakika moja tu, nataka baada ya maelezo yako na kadhalika, Mheshimiwa Nusrat ulisoma mwenyewe kanuni hili jambo limetokea leo wapi. Kuna mahali limetokea hili jambo la vijana na kuunda baraza na kadhalika? (*Makof*)

Waheshimiwa tunaendelea. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

(Majadiliano Yanaendelea)

MWENYEKITI: Tunaendelea na uchangiaji, tuzingatie dakika zetu 10 ni chache. Kwa hiyo ukijielekeza moja kwa moja itakuwa imetusaidia zaidi. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya na Mheshimiwa Halima James Mdee, ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu. Jambo la kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kuiongoza nchi hii na jinsi anavyoiweka kwenye ramani ya dunia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia hotuba aliyoitao katika Umoja wa Mataifa, lakini tumeshuhudia pia hotuba aliyoitao juzi; zote zimeleta matunda mazuri sana

katika nchi yetu. Kwa kweli tunampongeza sana sana. Pia tunampongeza Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na pia Rais wa Zanzibar kwa namna wanavyoshirikiana katika kuziongoza nchi zetu hizi mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuleta Mwongozo huu wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2022/2023. Kwa kweli ni mwongozo mzuri na ambao kwakweli nadhani tukiujazilizia jazilizia, basi unaweza ukaleta matunda mazuri sana. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Kamati ya Bajeti kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuchambua Mpango huu, Mkakati huu na *Frame Work* hii na mpaka hapa walipofikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya msingi ambayo kwa kweli yamezungumzwa katika Mpango huu na nimefurahi sana kuona dhima ilioandikwa katika Mpango huu ambayo imeandikwa kwamba Kujenga Uchumi Shindani na wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Dhima imekaa vizuri sana, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, isipokuwa Dira bado sijaiona kwenye hii labda Mheshimiwa Waziri angeiweka na Dira, nayo ikakaa vizuri, *short and clear* itatuweka vizuri sana mahali pazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yapo mambo ya msingi ambao Mpango wowote, Mwongozo wowote tunaoutoa na Mpango tutakaokwenda kuutekeleza, yapo mambo muhimu ambayo lazima Mpango wowote utakaokuja uende kuyajibu. Tutapenda Waziri atakapokuja na Mpango huo basi majibu halisi yapatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, jambo la kwanza ni umaskini uliokithiri katika maeneo mengi, Tanzania sasa hivi kuna umaskini mwingu. Sasa *framework* hii ituelekeze namna tutakavyoenda kukabiliana na umaskini wa nchi hii, umaskini wa watu walio wengi tutakavyoondokana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni suala la ajira. Ajira kwa vijana wetu, ajira katika nchi hii ambayo imekuwa ni tatizo kubwa. Sasa lazima *framework* hii ituelekeze namna tutakavyoweza kutatua tatizo la ajira katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ni ukuaji mdogo wa uchumi. Uchumi wetu hauendani na rasilimali tulizonazo, ukuaji wake bado upo chini sana. Sasa ni namna gani tunaenda kujipanga, tunakuja na mipango gani, tunatekeleza vipaumbele vipi na kwa namna gani ili uchumi ukue kwa kasi kubwa inayolingana na rasilimali tulizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hayo ni mambo muhimu ambayo tutapenda yawepo katika mpango ambao tunategemea uje. Kuna teknolojia duni ambayo imekuwepo katika nchi yetu, huduma duni katika maeneo mengi, lakini uongozi usiokuwa na maono katika baadhi ya maeneo. Sasa hivi Rais wetu na viongozi wa juu wana maono mazuri sana, mawaziri wana maono, lakini tuna tatizo la uongozi kutoka kwenye ngazi ya kati na kushuka chini. Sasa hili lazima tuliangalie vizuri, namna tutakavyoliweka vizuri ili sasa mambo yaende vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo pia tatizo la mapato kidogo ya Serikali. Ukiangalia mapato yetu ya Serikali sasa hivi makusanyo kwenye upande wa kodi ni asilimia 13 ya *GDP* na Mpango sasa hivi unaelekeza kwamba *framework* hii tutaenda kukusanya asilimia 16 ya Pato la Taifa. Sasa nadhani bado tupo chini ukilinganisha na nchi zingine zilizoendelea na nchi za wenzetu zinazoendelea kwa *speed* kali sana. Kwa hiyo ni muhimu tukayaangalia haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeangalia uwiano wa ukuaji wa mchango wa Sekta mbalimbali katika uchumi wa Taifa letu. Nimeangalia kwa mfano ujenzi, ilikuwa kwa asilimia 9.1 na imetoa mchango kwenye pato la Taifa kwa asilimia 14.4; lakini ukichukua Uchukuzi imekuwa kwa asilimia 8.4 na imechangia kwa asilimia 7.5 kwenye pato la Taifa; Madini ilikuwa kwa asilimia 6.7 na imechangia kwa asilimia 6.7.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya kwenye huu Muongozo haijaonyesha kilimo kilikuwa kwa asilimia ngapi? hili halijaonyeshwa, lakini imeonyeshwa mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa ambao ni asilimia 26.9. Sasa kilimo kinatoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa, lakini kilikuwa kwa kiwango gani na tuweke mikakati gani ili kilimo kikue kifiki katika kiwango tunachokitaka, hili nafikiri ni muhimu tukaliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia viwanda, biashara vyote hivi vimeonyeshwa mchango wake kwenye pato la Taifa, lakini vimekua kwa kiwango gani ili tutoke hapo sasa, Mpango utuelekeze tunataka tufike asilimia ngapi ya ukuaji ili tufikie malengo yetu, bado Mpango huu haukuweza kueleza. Sasa nafikiri hayo ni mambo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia vile vile uwiano wa ugawaji wa rasilimali ambao tunaenda kuufanya sasa. Sekta zipo kama tatu; kuna Sekta za Uzalishaji ambazo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hii. La pili, kuna Sekta za Biashara na Huduma na sehemu ya tatu ni Huduma za Jamii. Sasa katika uzalishaji wote, lazima tuuangularie katika Mpango huo na katika Mpango unaokuja tuone rasilimali zinaenda kuwekeza kwa asilimia ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo swalı ambalo tunajuliza ni kiasi gani rasilimali zitatengwa kwenda kwenye Sekta za Uzalishaji na hasa kilimo ambacho kinaajiri watu wengi ambapo kwenye kilimo hapo ndiyo tunapata chakula chote, fedha za kigeni na wananchi wetu wanapata ajira yao, lakini ndiyo tunapata ajira nyingi kwa sababu ndio tunapata malighafi zote za viwandani, uchumi wetu kwa kiwango kikubwa unategemea kilimo. Sasa ukikichukua kilimo kwa mapana yake ndiyo unaweza ukatatua hata tatizo la umaskini na tatizo la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namna gani tunaenda kufanya hilo ili kusudi tuone sasa sekta inatengewa kiasi gani, asilimia ngapi inatengewa kwa ajili ya kwenda kwenye sekta za uzalishaji, zikiungana na Sekta ya Uvusi, Sekta ya Ufugaji,

Sekta ya Madini, Viwanda, Utalii na Mazingira na hizo ndiyo sekta za uzalishaji, rasilimali kiasi gani zinaenda kutengwa kwa ajili ya kwenda kuongeza uzalishaji kwenye maeneo hayo. Tukiongeza uzalishaji kwenye maeneo hayo maana yake hata eneo la biashara litakaa vizuri, biashara itakaa vizuri, mambo mbalimbali ya biashara yatakwenda vizuri, lakini ndipo huduma za jamii tutakapokwenda kwenye maji, elimu, afya, ushauri na utafiti yatakaa vizuri. Sasa lazima tuwe na jedwali lile linaloonyesha mgawano wa hizo rasilimali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tumefika mahali sasa tuweke malengo shabaha. Shabaha za kila sekta, tunataka sekta ya kilimo ikue kwa asilimia ngapi, ichangie kwa asilimia ngapi? Ili tunapofanya kazi tukajipime kwa kiwango hicho. Kama ni ufugaji tufanye hivyo, kama ni biashara tufanye hivyo, kama ni huduma tufanye hivyo. Basi nafikiri hilli litatusaidia sana katika kuweza kuimarisha ukuzaji wa uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naangalia mambo muhimu, nchi ya kwetu ndiyo pekee ina bahari, ina maziwa, bandari pale, hivi tutaimarishaje? Kwenye kilimo, upatikanaji wa mbegu. Sasa hivi hali ni mbaya, mbegu sasa hivi nimesikitika sana, mpaka leo tunapoongea mwezi Novemba Serikali bado haijatangaza hata bei za mbolea, haijatangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezoea huwa wanatutangazia bei elekezi. Tunaponunua mbolea kwa mfuko wa pamoja huwa kunakuwa na bei elekezi, mpaka leo hazijatangazwa. Tunakwendaje kuzalisha, wakulima wa nchi hii wanakwendaje sasa kuzalisha, ambayo itaathiri kwa kiwango kikubwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, nilidhani kwamba hilo ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri angeliangalia waone kitu ambacho kinaweza kufanyika ili kiweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia hali ya uchumi sasa hivi, kwa mfano mazingira yamebadilika, mvua hazijanyesha. Kule Mikoa ya Mbeya, Songwe, tunategemea sana mvua za mwezi Septemba na Oktoba kwa ajili ya zao

la kahawa. Sasa hivi hazikunyesha, zimeanza kunyesha mwezi Novemba. Maana yake maua yote ya kahawa yameshaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwaka mzima mwakani hatutaweza kupata kahawa ya kutosha. Sasa mkakati tunauwekaje ili kukabiliana na hii hali. Kwa hiyo, ninadhani ni maeneo muhimu sana ya kuyaangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie Reli ya *TAZARA*, itachangiaje kwenye uchumi. Siyo tu suala la kwamba hii reli inamiliikiwa na nchi mbili, suala ni kwamba tunaongezaje mabehewa ya kuweza kusafirisha mizigo mbalimbali ili hii treni isaidie katika kukuza uchumi wa nchi yetu, hata kuishia pale mpakani tu. Tutajengaje pale kituo bandari kavu ili mizigo kutoka Dar es Salaam ifike pale nchi za *SADC*waje kuchukulia eneo hilli. Nafikiri ni kitu ambacho lazima tukiangalie vizuri.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga. Nilikutaja Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, na Mheshimiwa Halima Mdee jiandae.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Lakini nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza sana Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kwamba Corona ilikuwa ni janga kubwa lakini mama yetu amekuwa jasiri sasa hivi tuna chanjo Tanzania. Wote tunatambua kwamba Corona imeleta madhara mengi lakini mama yetu ame-*fight* akapata fedha za UVICO kutoka *IMF* na sasa hivi tuna fedha za kutosha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kwamba Tanzania ilianza kusahaulika. Mama yetu sasa hivi anaifungua, sasa hivi Tanzania inajulikana nchi za nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kumpongeza sana ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi ambayo wanaifanya. Nikushukuru sana Waziri kwa kazi mnayoifanya na kuleta rasimu ya huu mpango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina mambo matatu ambayo ninapenda kuishauri Serikali. Jambo la kwanza, ninapenda kuishauri Serikali kwenye mfumo wa kukamilisha miradi mikubwa ya maji; la pili, ninapenda kuishauri Serikali kuhusu huduma za afya, hususan *paradox* iliyopo kati ya zahanati na vituo vya afya; jambo la tatu, ninapenda kuishauri Serikali kuhusu mfumo mzuri wa kutoa mikopo ya elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu, mama Samia Suluhu Hassan. Kwa upande wangu mimi Jimbo la Manyoni Mashariki nina mradi mkubwa sana wa maji wa Kintinku – Lusilile wa takribani bilioni 11, mpaka sasa tumepewa takribani bilioni tano. Na mwaka huu wamenitengea bilioni 2.4 na juzi hela za UVIKO ametupatia takribani milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha huu mradi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la miradi ya maji nina hoja takribani tatu. Hoja ya kwanza ni kwamba tuna miradi mikubwa ya maji lakini tunatumia muda mrefu sana kuikamilisha. Nitatolea mfano mdogo wa mradi wangu wa Kintinku; mpaka sasa hivi *tumesha-spend fifty percent* ya bajeti ya *eleven billion. Ile fifty percent* imeshakaa zaidi ya miaka mitatu. Hiyo ni *sunk cost*, maana yake kuna *wear and tear* ambayo inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushauri kwenye hili. Cha kwanza, natamani kuona ni jinsi gani Wizara inaweza ikaja na *modality* mpya ya kuhakikisha kwamba

tunakamilisha hii miradi ya maji kwa wakati. Ninapenda kumshauri Waziri mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Nchi za Malaysia, Uturuki, hata Indonesia wanachofanya wameingia kwenye *Public Private Partnership* na *manufacturers* wa mabomba. Wanachofanya kwa sababu sisi tunajua kwamba tuna changamoto ya ku-raise hela kwa kutumia *taxation*, tunahitaji ku-tax ili tu-spend, kinachofanyika hapa, Serikali inaingia kwenye *long-term agreement* na *manufacturers* wa mabomba, *then* tunakuwa tunawalipa by *installments*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo tutakuwa na uhakika kwamba tunaweza tukakamilisha utekelezaji wa hii miradi ya maji ambayo kwa kweli inaweza ikawa na *impact* kubwa sana. Na kwa kupitia hilo vilevile tunaweza tukaweka *incentive*. Tunaweka *incentive* vipi; *incentive* ya kwanza tunaweza tukawa-exempt hawa *manufactures* kwa sababu wana-import raw material/kutoka nje, wawe na zero tax kwenye importation ya raw material. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hii vilevile ita-facilitate viwanda vyetu vya ndani vitakuwa, tutakuza ajira, lakini vilevile tutapunguza ile profit margin ambayo wanaweza wakai-set kwa sababu ya ile payment schedule ambayo tunaweza tukawa tunawalipa hawa *manufacturers*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye hili ni kwamba kama tutaenda na huu mfumo wa kutumia *private sector* waweze kuingia hiyo *long-term agreement* na Serikali, bado tunaweza tuka-opt kutumia ile force account kwa sababu tayari tutakuwa tuna uhakika wa kupata mabomba, tuna uhakika wa kupata fittings na tunaweza tukatumia force account ili kuhakikisha kwamba tunapunguza tatizo la kutokamilisha miradi kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu utaisaidia Serikali kukamilisha miradi mikubwa ya maji ukiwepo Mradi wa Kintinku – Lusilile ambao sasa hivi ni mradi wa zaidi ya miaka

15, bado tunasuasua kuukamilisha. Nina imani kabisa kwamba *approach* hii itakwenda kusaidia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushauri upande wa afya. Mimi nitumie nafasi hii kumshukuru sana Rais. Sisi kwa upande wa Jimbo la Manyoni Mashariki kwanza ametupatia milioni 250 za fedha za tozo ambazo tunakwenda kukamilisha Kituo cha Afya cha Chibumagwa, lakini vilevile tunaanza ujenzi wa Kituo kipywa cha Afya cha Sanza. Mbali ya hiyo, kwenye hela za UVKO ametupatia takribani milioni 300, tunakwenda kujenga jengo la dharura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi nina ishu kubwa mbili upande wa afya. Ishu ya kwanza Sera yetu ya Afya ilikuwa inasema kwamba kila kata tunahitaji kujenga kituo cha afya, lakini kila kijiji tunahitaji kuwa na zahanati. Kulingana na uwezo wa Serikali nadhani suala la kujenga kituo cha afya kila kata sasa hivi siyo wazo ambalo ni *realistic*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri nini; la kwanza, mimi naomba nishauri kwamba hatuhitaji kujenga kituo cha afya kila kata, zaidi tunahitaji kujenga vituo vya afya vya kimkakati. Na hivi vituo vya afya viwe *clustered* ili Serikali iwe kwanza na uwezo wa kupeleka watumishi pale, lakini iwe na uwezo wa kupeleka vifaa, lakini vilevile tutakuwa na uwezo hata wa kusaidia...

MWENYEKITI: Kengele ya kwanza hiyo.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la zahanati; zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wanaishi vijijini. *Demand* kubwa upande wa afya ipo kwenye zahanati kuliko iliyopo kwenye vituo vya afya. Vituo vya afya ni *referral point*, mtu akishindwa kwenye zahanati anakuwa *referred* kwenda kwenye kituo cha afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo najua utaratibu wa Serikali ni kwamba kila mwaka tunatenga takribani zahanati tatu kwa kila jimbo. Kwa upande wangu na maono yangu naona kwamba zahanati tatu kwa kila jimbo ni chache sana,

na kwa sababu tunataka kuhakikisha tunafikisha huduma za afya karibu na wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni nini? Kwanza tunahitaji ku-*invest* zaidi kwenye zahanati tuongeze zahanati sasa kutoka tatu kwenda angalau sita kila jimbo kila mwaka, lakini kama nilivyoshauri kwamba tutakuwa na zile *clustered health facilities* ambazo sasa angalau kata tatu zitajengewa kituo cha afya kimoja ili ziwe *referral points* kwa ajili ya wale wanaotoka kwenye zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la mikopo ya elimu ya juu. Katika wiki mbili hizi Wabunge wengi tumepokea simu nydingi sana za vijana wetu ambao wamekwenda vyuo vikuu, na katika hili niseme bado ule mfumo wetu wa *means testing* wa kuwachuja vijana ambao wana uhitaji mimi nauona bado una mapungufu makubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili niseme kwa sabbau gani; bado tunapata simu nydingi za vijana wetu ambao wanatoka kwenye maeneo yetu ambao tunajua kabisa ni watoto wa maskini lakini bado hawajapata mikopo. Na tatizo liliopo vilevile ule mfumo ni *very bureaucratic*, mtoto wa kijiji ambako mtandao haujafika anatakiwa *a-upload, a-apply* na aweke *documents* zote kwenye mfumo. Mimi nashauri mfumo huu ufanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ni marekebisho gani nashauri; kwanza nashauri tuachane na huu mfumo wa *means testing*. Na ningeshauri mambo matatu; la kwanza, tuje na mfumo wa *category*, tuwe na *categories* tano, *category* ya kwanza kwa wale wanafunzi waliosoma shule za Serikali *form four* na *form six* hawa ningeshauri wapewe mkopo asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *category* ya pili ni wale wanafunzi waliosoma kidato cha nne...

MWENYEKITI: Kengele ya pili hiyo.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi nikushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Nikiwa sehemu ya Wajumbe wa Kamati ya Bajeti nitachangia mambo kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Kamati ya Bajeti imependekeza kwamba Shirika letu la Ndege (*ATCL*) liangaliwe ili liweze kuboreshwa zaidi ili liweze kufanya kazi kwa ufanisi. Lakini nikiwa naunga mkono hiyo hoja nitazungumza mambo kadhaa kwa sababu lazima tujue tulikotoka ili kuweza kujua tunakwendaje mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa *ATCL* ina madeni yenye thamani ya bilioni 472, thamani ya mali za *ATCL* ni bilioni 256. Tafsiri yake ni kwamba *ATCL* ina mtaji hasi wa shilingi bilioni 216. Na unapokuwa na mtaji hasi tafsiri yake ni kwamba umekufa tu lakini upouopo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine, malengo ya biashara ya *ATCL* wakati tunaifufua, na watu tulizungumza tukasema tunaingiza fedha lakini wakati tunaingiza hizi fedha nydingi lazima tuhakikishe shirika liko tayari, Taifa liko tayari, wananchi wako tayari. Zikapigwa porojoporojo hapa, mambo yakaenda, tumefika hapa tulipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo yalikuwa bilioni 600, malengo ya kibiashara, kutengeneza, wamefanikiwa bilioni 157; asilimia 24 tu ya lengo. Naunga mkono tui-boost, tuifufue, sikatai, ila lazima tujue tulitoka wapi, tumeteleza wapi, tunakwenda wapi na tusifanye maamuzi yanayohusu pesa za Umma kimihemkohemko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa 2015/2016 – 2021/2022 malengo kwa *ATCL* peke yake ilikuwa ipewe triliioni

3.39, mpaka sasa imefanikiwa kupata trillioni 1.9 kwenye hiki kipindi cha miaka mitano. Sasa nikiwasikiliza ndugu zangu hapa wanazungumza kilimo, mkongwe hapa, tumepeiga hizi *sound* za kilimo tu kwenye mipango, tumezipiga yaani hawasikii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilimo ambachao tunajua kinachangia asilimia 26 ya *GDP*, Pato la Taifa, yaani kwenye zile trillioni 163, kilimo anachofanya mkulima mmojammoja kwa *support* kiduchu ya Serikali inachangia trillioni 44. Tumeipenda sana tumeipa bajeti 294, ukija utekelezaji utakuta wamebajeti bilioni 100, ikizidi sana bilioni 60. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndugu zangu hawa wa *ATCL* wamepigwa trillioni zao 1.9, ukiuliza hivi inachangia pato la Taiifa kiasi gani, sidhani kama asilimia moja inafika. Kuna wenzangu na mimi hapa walikuwa wanajifanya, oh, wanaleta watalii; ndege gani ya *ATCL* inatoka Mpanda inaleta watalii Bongo? Nendeni Kilimanjaro pale, nendeni huko Mwanza muangalie kuna ndege gani ya *ATCL* inaleta Wazungu kutoka Ulaya kuja Tanzania kwa utalii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia safari za ndani ufanye *analysis* ujue kama hizi ndege zina mchango kwenye utalii. Nazungumza tujitathmini. Tujitathmini. Sina nia mbaya. Kwa sababu midude iko hapa, yalikuja 11 yameshalipiwa mengine sasa hivi tunaambiwa 16 halafu hadi kuelekea ule uchaguzi zitatimia 19. Yaani hili ni eneo pekee ambalo mtatekeleza bajeti kwa asilimia mia lakini *output* ikoje, *productivity* ipo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, hili shirika tunavyozungumza limepewa asilimia 600 ya bajeti ya kilimo kama ikipelekwa kwa ukamilifu. Hebu tujiulize tu, hiki kilimo hiki kingepewa hata trillioni moja, ingekuwa *boosted* kwenye mifumo ya umwagiliaji. Hatusemi muwape hela mfukoni, wakulima wetu wanahitaji miundombinu wezeshi, wanahitaji kupewa *channels* za masoko. Kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi mna-*enjoy* nini kwa mfano. Ndiyo, tuna ndege 19, taarifa ya *ATCL* wenyewe wanatuambia eti wanahudumia abiria 60,000; halafu eti wamepungua kwa sababu ya *Covid* mpaka 11,000 halafu watu wazima tunakaa hapa tunapitisha mpango. Tumetoka kulipa bilioni 500 juzi, ndege nyingine mpya tano. Hatuoni aibu, tupo tu, hatuoni aibu.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu... msinichanganye jamani, acheni nina uchungu.

MWENYEKITI: Ni upande gani hiyo taarifa? Endelea, nakuruhusu. Nimekuona Mheshimiwa Shigongo.

TAARIFA

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Mdee, namheshimu kwa sababu ni mtu anayeelewa vitu vingi lakini natofautiana naye sehemu moja tu; katika biashara kuna suala linaitwa *trading* na *investing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapo-*trade* unachukua kitu unaauza na unapata faida *immediately*, tunapozungumzia *investing* kuna *incubation period* ya kusubiri ndiyo uanze kupata faida. Itachukua muda *ATCL* ianzé kutupa faida, lakini *finally ATCL will pay*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya ndege siyo *trading* ni *investing*. *Let's be patient, ATCL itatulipa.* (*Makof!*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo unaipokea Mheshimiwa Halima?

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shigongo naye anajua biashara mwenyewe hayuko vizuri sasa hivi, kwa hiyo atulie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni nini? Sipingi ndege kununuliwa, nappinga maandalizi. Nitawasomea kitu kimoja hapa, taarifa ya *ATCL* wenyewe, wanasema hivi; Serikali inakabiliwa na mashauri ya kesi zilizokwishaamuliwa mahakamani, utekelezaji wa maamuzi ya kesi hizo haujafanyika na hivyo madeni haya yanaweka mali za Serikali katika hatari ya kukamatwa kwa ajili ya kukazia utekelezaji wa hukumu. Hatari hii inafanya tuogope kupeleka ndege zetu nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria sisi watu wazima tumenunua ndege, tumetumia triliuni 1.9, tunaogopa kulipa madeni ya kesi za Wazungu huko kwa hiyo ndege tuko nazo nyumbani. Hivi hizo ni akili ama nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema tunapenda sana shirika letu changamoto illyopo kulikuwa hakuna *business plan*, ndio maana leo madeni ya *ATCL* mwaka 2014 ilikuwa ni bilioni 74, ilikuwa haifiki hata milioni 100 mwaka 2014/2015, leo bilioni 400 pamoja na ku-*inject 1.9 trillion*, hivi hamuoni?

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, wanao mtindo wa kuninyima michango yangu nikichangia, ninashtaki kwako leo ili wanipe, tunasaidia Nchi jamani hatutafutani mchawi hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Halima. Mheshimiwa Godwin Kunambi tafadhali, atafuatia na Mheshimiwa Pindi Hazara Chana.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii, lakini mchango wangu utajielekeza sana nianze kwenye eneo la *actorswa Mpango wenyewe*. Maana kupanga jambo moja, kutekeleza jambo la pili, mipango yetu ni mizuri sana na kila mwaka tumekuwa tukiwa na mipango mizuri ya namna hii. Lakini njielekeze

kwa *actors* wa Mpango huu yaani watekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa namna ambavyo sekta ya Utumishi wa Umma inapimwa. Taasisi zetu za Serikali zinapimwa kwenye uwajibikaji. Ukisoma Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura Na. 298 imeeleza kuhusu namna gani Watumishi wa Umma wanapimwa yaani kuna *OPRAS* inaitwa *Open Performance Review and Appraisal (OPRAS)*. Mimi nimehudumu na nilikuwa Mtumishi wa Umma kama Mkurugenzi wa Jiji kwa kipindi cha miaka minne na miezi kadhaa, hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo gumu sana kwenye kumpima Mtumishi Umma ni kwenye ujazaji wa *OPRAS*. *OPRAS* ni formula tu na kama utaratibu ambao tumeuzoea hizi *business as usual*. Kumpima Mtumishi wa Umma au Taasisi za Umma kwa kutumia *OPRAS* nadhani jambo hili limepitwa na wakati. Ukitazama eneo hili la *OPRAS*, ukitazama nchi zingine kwa mfano wenzetu Rwanda, Kenya na nchi zingine wanatumia *Performance Contract* kwenye kuwapima watumishi wake. Leo hii nikiuliza hapa bahati mbaya najaribu kuangalia Waziri wa Utawala Bora, Utumishi wa Umma sijamuona, nikiuliza hapa ni watumishi wangapi nchini wameshushwa vyeo kwa kupimwa *performance* yao, si tuna *OPRAS yes!* Mimi nimehudumu na nilivyokuwa Mkurugenzi wa Jiji ni mamlaka ya nidhamu lakini ni mwajiri pia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimepata uzoefu hapo kidogo ni ngumu sana kumpima Mtumishi wa Umma kwa kutumia *OPRAS*, ni formula tu! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu tunaona Mheshimiwa Rais, anapambana kweli kweli, usiku na mchana kwa ajili ya Taifa letu, lakini namna gani anasaidiwa kupima *performance* ya taasisi zake? *OPRAS* nadhani imepitwa na wakati, tuanze sasa na mfumo ambao wenzetu wanautumia duniani nimetoa mfano wa nchi mbili, nimesema Rwanda, leo hii Kagame anavyomteua Mkurugenzi wa Taasisi au

kiongozi yeote anakuja anampa malengo ya mwaka na anamwambia ndani ya mwaka ukishindwa kutimiza malengo haya uje na *resignation letter*, yaani uandike barua ya kuacha kazi mwenyewe au vinginevyo. Sasa sisi tunapima kwa kuangalia Vyombo vya Habari na sasa hivi tunakwenda kwenye Vyombo vya Habari, hapana huu utaratibu haufai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumsaidie Mheshimiwa Rais kwa mfumo wa *performance contract* ndiyo mfumo unaotumika sasa duniani, ndiyo mfumo wa kisasa, kila mtu ataachia ngazi mwenyewe wala huna haja ya kuhanganya na mtu, anapewa malengo kwa sababu tuna mpango mkakati, anapewa malengo na unaainisha majukumu yake, asipotimiza analeta barua tu ya kuacha kazi mwenyewe kwa *level* yoyote ile. Sasa *OPRAS weakness* nyingine inagusa tu Watumishi wa Kada za chini, leo hii taasisi zetu kwenye ngazi za Wizara tunapimaje?

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa. Nakuruhusu uko ulipo aah! Mheshimiwa Tunza.

TAARIFA

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemuelewa mzungumzaji nataka tu nimpe taarifa na wananchi wa Mlimba naye wampe *Performance Contract* ili akimaliza miaka yake mitano naye wamuone ame-*perform* vi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: *Actually*, Wabunge mnapimwa kwa *performance contract*, kabisa tofauti na wafanyakazi, hakuna *OPRAS* kwa wapiga kura. Ume-*perform* unachaguliwa tena, huja-*perform* wajumbe wale

wanakupiga nje kabisa. Mheshimiwa endelea nimetunza muda wako. (*Kicheko*)

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna Waraka mwiningine ukiachana na Sheria hii Sura, 298. Mwaka 2018 kulikuwa na Waraka wa Serikali juu ya jambo hili ninalozungumza hapa, wala siyo jambo geni. Sasa hoja yangu sijui inaishia wapi na ninaomba baadae kwenye hitimisho tungepata maeleo kwamba ule waraka maana yake Waraka ni sehemu tu lakini tunaweza kuona na mimi ushauri wangu mwishoni, sasa tuitazame upya hii Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura Na. 298 tuifanyie mapitio upya, badala ya *OPRAS* tuweke *Performance Contract*. (*Makofii*)

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

MWENYEKITI: Ruhusa!

T A A R I F A

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwenye eneo la *OPRAS*na utekelezaji wake sasa hivi tunaona mwaka 2017 Watumishi wengi waliondolewa kazini kwa kigezo cha *OPRAS*. Tena hapa, *OPRAS* imetumika vibaya sana, kuna *tick* tu ya kujaza kwamba nipo *form four* bila kuthibitisha cheti nimekileta au sijakileta lakini ukizingatia mwajiri ndiyo mwenye sifa zangu zote wakati ananiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *OPRAS* imeondoa Watumishi zaidi ya 4000 na wameshindwa kuwarudisha kazini. Hata hawajapeleka cheti chochote cha *Form Four*wala *Form Six*, *OPRAS*tu imesema *form four*wakati miaka 20 kafanyakazi akiwa darasa la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa mzungumzaji taarifa hiyo.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sipokei taarifa hiyo. *OPRAS* haisiani kabisa inahusiana na *performance*, nazungumza *performance*. *Brother* nazungumzia *performance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unanielewa nazungumzia *performance*. Kuondoka kwa Watumishi wa Umma hakuhusiani kabisa na *OPRAS*, *OPRAS* inapima.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kunambi unaongea na mimi endelea. (*Kicheko*)

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wanantoa kwenye mstari ngoja niendelee tu. Namsamehe kwa sababu mimi ni *Chief* wa Waluguru ninamsamee aendelee kwa sababu yeye ni mdogo wangu huyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika sekta ya kilimo, nitoke huko niongelee sekta ya kilimo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa! (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Taarifa!

TAARIFA

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpe taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Kunambi kwamba hata katika *promotion* za Utumishi wa Umma ni lazima *OPRAS* itumike. *OPRAS* ile inavyotakiwa

kujazwa ni kwamba yule *supervisor* anamjazia *subordinate* wake, utendaji kazi wake na kuona lakini tunafanya maboresho kwamba sasa tutajaza ile *OPRAS* kutokana na *job description* yako mwenyewe badala ya kuwa *one fit all* sasa hivi itakuwa Mhudumu atakuwa na *job description* yake ambayo atajaza pale, ukija Injinia atakuwa *job description* yake na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuitumia *OPRAS* katika kupima *performance* ya Watumishi wa Umma, ila tu kuna vitu ambavyo vitaongezewa na ndivyo tutavitumia hivyo vigezo hata katika kuangalia namna gani tunafanya *promotion* katika Utumishi wa Umma.

MWENYEKITI: Hoja ya Mheshimiwa Kunambi ni kwamba, kupima *performance* kwa *job description* ni msingi mbovu. Pima *performance* kwa kupima *performance indicators*. Ulitakiwa ufanye, tumekupa kazi tarehe fulani, ultakiwa ufanye 1, 2, 3, 4, 5, ...10 umeyafanya? Watu hawafanyi kazi! Ndiyo maana Kunambi alitandika makofi baadhi ya watu hapa Mjini.

Mhehimiwa Kunambi endelea. (*Kicheko*)

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nijielekeze kwenye kilimo. Sekta ya Kilimo wote ni mashahidi ni sekta muhimu sana kwa Taifa letu na mchango wake hata kipindi hiki cha *Covid* kilimo ndiyo sekta iliyoongoza. Asilimia 26.9 ya pato letu la Taifa, ukiangalia inafuatiwa na sekta ya ujenzi na maeneo mengine lakini kilimo ndiyo tunasema sekta muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe tu, nimeona kwenye mpango tuna miradi takribani 21 ambayo imekamilika kwa mwaka uliopita kwa Bilioni 7.5. Umwagiliaji utatusaidia sana kuinua kilimo chetu Nchini, nadhani Serikali sasa iongeze bajeti kwenye umwagiliaji lakini haitoshi siyo tu

kwenye umwagiliaji tuwe na *Agro-Base Industries*, viwanda vidogo vidogo vinavyo chakata mazao ya kilimo kuwa bidhaa, tuwekeze huko. Lakini pia tuongeze tafiti za masoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi ni mkulima wa mpunga, nina mpunga ndani sijauza gunia moja sasa ni shilingi laki moja, kutafuta hilo gunia moja ni zaidi kama 112,000. Sasa unauzu laki moja si hasara hiyo? Nimefungia mpunga ndani! Kwa hiyo, Serikali ijielekeze kufanya tafiti ya masoko pia, tulime kwa umwagiliaji lakini pia ifanye tafiti za masoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwenye jambo la barabara. Bahati nzuri barabara ya Morogoro – *Njombe border* ni barabara inayofungua uchumi wa nchi yetu na ni barabara ambayo inakwenda kutoa huduma Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Lakini barabara hiyo kwenye taarifa ya mpango nikiwa naipitia imenishangaza kidogo labda Mheshimiwa Waziri aje atolee ufanuzi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka wa fedha tulionao sasa, imeelezwa kwenye bajeti barabara hii kipande cha kilometra 125 kitaanzwa ujenzi na tayari upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi umekamilika. Sasa taarifa ninazopata kwenye mpango ni kilometra 220 zinakwenda kufanyiwa usanifu, zinatafutwa kandarasi za usanifu na upembuzi yakinifu wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, barabara hii umuhimu wake ni barabara mbadala wa Kitonga, mnaufahamu umuhimu wa barabara ya Kitonga, mizigo kwenda Zambia, mizigo kwenda *South Africa*, mizigo kwenda Malawi inapita Kitonga, Kitonga ikifunga na bahati fulani wakati wa masika Kitonga ilifunga tulikaa karibu mwezi mzima haipitiki ile barabara, walipata shida sana wafanyabiashara wetu. Mbadala wa barabara ya kitonga ni hii Morogoro – *Njombe Border* ni uchumi wa nchi yetu na ina-service Mikoa ifuatayo ya Njombe, Mkoa wa Ruvuma, Mkoa wa Mbeya na hadi Mkoa wa Rukwa. Ukipima umbali kutoka hapo Makambako uje uitafute Mikumi

kuna zaidi ya kilometra 400, ukitumia barabara hii kutoka Makambako - Njombe kuja Mikumi kilometra karibu 300 na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inanishangaza sana kuona kwenye mpango naelezwa habari ya kilometra 220 tafuta Mkandarasi na *ADB ndiyo financiersawa!* Hoja yangu ya msingi, hizi kilometra 125 ambazo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina za mradi zimekamilika na bajeti inaeleza kilometra 50 zianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo ya kina kwenye hili. Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Pindi Chana, simuoni tunaendelea na Mheshimiwa Seif Khamis Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Kishimba.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii kuweza kuchangia kwenye mpango huu wa maendeleo wa Tatu wa Taifa.

Nheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo analifanya Taifa letu. Majuzi hapa tumeona tumepokea fedha Trillioni 1.3 ambazo fedha hizo zimegawanywa katika kila Jimbo la Mbunge aliymo humu ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakwenda kujenga madarasa kila Jimbo, kulikuwa na kero kubwa sana ya madarasa na ilikuwa ni hoja ya kila mwaka inajirudia madarasa, madarasa ambapo ilikuwa wakati mwagine tunachangisha wananchi wetu. Michango hii tulikuwa tunachanga wananchi kule kijijiini wakati mwagine walikuwa wanakimbia kijijiini. Mwingine alikuwa anaamka saa nane usiku anamkimbia Mtendaji wa Kijiji/Kata kwa sababu ya mchango wa kujenga madarasa. Kupatikana kwa madarasa haya imekwenda kuondoa adha ya michango ilikuwepo uitiri wa michango kwenye ujenzi wa madarasa, nampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimsikia mmoja wa Wabunge wakati anachangia jana akasema tunapiga makofi kwa Triliioni 1.3. Kwa historia yetu toka tupate uhuru hatujapata fedha za kujenga madarasa mengi kwa kiwango hiki, haijawahi kutokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Mheshimiwa Mbunge yule kubeza fedha hizi hakikuwa cha kiungwana. Fedha ni nyingi, tunajenga madarasa kila kata na kama unavyoju, kila Kata katika nchi hii tuna shule za sekondari. Kwa hiyo tunakwenda kujenga haya madarasa na mpaka kwa huyo Mbunge tunaenda kujenga madarasa, tunajenga madarasa kila kona na pembe ya Nchi hii. Huwezi kubeza, 1.3 Triliioni zilizokuja kumwagika kwenye Majimbo yetu. Mimi hapa Jimboni kwangu natembea navimba, navimba kwa madarasa haya ya Mama Samia Suluhu Hassani, kwa hiyo nampongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuishia madarasa, tumepata fedha kila Mbunge hapa milioni 500 za maji. Unabeza vipi Triliioni 1.3 ambazo hazijawahi kutolewa kwa kipindi kifupi tunakwenda kujenga ndani ya miezi sita mpaka tisa kukamilisha *project* hii kubwa. Tumepata fedha za kununua mitambo ya kuchimba mabwawa makubwa kila Kanda ya nchi yetu imepata, unawezaje kubeza Triliioni 1.3 za *Corona*. Lugha iliyotumika kwenye hii fedha 1.3 kwa yule Mbunge kwenye hii ya *Corona* haikuwa lugha nzuri. Fedha hizi tunatakiwa tutembee kifua mbele, tuzinadi na tuhakikishe wananchi wetu wanapata uelewa wa fedha hizi katika kutekeleza miradi na hizi fedha tulioomo humu wengine zinaweza zikatuokoa kurudi hata katika kipindi kijacho. Leo unawezaje kubeza hizi fedha, tena tunahitajiwa tuzisimamie kwa ukaribu ili zisichakachuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Triliioni 1.3 haijawahi kutokea. Fedha hizi za *Corona* binafsi na wananchi wa Jimbo la Manonga tunawapongeza sana, tunapongeza Mama lakini tunawapongeza Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri, Waziri wa TAMISEMI kwa uchambuzi mzuri na mgawanyo ulio sawa Majimbo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hizi zimetoka kwa wataalam walioajiriwa na Serikali katika kila Halmashauri, kwa hiyo kila Halmashauri imepata mgao, tunakwenda kujenga madarasa 12,000 nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi napongeza na pongezi hizi zinakwenda sambamba na ile *projectya* kwenye mpango wetu tumeona Mheshimiwa Waziri umewasikia Wabunge hapa kila mmoja akizungumzia na tumekuwa tunazungumzia juu ya kuboresha sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo imepigiza kelele miaka nenda miaka rudi na mpango wetu huu ni wa tatu, tumekuwa na mpango wa kwanza wa 2011/2012, umezungumzia kilimo. Mpango wa pili wa Taifa wa 2016 kuja 2021 umezungumzia kilimo, tumekuja na ppango wa tatu wa maendeleo wa Taifa unazungumzia kilimo lakini hatujaona bado hatujawekeza vya kutosha kwenye kumkomboa mkulima kutoka pale alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa katika mpango huu tunaotaka kwenda kupilisha bajeti ya 2022/2023 ielekeze fedha kuwekeza kwenye kilimo. Tutenge fedha kama tunashindwa kuweka Trilioni Moja basi tuweke Bilioni 500 mpaka 700 kwenye sekta ya kilimo. Kama tunaweza wananchi mmoja mmoja akaweza kuchangia Pato ya Taifa mpaka asilimia 26 na Serikali haijewekeza vya kutosha. Je, tukiwekeza kwenye Bilioni 500 – 700 tutawezaje kupindua maendeleo ya wananchi wetu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mataifa yote duniani, narudia kusema biashara ya utumwa ilikuwa ni kilimo, maendeleo ya viwanda ilikuwa ni kilimo, kule Brazil, Marekani ilikuwa ni kilimo. Tuwekeze kwenye kilimo, tuwekeze kwenye kutafuta masoko, pia tuweke fedha za ruzuku kusaidia mbolea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mbolea ni shilingi 100,000 kwa mkulima. Bei ya mbolea inazidi kupanda na hatujawekeza mikakati ya kumsaidia mkulima katika kuhakikisha kwamba anapata mbolea kwa bei rahisi, kwa

sababu tunategemea mvua ambazo zinaweza zikaja chache au pungufu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inayokuja kuitia mipango yetu hii tunayoweka, lazima tuweke fedha ya ku-support mbolea, kuhakikisha kwamba tunaweka ruzuku kupunguza bei ya mbolea kutoka bei iliyopo sasa, kushuka chini hata shilingi 40,000 au shilingi 30,000. Tukifanya hivyo tutaongeza *production* katika nchi yetu. Pia tuhakikishe wakati tunafanya haya, tutafute masoko ya wakulima wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunalima kwa wasiwasi, bado tuna mazao ya kutosheleza na yamebaki kwenye maghala, na bado Serikali haijaonyesha njia ya kusukuma haya mazao yatoke: Je, tukienda kwenye kuwekeza zaldi, tutapata zaldi? Tumezungukwa na Mataifa ambayo wakati mwingine yana njaa; tumezungukwa na Sudan Kusini, tumezungukwa na nchi ya Kenya, tumezungukwa na nchi kama Burundi, Msumbiji na Zimbabwe. Tuna uwezo wa kupeleka mazao yetu kwenye Mataifa haya tukitengeneza miundombinu mizuri kwa wakulima wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mpango wako uwekeze zaidi kwenye sekta ya kilimo, kama kweli tunahitaji kuleta mapinduzi katika Taifa letu. Tumeona mikakati mingi ilikuwepo, ni hatua nzuri sana kupata miundombinu ile, wanasema zana za uchimbaji wa mabwawa. Ni nzuri na tunapongeza sana Serikali. Itasaidia ujenzi wa mabwawa, lakini pia tukajenge sasa *schemes* za umwagiliaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi jimboni kwetu pale Manonga, tuna maeneo mengi ya kujenga *schemes* za umwagiliaji. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa, sasa muda hauko upande wako.

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi uliyonipatia, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, baadhi ya Wabunge wamekuwa wakisema tu vizuri kuhusu mgawanyo ulio sawa wa rasilimali kwa Majimbo au kwa Wilaya zetu. Nilitoa mfano asubuhi wale tuliokuwa pale Morena kwamba, Wilaya ya Geita Vijijini watoto waliofanya mtihani darasa la nne juzi ni 48,000. Darasa la nne peke yake. Kuna takwimu za miaka ya hivi karibuni nimejaribu tu ku-surf hapa mara moja, kuna takwimu za watoto wa Shule ya Msingi za miaka ya karibuni sana. Kwa mfano, watoto wa Kibaha kwa mwaka huo, darasa la kwanza hadi la saba ni 15,000; wa Bagamoyo ni 23,000; wa Njombe 18,000; wa Makete 19,000; wa Makambako 22,000. Yaani nikiendelea hapa utakuta ni vichekesho. Hawa ni la darasa la kwanza mpaka la saba. Wale ni darasa la nne peke yake 48,000. Hao wengine 10,000 wengine 9,000 wengine 12,000 na kadhalika. *Basis* iwe ni *population* jamani. (*Makof*)

Tusidanganyane na hiki kigezo cha Majimbo, Majimbo. Yapo mambo kweli tunaweza tukafanya hivyo, lakini *basis* iwe ni *population*. Kwa sababu, tuna *disparity* kubwa. Wa kwako wewe la kwanza mpaka la saba hawafikii la nne la Geita. Sasa utasema kweli unapogawa rasilimali Geita ipate sawa na wewe au maeneo kama hayo? Itakuwa hatutendi haki. Lazima pamoja na mambo mengine ya jiografia, ukubwa wa eneo, lakini tukubali kabisa, kwa baadhi ya mambo, wale ambao wana watu wengi sana wajaribu kuangaliwa na Serikali kipekee katika kugawa rasilimali.

Tunaendelea na Mheshimiwa Jumanne Kishimba, Profesa na atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Lugangira.
(*Makof*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Muswada huu wa Bajeti ya mwaka 2022/2023. Pia mimi nam-support, namunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa sana aliyofanya, hasa hii juzi kwa hizi fedha shilingi trilioni moja, ukilinganisha na wakati huu wa *Corona* ambapo hali ya dunia kiuchumi siyo nzuri. Namshukuru sana na imetufikia kwenye maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwa malalamiko makubwa hasa kwa upande wangu wa Jimbo la Kahama Mjini. Nimekuwa nkipata zawadi, heshima kubwa, nimekuwa wa kwanza kwenye mapato, kwenye makusanyo na kwenye kila kitu. Hata hivyo, ninavyoongea, barabara zangu za mjini ni mbaya sana. Haiwezekani mtu anayeongoza kwa mapato halafu unamnyima fedha ya barabara. Atapataje hizo fedha bila barabara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata sasa hivi, zile shilingi milioni 500 za Mheshimiwa Rais bado sijapata. Ninavyoongea nina shilingi milioni 18 peke yake. Sasa itawezekana mnanipa mimi zawadi na matunzo. Afadhalii mtoe zile zawadi za ushindi, mnipe fedha za barabara. Baadaye nikiwa salama, mrudishe yale matunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipita juzi Kahama ukiwa unaenda Chato. Kweli ukiwa barabarani pale unaona mji unang'aa, lakini kule ndani hali ni mbaya sana. Mapato ya Serikali yanayokuja yanatoka maeneo yale. Kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atupatie hizo fedha ili wananchi hawa wakati huu msimu wa mvua unapoanza waweze kufanya kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo umeliongea, nami nilikuwa nakuja huko huko. Labda tu sasa kwa wachumi wetu tuone kama wanaweza kufanya namna. Maana yake wote tunaziona kero. Ujenzi unaoendelea kwa zahanati, hospitali; madarasa hatuna shida sana. Unaangalia, kweli vijiji vyetu au kata zetu hazikukatwa kama madarasa. Wananchi walikuwa wanakaa maeneo yale, lakini

unapotamka kijiji ukasema utaweka zahanati kila kijiji au Kituo cha Afya kila Kata, unatumia uwiano gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati zile ni kubwa, Vituo vya Afya kwa michoro ile, inatugharimu kweli shilingi 400/= mpaka shilingi 500/=. Mahudhurio ya wagonjwa ni wagonjwa 20 au 18 kwa siku. Kwa nini Serikali wasijenge jengo dogo la shilingi milioni 30, ile shilingi milioni 370 ikawekwa benki kwenye *fixed account*, fedha itakayopatikana iwatibu wagonjwa bure iwave mpaka uji? Maana yake wagonjwa hawafuati jengo, wagonjwa wanachofuata ni dawa na huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vijiji kwa leo baada ya mabadiliko makubwa ya pikipiki, *WhatsApp*, kila kitu viro karibu karibu sana. Ni bora hizo fedha watupati tuweke *fixed deposit*, wataalam watuchoree michoro ya kawalda ya fedha kidogo. Hizi fedha tuziweke *fixed deposit*, ile *interest* iwasaidie wagonjwa kwa kuwatibu bure pamoja na chakula. Sasa hivi sisi kule Kanda ya Ziwa tuna-*compete* na Waganga wa Kienyeji. Haiwezekani wewe una hospitali nzuri haina watu, Mganga wa Kienyeji ana nyumba ya makuti amejaza wagonjwa. Ina maana kuna tatizo pale kwako. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli mimi najua tunachenga chenga, lakini mfungwa ni mali ya Magereza, mhalifu ni mali ya Polisi, huyu mgonjwa ni mali ya nani? Maana yake mgonjwa hana mwenyewe. Katiba yetu inasema, Serikali italicinda watu wake na mali zake kwa nguvu zote, kwa hali na mali mpaka na jeshi. Kwa nini hatuna namna yoyote ya kumwokoa mtu anapokuwa anaumwa? Mimi nafikiri nimwulize Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa nini hapo panachengwa? Ila baada ya kifo tunakuwa na misiba, tunakuwa na mambo mengi yanakuja, lakini kwenye dawa hakuna mtu anataka kupagusa wala kwenye matibabu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha alifikirie sana. Nafikiri hili

linaweza likawa ndiyo kero kubwa kuliko kero yoyote. Leo hii bei ya dawa/matibabu, wote ni mashahidi humu, sasa hivi umezuka mtindo, unapokuwa na mgonjwa mahututi, wanaositisha matibabu kwa sababu *bili*/imekuwa kubwa. Sasa kama wamesitisha nawe huna fedha, ina maana unatakiwa ukabiliane na kifo. Je, ni sahihi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haina namna yoyote? Nani tumwombe na nani tumwulize? Hali ya kule vijijiini, maisha ni magumu sana, na ugonjwa hauna kusema huyu ni tajiri, huyu ni masikini, huyu ni nani? Mtu ye yoyote anaweza kuugua wakati wowote. Nafikiri mambo mengine ni kwa ajili ya mabadiliko makubwa ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, labda Serikali ingefikiria baadhi ya miradi kama mnaweza kuitazama upya, inatakiwa kuendelea sasa hivi au tuishie wapi? Kwa sababu, ninachosema, leo bei ya *container* kutoka Dubai kuja Dar es Salaam ni dola 15,000, kutoka dola 3,500. Je, hii miradi ikipanda mara nne, tutapata wapi fedha? (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili?

MWENYEKITI: Ndiyo.

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hoja zako za msingi sana Mheshimiwa Kishimba.

Ninyi Wabunge wenzangu ni mashahidi. Zahanati kila Kijiji; kuna vijiji vingine siku hizi ni kijiji kimoja tangu zamani,

Iakini sasa kijiji hicho hicho kinaitwa kijiji A, sijui nini B, sijui nini C, Iakini zamani ni kijiji kimoja. Sasa leo eti hapa tujenge zahanati tatu au mbili kwa sababu kuna Kijiji A na Kijiji B chenye jina lile lile. Mantiki, kila kijiji ukijenga zahanati yake, wagonjwa 20 hawafiki kwa kutwa. Zahanati zenyewe ndiyo zile, TAMISEMI wana zahanati kubwa, sijui za nini zahanati kubwa zile.

Mimi nauliza kila siku, fedha nydingi zinatumika; mambo ya zahanati, tungekwenda na ramani ile kwa mfano tulioachiwa na mkoloni ile, tungeshamaliza zahanati kwa vijiji vyote. Pia ukiviangalia vijiji vinaunganika. Ndani ya kijiji kimoja, vinazidi kutoka kadhaa kwa sababu ya idadi ya watu. *Centrally* ingekuwepo tu moja, inatosha. Mgonjwa akizidiwa anakwenda Kituo cha Afya na kadhalika.

Kwa hiyo, mambo mengine yanayotupelekesha ni lugha zetu sisi wenywewe; zahanati kila Kijiji, wakati siyo lazima kwamba kila kijiji kiwe na zahanati kwa sababu vijiji vingine kwa mgeni wala huwezi kujua hapa ni vijiji viwili au vitatu. Unaipopita pale, unaona ni kijiji hicho hicho tu. Ila sasa unaambiwa hapa mpaka, hiki ni kingine. Halafu hapa baada ya korongo hili, hiki ni kingine na kadhalika. Shule ndiyo zinaweza zikawa nydingi, Iakini zahanati! (*Makof!*)

Lile la Bima ya Afya, ndiyo maana tunamshughulisha Mheshimiwa Waziri wa Afya na Waziri wa Fedha, hawalali kuhusu watu wanavyougu na matatizo yao. Tunaendelea kuwa pamoja Waheshimiwa Wabunge katika hili la afya. Tunajua ni *headache*, Serikali msione tunasema, tunajua kwamba ni gumu hili la bima ya afya. Ni gumu, Iakini sasa si lazima tudai, kwani magumu ndiyo tuache wakati ni muhimu! Tunaendelea kuvuta kamba tu sisi ndiyo kazi yetu. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda halafu Neema.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu mpendwa,

Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania na kwenda maeneo mbalimbali duniani, kutafuta nusura ya Watanzania hasa katika mambo ya msingi yanayotukabili. Nampongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa tunaanza kupokea huu Mpango ulituongoza ukatueleza na kutusomea kanuni, nami nimezingatia sana. Ukasema Mpango huu ni mwongozo wa bajeti ijayo, lakini ukasema vile vile tushauri vyanzo vipyta vya mapato; na la tatu, ukasema tushauri vipaumbele vya bajeti. Nami nitajielekeza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kwenda huko, katika maeleo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake, ukurasa wa saba ameelezea utekelezaji wa baadhi ya miradi katika kipindi hiki, lakini nataka kuzungumza moja ya jambo kubwa ambalo nimekuwa nikilizungumza hapa Bungeni na ambalo nilijiteua kuwa balozi mimi mwenyewe, nalo linahusu suala la riba za mabenki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mzee Kime, Mbunge mwenzangu ambaye ni mbobezi kwenye masuala ya mabenki alilizungumza vizuri sana kwa lugha ya kitaalam zaidi, mimi nitalishusha katika lugha ya kawaida ambayo kila mmoja anaweza akaielewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa 2019/2020 watu waliokopa katika mabenki walikuwa asilimia 8.1, lakini mwaka wa 2020/2021 waliokopa katika mabenki walikuwa asilimia 4.3 yaani wakopaji wameshuka. Riba za mabenki kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, zimeshuka kutoka asilimia 16.8 mpaka asilimia 16.6. Yaani kushuka kwenyewe ni kwa 0.2 percent. Napenda kuipongeza sana Kamati ya Bajeti, sana sana; Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Bajeti, wamekokotoa jambo hili vizuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati riba za mabenki zimeshuka kwa 0.2%, riba za mikopo inayotolewa na Benki

Kuu kwa mabenki ya biashara imeshuka kutoka 12% mpaka 7%. Maana yake imeshuka kwa 5%. Kilichotokea ni nini? Ni kwamba Benki Kuu imeshusha kwa 5%, mabenki ya biashara ambako ndiko yanakwenda sasa kwa watu wetu, hao ambao tunasema tunataka kuinua sekta binafsi, wameshusha kwa 0.2%. Hapa kushusha kwa Benki Kuu kumeenda kunufaisha mabenki badala ya kuwanufaisha wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ukiliangalia kwa sura ya kawaida, unaweza ukalionia tu; lakini ukiingia ndani zaidi, unaweza ukasema hapa kuna ufisadi. Kwa nini nasema hivyo? Maana Serikali yenyewe, Benki Kuu yake inatoa kuyapa mabenki ya biashara kwa 7%, lakini Serikali yenyewe inakwenda kukopa kwenye mabenki ya biashara kwa 15% ya riba. Najua kwa mujibu wa sheria Serikali haiwezi kukopa Benki Kuu, lakini huu ni mzigo mkubwa sana kwa wananchi, asilimia 15 ya riba kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imeishauri Serikali na ninataka kuiomba Serikali yetu sikuvi, izingatie ushauri huu. Isipozingatia ushauri huu, siku moja kwenye ukumbi huu tutaikataa bajeti. Imeishauri Serikali isikope kwenye mabenki ya biashara kwa zaidi ya asilimia 10. Msingi wake ni nini? Kuwapunguzia mzigo walipa kodi Watanzania wa kulipa asilimia kubwa ya riba ya mabenki. Isikope kwa zaidi ya asilimia 10. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili mnalitazamaje? Ni kwamba kama Benki Kuu inakopesha kwa 7% halafu wanatoka watu wa benki za biashara wanakopesha Serikali kwa asilimia 15 inawezekana wapo watu kwenye Serikali yetu, wana hisa kwenye haya mabenki, wanapiga hela kutoka huku Benki Kuu wanaleta huku, wanaikopesha Serikali, ikitrudishwa wenyewe wanapata gawio kubwa. Ndiyo maana yake. Jambo hili ndiyo nasema, sitaki mimi nijipe kazi ya kuanza kuangalia kuna wakubwa gani kwenye Serikali wana hisa kubwa kwenye mabenki, kwa hiyo, wananaufaika na mchezo huu? Sitaki kujipa kazi hiyo, lakini itoshe kusema busara ituongoze katika hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hapa, nikamwuliza Waziri wa Fedha na kwa bahati mbaya haya maneno yetu huwa tunazungumza hapa wakati mwingine huwa yanageuka kama ngonjera tu, kwamba wayachukue wasiyachukue, sawa sawa. Ni kwamba, hivi ni nani anaye-control hizi *microfinance institutions*? Kampuni hizi za kukopesha wananchi ambazo zinapiga riba na wananchi wetu wanateseka, wamenyang'anywa *ma-fridge* na nini? Sikupata majibu mpaka leo na kazi hiyo inaendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha hata hii taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha inayosema, riba zimeshuka kutoka asilimia 16.8 mpaka asilimia 16.6, bado haina usahihi sana na hali ya sasa. Mimi nimekopa benki mwezi jana (Oktoba), na mwezi huu nimeanza kulipa mikopo ya kibashara. Siyo mikopo yetu hii, hapana, ni mikopo ya kibashara, maana mimi ni mfanyakibashara vilevile. Nimekopa kwa riba ya asilimia 21, akitaka mikataba yangu nitampa alone. (*Makof*)

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, nimekuruhusu Mheshimiwa.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: nikubaliane na mchangiaji na nimwongezee tu kwamba mfanyakibashara unapokopa kama una hati ya nyumba kwa maana ya dhamana ni asilimia 21 na kama hauna hati ni asilimia 24.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Ni sahihi sana na naipokea taarifa....

MWENYEKITI: Na bado mnakopa Waheshimiwa? Asilimia 24?

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Ni sahihi kabisa.

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, una kitu kinaitwa *letter of offer* asilimia 24, kama una *tittle deed* asilimia 21. Kwa hiyo asilimia 16 inayozungumzwa hapa haipo, sijui labda kwenye baadhi ya mabenki, Kamati ya Bajeti inatueleza nini? Kamati ya Bajeti inatueleza kwamba *BOT*imeshindwa kuwasaidia wananchi katika kupunguza riba za mabenki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, katika mambo yanayohusu utumishi wa wananchi sina urafiki. *BOT* siku moja inaweza ikamrudisha Waziri wa Fedha viti vyaa nyuma, asipoiangalia *BOT* siku moja itamrudisha viti vyaa nyuma. Hatuwezi kwenda hivi, wananchi wanapiga kelele, hali mbaya ya uchumi, tunasema, tunasema lakini hakuna linalokwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wenzangu wametangulia kusema hapa na naomba niseme, narudia kumpongeza sana Raisi wetu mpendwa. Jana kuna lugha ilitoka hapa, ni vizuri katika mambo haya kuwekana wazi, Mheshimiwa mwenzetu Mheshimiwa Mpina, alisema lugha ambayo wengi haikutufurahisha. Haikutufurahisha kwa sababu mama au kiongozi wa nchi anapokwenda kutafuta manufaa kwa ajili ya watu wake, akija hata kama na uji, onyesheni kushukuru. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Raisi amekuja na trillioni 1.3, kuna kazi inafanyika ambayo haijawahi kufanya ndani ya kipindi kifupi kama hiyo kwenye majimbo yetu; Mheshimiwa Mpina anachotueleza nini kwamba wameacha pesa nyingi huku, pesa gani anazosema? Pesa ambazo zipo katika Mahakama ya Usuluhishi wa Kikodi baina ya *Barrick* na Serikali kuhusu masuala ya kodi zinazotokana na madini, yaani zipo kwenye Mahakama, yeye ndio anatuambia ndio pesa zimeachwa. Ikihukumiwa kwamba nyie hamna kitu maana yake hamna kitu. Sasa huo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kilumbe nikuhakikishie...

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Ndio.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpina huwa analewa togwa, kwa hiyo msamehe tu, asikupotezee dakika zako. (*Kicheko*)

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka kusema habari ya kutuambia kwamba tunapiga makofi mpaka mikono inataka kuchubuka kwa sababu ya trilioni 1.3, kama yeze amezipuuza nashauri ile miradi ya maendeleo iliyopelekwa Jimboni kwake iletwe Jimboni kwangu mimi nazithamini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwelekeo wa bajeti; napendekeza,

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Ni ya kwanza hiyo Mheshimiwa?

MWENYEKITI: Ya pili, bahati mbaya.

Mheshimiwa Neema Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanza kwa kuunga mkono hoja. Ningependa kumpongeza Mheshimiwa Raisi kwa kupata billion 32 za kwenda kujenga upya soko la Kariakoo. Kimsingi soko lile linakwenda kutumiwa na wafanyabiashara ambao wanafanya kazi kwenye minyororo ya thamani ya sekta za uzalishaji kwa maana ya kilimo, mifugo na uvuvi. Hiyo inaendeleza azma ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha ya kwamba tunaimarisha hizi sekta za uzalishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kunufaika na hizi sekta za uzalishaji, napenda kuishauri Serikali lazima tuwekeze kwenye mbegu kwa maana ya mbegu bora, hususani zitakazoweza kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Lazima

tuwekeze pia katika afya ya udongo wetu, lakini tatu lazima pia tuwekeze katika utafiti na huduma za ugani. Ili tuweze kufanya matatu yote haya lazima tuwekeze kwenye teknolojia na masuala ya TEHAMA, matumizi ya teknolojia kwa ajili ya kukuza kilimo na uzalishaji wetu na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa hapa nirejee, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, mapema mwaka huu alisema kwamba tunakwenda kujenga kituo kikubwa cha TEHAMA hapa nchini. Kwa hiyo, hiyo inaonyesha dhamira yake kwenye masuala ya TEHAMA na kwenye Mpango huu ningependekeza Serikali ioneshe jitihada za makusudi kabisa, inakwenda kuinua jiteknekaji ya kilimo kwa kutumia teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kwenye mwezi wa Nane aliyekuwa Waziri wa Wizara Inayosimamia masuala ya TEHAMA alisema kwamba Tanzania imepata dola milioni 150 kwenye mradi ambao unaitwa *Tanzania Digital Project*. Kwa hiyo ningependa kupendekeza baadhi ya zile fedha kama mgao ulivyofanyika kwenye hizi pesa za *Covid*, basi hata katika zile baadhi zielekezwe katika kufanya tafiti na kuja na ubunifu wa kiteknolojia ambao utatuwezesha kuwa na mbegu bora, kufahamu afya ya udongo wetu, lakini pia kutoa huduma za ugani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hivi karibuni tumetangaziwa kwamba Benki ya CRDB imepata dola milioni moja kutoka kwenye Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi ili kutoa mikopo kwa wakulima wadogo. Niilombwa sana Serikali ihakikishe kwamba fedha zile zinakwenda kweli kwa wakulima wadogo na sio kunufaisha wafanyabiashara wakubwa, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya zile fedha pia zinaweza zikaelekezwa katika kutafuta mbinu kwa kutumia teknolojia za kupambana na haya mabadiliko ya tabianchi ikiwemo narudia tena mbegu bora, kufahamu afya ya udongo wetu na kutoa huduma za ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeshasema kwamba ungependa kuona Bunge lako la Kumi na Mbili linaacha historia na *legacy* yake kwenye sekta ya kilimo. Wengi tumeongea kwamba tunahitaji bajeti iongezeke kwenye sekta ya kilimo, lakini tunayo fursa ambayo naiona ni *low-hanging fruits*. Kwenye sheria ambazo zipo chini ya TAMISEMI, kila halmashauri inatakiwa ifanye *reinvestment* kwa maana kwamba kama kwenye mapato ya *council*/ilipatikana shilingi milioni moja kutokea kwenye sekta ya kilimo, wanatakiwa wafanye *reinvestment* asilimia 20 kwenda kukuza ile sekta ya kilimo. Asilimia 15 wafanye *reinvestment* kwenye sekta ya mifugo, asilimia tano kwenye sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la *reinvestment* halifanyiki. Kwa hiyo ni *low-hanging fruits* ambao sisi kama Bunge tunaweza tukahakikisha kwamba TAMISEMI watekeleze sheria hiyo, TAMISEMI watekeleza takwa hilo la kisheria, kwa sababu moja kwa moja hapo sekta ya kilimo itaweza kupata fedha nyongeza zinazotokana na uzalishaji kutokana na sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali kwamba wamekuja na mpango wa *e-commerce* yaani biashara ya mtando. Wanufaika wakubwa na biashara wa mtando ni watu ambao wapo kwenye sekta za uzalishaji, kilimo, mifugo na uvuvi, lakini mpaka hivi sasa kwa mujibu wa taarifa za Shirikisho la Watoa Huduma za Simu - *GSMA* wanasema bado mpaka sasa asilimia 48 ya Watanzania hawatumii *mobile internet*. Sasa ikiwa bado hatutumii *mobile internet* ina maana hata matumizi yale ya *e-commerce* hatutaweza kufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda nipendekeze kwa Serikali iwekeze jitihada kubwa kwa kushirikiana na wadau kuja na mfumo wa kuhakikisha kwamba wanatoa elimu ya *digital literacy* na *digital skills*, kwa sababu bila ya kufanya hivyo hata huu mpango wa biashara mtando hatutaweza kunufaika nao kutoka na kwamba watu tunazo simu lakini hatutumii simu zetu kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nielezee suala zima la vyanzo vipyta ya mapato. Nakumbuka Mheshimiwa Raisi alivyokuja hapa kuhutubia kwenye Bunge lako Tukufu mwezi Aprili alisema kwamba tutanue wigo wa walipakodi. Hapa narudia tena kusema, lipo kundi kubwa la wafanyakishara walio kwenye sekta isiyo rasmi. Katika kila shilingi kumi ambayo inazunguka kwenye uchumi wetu shilingi sita ipo kwenye sekta isiyo rasmi. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ije na mpango mkakati wa namna gani tutarasimisha biashara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ningependa kupendekeza, ikiwa kama Serikali inaweze ikaweka mazingira wezeshi ya kuvutia wawekezaji, inaweza ikatoa misamaha ya kodi kwa ajili ya wawekezaji, kwa nini isifanye hivyo kuhakikisha kwamba inawavutia wale wajasiriamali ambao biashara zao hazijarasimisha waweze kuzirasimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kuna swali liliulizwa kwamba tuna mabilionea wangapi? Kwa hivyo, ninachopenda kupendekeza ni Serikali ije na mpango wa kuweka angalau miaka miwili ya *tax holiday*, misamaha ya kodi kwa wazalishaji...

MWENYEKITU: Hivi tulijibiwa tuna mabilionea wangapi?

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijibiwa kwamba tuna mabilionea takriban 5000 na wote ni kwa hisani ya Chama cha Mapinduzi, kama nipo sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwamba, tunahitaji kuja na mpango ambao utawavutia wale walio kwenye sekta isiyo rasmi kurasimisha biashara zao. Mpango ambao utawavutia vijana, wanawake na wenye ulemavu kuingia kwenye biashara rasmi. Kwa hiyo ningependa kuiomba Serikali ije na angalau miaka miwili ya msamaha wa kodi kwa biashara mpya ambazo zinaanzishwa na makundi haya na kama inafanya hivyo kwa wawekezaji

naamini kabisa inaweza pia ikafanya hivyo kwa kundi hili la vijana, wanawake, watu wenyewe ulemavu na hapo ndio tutakuwa tunafanya kazi ile dhana nzima ya kuongeza wigo wa walipakodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hapa tunafurahia na tunamshukuru sana Mheshimiwa Raisi Samia Suluhu Hassan kwa pesa za *Covid-19* ambazo zimeingia nchini. Pia ningependa kutumia fursa hii nipendekeze kwa Serikali iko haja ya kutumia makundi yenye ushawishi mkubwa kwenye jamii kumuunga mkono Mheshimiwa Raisi katika vita hii ya *Covid-19* na kutoa elimu kwenye jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka siku ya Mkutano Mkuu wa *NGOs*, binafsi nilimwomba Raisi Samia Suluhu Hassan kwamba *NGOs* ziweze kushiriki kwenye kutoa elimu kwa jamii, wasanii washiriki kwenye kutoa elimu kwa jamii, vyombo vya habari vishiriki kwenye kutoa elimu kwa jamii, watu mashuhuri washiriki kwenye kutoa elimu kwa jamii kuhusu *Covid-19*, hata na sisi Wabunge tushiriki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kuishauri sana Serikali, kama ambavyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI wameweka wazi mgao basi na Wizara ya Afya pia iweke wazi mgao wa kile kipande cha elimu ya jamii kwenye upande mzima wa *Covid-19*, kwa sababu mpaka sasa hauelewi kipande kile kinatumikaje na nani ambaye anafanya au anatoa elimu hiyo ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kusisitiza sana iko haja kubwa ya kuweka kipaumbele kama ambavyo Wabunge wamesema katika Sekta ya Kilimo, Sekta ya Mifugo na Sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga tena mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Neema. Mchango wako wa mwisho hata sijausikia nilikuwa bado napiga hesabu ya mabilionea, unajua jana sikuwepo, napiga

hesabu ya mabilionea 5,000 ukigawa kwa mikoa 26 ni *roughly* kama mabilionea 200 kwa Mkoa. Sasa nikiangalia hapa Dodoma mabilionea 200 Kongwa hamna, Mpwapwa wa Simbachawene labda mmoja au wawili, Bahi hamna, Chamwino kule kwa Mheshimiwa Ndejembie wale ng'ombe, aaah wapi hamna. Kwa hiyo sisi Dodoma hiyo 200 labda 10, tena mjini hapa hapa.

Ahsante sana. Tunaendelea, nilishamtaja Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Dkt. Oscar Kikoyo.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mpango huu. Nimeona Wabunge wanzangu wengi wamezungumzia suala la kilimo, bado na mimi nitaendelea kujikita hapo kwa sababu bado nchi yetu kwa asilimia zaidi ya 65, watu wetu wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo taarifa ya Kamati imesema, Kamati imeongea vizuri sana na imetoa maoni mazuri sana kwa Serikali, kilimo kwa asilimia zaidi ya 26 ndio inaongoza katika pato la Taifa, lakini cha kushangaza inakuwa kwa asilimia tatu mpaka nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema asilimai 65 ya watu ni wakulima bado, leo hii pesa ya maendeleo ya kilimo bilioni 200 karibu ambazo zinatengwa 294 kwa kweli ni ndogo na Kamati imeshauri imesema ni bora pesa hiyo ikaongezeka angalau ikafika bilioni 450 ili kuweza kuisaidia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu wakulima wetu wengi sana wanajitegemea na kikubwa zaidi ambacho kinawatesa ni ukosefu wa pembejeo, ukosefu wa Wagani na watu ambao wanaweza kusimamia kazi za kilimo. Tunaomba Serikali iweze kuona umuhimu wa kuleta ruzuku kwenye mbolea. Tunaona sasa hivi hasa Nyanda za Juu Kusini ambao sisi tunalisha *almost* nchi nzima, leo hii kilimo bado hakijaanza kwa sababu watu wanatafakari namna gani wataendelea kulima kwa sababu mbolea zimepanda bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa kilimo kwenye wilaya ni wachache, leo hii Serikali haijaajiri kwa muda mrefu Maafisa Ugani na waliopo hawana vifaa vyta kuweza kuwasaidia kutenda kazi. Majimbo ni makubwa na maeneo wanayofanya kazi ni makubwa wanashindwa kuwafuatilia wananchi na kuhakikisha wanatoa mazao kama inavyopaswa. Sasa kumetokea kuna watu binafsi wanaoingia kwenye mambo ya kilimo na kuwadanganya wakulima. Naamini wewe umesikia na Wabunge wenzangu wamesikia, sehemu za Njombe kuna watu wamesema kuna mazao ambaao wananchi wakiyalima watapata mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna zao hili la vanila, watu wametoa fedha kwa makampuni binafsi wamelima hizo vanilla, wamedanganya kilo moja ni milioni moja na mwisho wa siku hawajapata hicho ambacho walichetegemea. Serikali ilikuwa na wajibu wa kuweka Maafisa Ugani ambaao wao ndio wangekuwa waanawaambia wakulima na wala sio watu binafsi, mwisho wa siku wanawadanganya. Tunahitaji kuongeza nguvu kwa watu wetu ili kilimo kiweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya mazao ni shida, leo hii kilimo cha chai katika Wilaya ya Rungwe na Mikoa ya Njombe bado chai inauzwa kwa bei ndogo sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu amejitahidi kufika maeneo yetu na tumelalamika muda mrefu, lakini bado bei inasuasua, wakati bei ya soko la dunia bado iko juu, hatuelewi kwa nini watu wetu hawapati soko la chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ndizi zinazalishwa kwa wingi sana. Leo hii kuna nchi kama za Jamaica wanaishi kwa sababu ya ndizi, leo sisi tuna ndizi tunalima na watu wetu wanalima mwisho wa siku ndizi mkungu mmoja shilingi elfu mbili. Naomba Wizara husika isimamie kuhakikisha zao hili linakuwa zao la kibashara vinginevyo wanaingia wafanyabiashara wale ambaao tunasema ni wachuuzi, wananunua kwa kuwalangua wakulima kupeleka ndizi Malawi, kupeleka ndizi Zambia, wakati huo wanapata wao faida, lakini mkulima wa Wilaya ya Rungwe au Mikoa wa Mbeya hapati faida yoyote. Tunaomba Wizara isimamie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa zao la *cocoa* tunafahamu kuwa *cocoa* ni zao ambao Ikinaleta faida katika dunia na Tanzania nafikiri *cocoa* yake ni bora, ya pili kwa maana baada ya Ghana inafuata Tanzania. Tunaomba Wizara hii na hasa Mheshimiwa Bashe najua anajitahidi, lakini kwa hili tunahitaji *cocoa* iongezeke bei kutoka elfu tano ambayo imepanda msimu huu, iende mbele zaidi maana soko la dunia *cocoa* ina bei kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali ina haja ya kuongeza fedha kwa watu wanaonuna *NFRA*, wanaonunua mazao. Kwanza kabisa *capacityya* kubeba mazao hawana kwa sababu hawana maghala mengi katika maeneo mbalimbali. Naomba Serikali iijengee uwezo taasisi hii na hasa wakati wa msimu wa kununua mazao pia wawe na pesa za kutosha waweze kununua mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke hapo kwenye kilimo niende kwenye eneo la miundombinu. Reli ya *TAZARA* ilianzishwa kati ya muungano wa nchi mbili, lakini sheria iliyoanzisha reli ya *TAZARA* nafikiri ina upungufu kwa sasa. Tunaomba Serikali sasa iletu marekebisho ya sheria ya reli hii ili kusudi Tanzania iwekeze kwa wingi fedha zake kwenye reli hii, maana ina faida kwa Nyanda za Juu Kusini ambapo mazao mengi yanazalishwa kule. Naomba Serikali ifanye hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kwenye sekta binafsi, sekta binafsi inasaidia sana uchumi wa Taifa letu, lakini kumekuwa na mlolongo mrefu sana kuisaidia sekta hii. Naomba Serikali iangalie makosa madogo madogo ambayo yanasaababisha sekta binafsi isifanye kazi yake vizuri. Kuna urasimu mkubwa wa usajili wa makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tozo zipo nyangi, unakuta mfanyabiashara anapotaka kufungua biashara tozo zipo sehemu nyangi nyangi na zinachukua muda mrefu, anaenda kwenye dirisha moja inamchukua wiki mbili, akienda sehemu nyiningine muda umekwenda, mwisho wa siku hata wawekezaji tunaowaita waje kuwekeza nchini inabidi

waende nchi jirani kwa kuwa sisi tuna mambo mengi sana ya ukiritimba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa nchi yetu inazungukwa na nchi mbalimbali, na tunafahamu – siwezi kuitaja hiyo nchi – lakini hiyo nchi inasubiri sisi tukosee ili wao waondoe yale ambayo sisi tunayaweka kama vikwazo na kuwakaribisha hao watu waende kwao na sisi tunakosa wawekezaji. Ninaamini Serikali imekuwa ikitamka sana suala la uwekezaji na kuwaita wawekezaji wengi wafike lakini mwisho wa siku hatuna ufanisi katika kuwakubalia hao watu na kuwasaidia ili waweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini sekta binafsi hii wanapotaka kupata mikopo kuna usumbufo mkubwa sana wa upatikanaji wa mikopo. Tumekuwa tunahangaika na kusema kila siku na riba, na wenzangu wametoka kuzungumza hapa kwamba riba zimekuwa kubwa sana. hatuwezi kusaidia sekta binafsi ikakua mwisho wa siku ambapo karibia takribani asilimia 35 inaongeza kwenye *GDP* ya Taifa tunashindwa kuisimamia sekta binafsi.

Tunaomba sana Serikali isimamie hilo, na katika mpango huu tunaomba sana Serikali ihakikishe kwamba inaondoa vikwazo vizivyokuwa na maana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo kimsingi hayaendi sawasawa katika maeneo mbalimbali ya maendeleo. Tunazungumzia maendeleo ya watu, maendeleo ya watu hayawesi kukua bila kuwa na elimu bora. Leo hili wewe mwenyewe umezungumza hapo kwamba usajili wa watoto umeongezeka. Ni kweli Serikali imepeleka shule kwa ajili ya kujenga, lakini je, hizo trilioni zilizokwenda huko chini usimamizi wake ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wabunge leo tumekuwa ni moja ya sehemu ya fedha hizo, lakini usimamizi wake ukoje; tunahakikishaje kwamba hizo fedha zitafanya kazi kwa viwango na kutimiza ule wajibu ambao umekusudiwa? Kumbuka hili ni deni, wala siyo hisani kutoka

kwa wale walio tupatia. Kwa hiyo, tunahitaji kuzisimamia, na Wabunge wenzangu naomba tuliangalie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya bado ninasisitiza kwamba tumekuwa na wimbo wa Taifa, kila siku tunarudia yaleyale lakini hayatimizi, tunapitisha kwenye bajeti ya Bunge lako Tukufu, mwisho wa siku fedha zinakwenda kidogo, tofauti na jinsi ambavyo tumeisimamia. Tunaomba kile tulichokipanga kama Wabunge kiweze kusimama kwenye Wizara husika na zikaenda kufanya kazi, hususan Wizara ya Kilimo ambayo ina asilimia kubwa ya Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusma hayo, ninaomba niishie hapa. Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru Rais wetu, hasa kwa pesa ambayo imeletwa kwenye majimbo yetu. Wakati unatoa takwimu za wanafunzi ambao wako darasa la nne nikawa naangalia kwenye Wilaya yangu ya Muleba, tunao zaidi ya wanafunzi 19,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mwaka huu kabla Mheshimiwa Rais hajasema neno lolote, tulikuwa tunajuliza Muleba kule hivi tunafanya nini na watoto ambao wamemaliza darasa la saba. Tukawa tumeanza ujenzi wa vyumba vyaa madarasa. Nashukuru kwa pesa ambayo ametuletea sasa tunao uhakika kwamba vijana wetu wa darasa la saba watapata madarasa wote na tuendelee kumshukuru Rais wetu kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yake. Pamoja na pongezi hizo, zaidi niwapongeze Kamati yetu ya Bajeti. Nimesoma maandiko yao yote na nipayenda kuwapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza zaidi kwenye sekta ambazo zinachochea uchumi katika majimbo yetu, hasa sisi tunaotoka vijiji. Mimi naomba nitoe ushauri wangu; kwa vipaumbele ambavyo napendekeza kwenye bajeti ijayo naomba tuangalie sekta ya kilimo, tuangalie sekta ya mifugo, tuangalie sekta ya uvuvi na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamechangia sekta ya kilimo na wengi wamesema inachukua zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania ambao ni karibia milioni 22 ya Watanzania, wanajihuisha na masuala ya kilimo. Na tumeona mchango wa sekta ya kilimo kwenye uchumi wetu. Lakini ukiangalia bajeti ambayo tunaipatia kilimo, nadhani hatukitendei haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imependekeza kwamba bajeti tuliyonayo ya mwaka huu tuiongeze mpaka ifike zaidi ya bilioni 400. Kama tunataka kutoka hapa tulipo, sikubaliani na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti, mimi napendekeza twende zaidi ya triliuni moja kwenye sekta ya kilimo ili tuweze kunusuru uchumi wa Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia uzalishaji wa mazao mengi *per hectare*, mazao mengi tunazalisha chini ya kiwango kwa sababu hatujawekeza vyta kutosha kwenye sekta ya kilimo. Ukiangalia mpango wa miaka mitano ambao tulijadili hapa mwaka jana tulikubaliana kwamba tunakwenda kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka ekari 500,600 kwenda milioni moja na laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia tulipo leo, tuna miaka mitatu kufikia mwaka 2025 ambako ndiyo *target* yetu, bado tunaekari 569,000 laki ni lengo letu ni kufikia ekari milioni moja na laki mbili, kwa miaka mitatu iliyobaki

tunakwenda kufanya muujiza gani ili tuweze kufikia hilo lengo letu. Tusipoongeza bajeti ya kilimo tutabaki tunaimba wimbo uleule, tutabakia hapohapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia uzalishaji kwa mfano wa mafuta ya kula. Mpaka leo tunapoongea ni aibu kwa nchi hii ambayo tunasema wakulima ni zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wote, bado tunaagiza mafuta ya kula kutoka nje ya nchi. Naomba kwenye mpango huu Waziri wa Fedha atupatlie mkakati wa nchi ili kuinusuru nchi hii kutokana na kuagiza mafuta kutoka nje wakati tunalima na wakati nchi hii tunasema ni nchi ya wakulima na ni nchi ya wafanyakazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya mikoa wamekuja na mazao mapya. Kwa mfano Kagera kule tuna mazao mapya ya vanilla, kwa mfano. Wakulima wamejitalidi wanaliima lakini hatuna masoko. Na Wabunge wengi hapa wamesema tunapowekeza kwenye kilimo tuhakikishe kwamba tunawekeza kwenye utafiti, tunawekeza kwenye kutafuta masoko tusije tukatumbukia kwenye janga ambalo tulinaswa nalo hapa juzi wakati tunahangaika kutafuta pesa ya kununua mahindi kutoka kwa wakulima. Naomba tunapohamasisha wakulima wetu wazalishe kwa wingi na Serikali ihakikishe kwamba inatafuta masoko kwa ajili ya mazao ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi; mwaka jana wakati nachangia hapa nilisema nchi yetu imebahatika kuwa na maziwa na bahari, lakini ukiangalia mchango unaotokana na mazao ya uvuvi na yenye hapa ni aibu. Ni aibu kwa nchi kama Tanzania tunapoagiza samaki kutoka nje ya nchi kwa kutumia pesa ya nje ni aibu kwetu. Naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri kwenye mpango tutakaokwenda kutunga sasa kutengeneza bajeti, atuambie tuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba sekta ya uvuvi na mazao ya uvuvi yanachangia kwenye pato la Taifa hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea mwaka jana hapa, na ninaomba nirudie niliyoyasema; tumejifunga na

kanuni na sheria ambazo zinarudisha uchumi wetu nyuma. Ukiangalia tozo tulizonazo kwenye sekta ya uvuvi, ukililinganisha Tanzania na nchi jirani, hasa zile tatu ambazo tuna-share Ziwa Victoria kwa mfano, kodi zetu hazikubaliki na hazibebeki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache tu, ukiangalia tozo ambazo sisi Tanzania tunatoza na wenzetu, majirani zetu, kwa mfano ukiangalia VAT Tanzania tozo yetu ni shilingi 552 wakati jirani yetu Uganda anatoza 115, mwenzetu Kenya anatoza shilingi 34. Matokeo yake ni nini; mazao mengi ya uvuvi yamekuwa yakielekezwa upande wa pili na sisi tumekuwa tukikosa kazi, na hasa vijana wetu ambaao wame-invest kwenye sekta ya uvuvi hawawezi kufanya kazi kwa sababu hawawezi kushindana na wenzao ambaao wako nchi jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hata viwanda vyaa kuchakata minofu ya samaki. Miaka ya nyuma Tanzania tulikuwa na viwanda vingi lakini kutokana na hizi sheria tulizojiwekea, tozo, sheria mbalimbali, vibali na nini, viwanda vyote vimehamia nchi za jirani, tumebakii na viwanda vichache hapa. Ni lazima tujulize tumejikwaa wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapoongea tumebakii na takribani viwanda nane. Uganda wana viwanda zaidi ya 20, Kenya wana zaidi ya viwanda vitano, na vyote vimehamia vimekimbia kutoka hapa kwa sababu ya mfumo tulionao wa biashara, mfumo wa tozo na mfumo wa sheria tulijojiwekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza kwa nini mpaka leo tunapoongea unapotaka kusafirisha mazao ya uvuvi lazima yasafirishwe kupitia Viwanja vya Ndege vya Entebbe na Viwanja vya Jomo Kenyatta, Kenya, mazao ya uvuvi yanayotokea Tanzania. Tuna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba sasa badala ya kusafirisha kwenda Entebbe na Nairobi, kwa nini tusitumie Viwanja vyetu vya Mwanza, Dar es Salaam au KIA? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mwanza tumejenga *facility* kwa pesa ya walipa kodi, *facility* nzuri hata inazidi *Jomo Kenyatta International Airport*, lakini hatuitumii. Na sote tuko hapa tumekaa hatujishughulishi na hatujilizi kwa nini hiyo *facility* ambayo tumeigharamia haitumiki. Na mwaka jana niliongekea hapa lakini tumemaliza tumerudi nyumbani, kila kitu kimeendelea *business as usual.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tubadilike, kama tunataka kuingia kwenye soko la ushindani na kwenye mpango tunesema tunakwenda kujenga uchumi shindani na uchumi shirkishi, tunaujengaje kama hatuwezi ku-*strain our minds* tukafikiri nje ya boksi ile tuweze kunusuru nchi yetu na kuhakikisha kwamba hii sekta ya uvuvi ambayo tumebarikiwa, ni mali ya Watanzania, ili iweze kutusaidia kuchangia uchumi wa nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo kundi la vijana, sijaona kwenye mpango. Ukienda huko vijiji tunakundi la vijana ambao wakiamka asubuhi hawana kazi ya kufanya, mchana hawana kazi ya kufanya, mpaka jioni hawana kazi ya kufanya. Naomba kwenye mpango huu Serikali ije na mkakati hawa vijana tunawafanyaje. Vinginevyo tunatengeneza bomu ambalo miaka kumi, sihirini ijayo, litakuja kutulipukia wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima mpango uangalie kama ni mikopo ambayo tunaitoa kwenye halmashauri zetu ya kuwasaidia *hawa* vijana, hii asilimia nne ambayo tumejipangia haitoshi. Lazima tuangalie mkakati wa kuwanusuru hawa vijana na kwa kufanya hivyo tuweze kuwashirikisha kwenye uchumi wetu... (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Priscus Tarimo.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa na mimi nafasi hii niweze kuchangia. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa kibali cha kuweza kusimama hapa leo nikiwa na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Naibu wake kwa hotuba nzuri sana ya mwelekeo wa mwongozo wa mpango wa mwaka 2022/2023. Lakini pia nikupongeze wewe na Naibu Spika kwa kazi nzuri ambazo mnaendelea kuzisimamia katika Bunge hili ambalo kwa kweli unaliendesha kwa kiwango cha hali ya juu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu, Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambazo anaendelea kulitumikia Taifa letu bila kujali tofauti zetu za kisiasa, udini, kanda, ukabila, na wote tunashuhudia; mama kazi iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kushusha fedha nydingi sana katika miradi ya maendeleo kwa nchi yetu, miradi ya afya, elimu, maji n.k. Lakini pia kwa Wilaya yangu ya Nyang'hwale kwa kweli Mheshimiwa Rais ameweza kutumwagia fedha nydingi kwa kipindi kifupi, zaidi ya bilioni nane kwenye miradi mbalimbali ya afya, elimu, maji, miundombinu hadi *TASAF*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni mfupi sana kwa leo, ushauri wangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, nizungumzie upande wa sekta ya madini; sekta hii hivi sasa na yenyewe inachangia sana pato la Taifa. Lakini pamoja na uchangiaji wa pato kubwa la Taifa kutookana na madini hizo fedha ambazo zinapatikana kwa wachimbaji

wadogo ni fedha ambazo tunaona ni nyingi sana, lakini nasema ni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba sana katika mpango huu tuweke mkakati wa kuweza kuwawezesha wachimbaji wetu wadogo ili waweze kuweza kujipatia kipato na kuongeza kipato cha Taifa. Leo hii tunasema sekta ya madini imechangia zaidi ya bilioni 500, ni wachimbaji wanaotumia sululu, je tukiwawezesha wachimbaji hao tutakusanya mabilioni na tutapata mabilioni mengi kutokana na hawa wachimbaji wetu wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo kwenye upande wa sekta ya madini, Mheshimiwa Waziri ninaomba sana sasa hivi kumekuwa na utoroshwaji mkubwa sana wa dhahabu inayotokana na uchenjuaji wa kutumia *mercury*. Kwa hiyo ninaomba sana tuweke mlkakati madhubuti ya kuweza kuitambua ile mialo na kuwatambua hawa wachennjuaji wanaotumia *mercury* ili tuweze kuidhibiti dhahabu hiyo ambayo sasa hivi inatoroshwa kwa wingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo bilioni 500 ambazo tumezipata zinatokana na wale ambao wana *elution machine* na wale ambao wana *VAT leaching*. Lakini kwa hawa wachenjuaji wadogo kwa kweli dhahabu zao hazukusanywi ipasavyo, kwa hiyo Taifa linapoteza mapato sana. kwa hiyo kwenye mpango wetu huu wa 2022/2023 tuweke mkakati ulio mzuri zaidi tuweze kuwatambua hao wenyе mialo ili tuweze kuzikusanya hizo dhahabu tuweze kuongeza pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, naomba pia nizungumzie kuhusu *TRA*; ushauri wangu, kwa kweli naiomba Serikali kupitia *TRA* waweze kuongezewa kibali cha kuajiri watumishi ili waweze kuwa wengi, waweze kudhibiti huu mtindo uliopo sasa hivi ambao wafanyabiashara wanakwepa sana kutoa risiti kwa sababu watumishi wa sekta hiyo ya *TRA* wanakuwa ni wachache, hawapiti maeneo mbalimbali kufanya ukaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalisema ushahidi wake ninao. Kwa sababu unapoingia dukani mpaka sasa hivi bado kuna mtindo wa wafanyabiashara anakuuliza nikupe bei ya risiti ya mkono ama ya *EFD machine*. Kwa nini wanasema hivyo; ni kwa sababu usimamizi haupo wa kutosha. Kwa hiyo, ninaomba sana *TRA* wajaribu kuangalia upande huo. Bado Serikali inapoteza mapato makubwa sana kwa wafanyabiashara wetu kwa sababu bado wanakwepa kutoa risiti za *EFD machine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri mwingine kuhusu suala hilo la *TRA*. *TRA* izidi kabisa kuendelea kutoa elimu ya mlipakodi, lakini pia kwa waanyabiashara wetu pamoja na wanunuzi. Elimu hii bado inahitajika sana, kwa sababu leo unakuta mtu anaulizwa nikupe risiti ambayo ni ya mkono au ya *EFD machine*, anapewa bei mbili tofauti kwa sababu elimu hiyo haijawaflikia vizuri sana Watanzania walio wengi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa ushauri kwamba tuweke mikakati ya kutosha kuhusu hawa wao wafanyabiashara wanaokwepa, ama kuwaongezea adhabu. Lakini pia wanunuzi wanaonunua bila kuomba risiti atakapokamatwa na kifaa ama bidhaa ambayo haina risiti inabidi naye adhibitiwe na afikishwe sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Sisi Wabunge tuliomo humu, kwa ushahidi ninao kabisa, tunakutana maeneo mbalimbali iwe kwenye maduka ama kwenye huduma mbalimbali, huwezi ukamkuta Mbunge anaomba risiti, wakati ni kiongozi. Kwa hiyo, na sisi Wabunge hebu tuwe sasa mstari wa mbele kuanza kuomba risiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili uthibitisho ninao. Nikiwaliza hapa Waheshimiwa Wabunge tunaoingia kwenye migahawa wangapi tunatoka na risiti? Tunaoingia kunyoa vipara ama kutengeneza saluni ya akinamama, akina mama wangapi Waheshimiwa Wabunge wanatoka na risiti za saluni, wangapi? Kwa hiyo, nasema hayo kwa sababu nina ushahidi na tunakutana maeneo hayo mbalimbali, na sisi pia kama

viongozi tuwe mfano wa kuweza kukusanya kodi kwa ajili ya pato la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hussein Nassor Amar. Nilishakutaja Mheshimiwa Priscus Tarimo, utafuatiwa na Mheshimiwa Eric Shigongo.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami niungane na wachangiaji waliotangulia kuipongeza Serikali ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu, kwa namna ambavyo wameweza kuweka ule mpango, hasa matumizi ya ile hela trillioni 1.3. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa namna ambavyo wallendelea kumshauri Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi kuanzia kwenye hela ile ambayo kimsingi ni hela ya *stimulus* yapo maeneo ambayo ningombala tuyafanyie kazi. Kunapokuwa na mdororo wa uchumi kwa sababu yoyote ile fedha kama hii inatusaidia kurudi, *ku-bounce back*, kwenye kuendeleza uchumi. Tunayo bahati hatukufunga biashara zetu, hatukujifungia na ndiyo maana katika *record* hata kwenye taarifa hii sisi ndiyo pekee tulikuwa tuna ukuaji chanya mwaka 2019, wenzetu walikuwa na 0.3, 0.8, wengine -3.4, sisi tulikuwa tuna 4.6 kwa sababu hatukujifungia tuliendelea na kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hatujapeleka kwenye *ku-stimulate* biashara kama *stimulus*, ningombala sana tuziangalie biashara zile zilizodhurika sana moja kwa moja na kuwepo kwa UVIKO-19 hasa kwenye utalii na hoteli. Kwa sababu, hatuwezi kuwapa hela na kwa sababu Wabunge wengi wameongelea riba za benki kwa ujumla, mimi ningesema tuwe na kipengele sasa cha kuzisaidia kabla hatujaja kwenye riba za ujumla. Kwamba, kampuni zile nyinyi zina mikopo benki, zimefanyiwa *restructuring*, zinalipa *interest* bado na baadaye watatakiwa walipe na ile *principle*,

tuweke *restructuring* ambayo tutaziangalia zile sekta na zile biashara tuzielekeze benki ziwapunguzie riba, ikiwezekana zisimamishe riba mpaka watakapokuwa wame-stabilize ili kuweza kuimarisha uchumi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo niende kwenye mpango wetu huu. Watu wengi wameongelea kilimo na mimi sitaacha kuongelea kilimo. Kuna vitu bado tunaendelea kuchanganya, kuna suala la mchango wa sekta ya kilimo kwenye *GDP*, hiyo ndiyo asilimia 29.1, lakini kuna suala la mchango wa kilimo katika ukuaji wa uchumi, ile asilimia Nne tulioitaja ambayo inaonekana ndiyo tulikuwanayo 2019 ilichangiwa sana na sekta ya kilimo ambayo kwa kipindi kile ilichangia kwa asilimia 26.1. Sasa kwenye kilimo kuna nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa sababu wewe ultoa mwongozo kwenye bajeti iliyopita. Katika bajeti iliyopita ya trilioni 36 kwenye kilimo ilienda bilioni 294, *it is less than 1%*, wakati imeajiri *directly* zaidi ya asilimia 55 ya Watanzania, lakini kwenye myororo wake, usafirishaji, usindikaji, na adhalika ni asilimia 70 ya watu wameajiriwa pale, lakini tumewapa *less than one percent* ya bajeti yetu, hatuwezi kusonga mbele kwa namna hiyo. Kwa hiyo, ninashauri sana hata ikiwezekana bajeti ijayo hata asilimia 10 ikiwezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea umwagiliaji siyo vitu vya kutoka mbinguni. Bwawa la Nyumba ya Mungu limetengenezwa miaka ya 70, siyo ziwa ni bwawa litengenezwa na ni baada ya uhuru. Tunaweza kutengeneza mabwawa ya namna hiyo maeneo mbalimbali yakasaidia umwagiliaji pamoja na kilimo cha uvuvi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba bajeti ijayo iangalie sana hii sekta ya kilimo. Tungetamani yale maeneo ambayo yamefanyiwa *research* yanaonekana mazao fulani yanafaa *tu-substitute*, hawa vijana wa bodaboda, bodaboda inauzwa milioni mbili na laki tano, ukiangalia tukiweka maeneo ya ardhi yenye rutuba ambayo

yana tija hawa vijana tunawahamishia kule wanalima na pato letu linaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na sekta ya kilimo ni kwenye mifugo. Wafugaji wetu ni wafugaji wa kitamaduni, hawafugi kwa ajili ya kuza kwa sababu, wao wanaamini wale ng'ombe ndiyo hela yao. Inahitajika elimu tujitoe hapo. Hapo Kongo soko la nyama lina thamani ya bilioni 70 kwa sasa au zaidi na wanununa nyama kutoka Belgium, Netherlands, Ujerumani, South Africa na India, lakini sisi hatuuzi nyama hapo na wako jirani tu. Tuwafunze wale wakulima wetu kwamba, hawa ng'ombe unaweza kuwaweka benki kwa kuwafuga vizuri, kwa kuzingatia njia za kisasa tukauza nyama tukapata hela za kigeni tena kuanzia hapa jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Serikali, imefanya kazi kubwa sana kwenye sekta ya afya. Tatizo kubwa sasa baada ya kuboresha hospitali za Wilaya na kutengeneza vituo vya afya na hospitali za Mikoa ni watumishi na kila tukiuliza tunaambiwa kuna utaratibu unaitwa *wage bill* kwamba, hatuwezi kuajiri tena tusubiri. Sasa kama chanzo cha mapato hospitali za Kanda ziwezeshwe kwa sababu, tumeshaweka vifaa. Tuangalie namna ya kutumia wataalam hata kwa *contracts* siyo kwa kuwaajiri ili tuangalie soko la *medical value tourism* ambayo India mwaka 2020 walikuwa wanatabiriwa kuwa na kipato cha kama *Nine billion dollars* kutokana na watu wanaoingia pale kwa ajili ya kutibiwa, ikifika 2022 wanasema itakuwa na thamani ya *13 billion dollars*. Kwa hiyo, hizi hospitali za Kanda tukishaimarisha hizi za chini zile tuziwekee utaratibu ambao tutaweza kuzitumia kama sehemu ya kipato nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mfano ni rahisi mtu anayetoka Mombasa kutibiwa *KCMC* kwa *distance* na ghamama kuliko kwenda Nairobi na imekuwa ikitokea hivyo hata katika *level* hii tuliyopo. Tukiangalia na Kanda nyingine za Mwanza na huko Kusini tunaweza tukaingiza hela kupitia kwenye *medical value tourism*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chanzo kingine cha mapato ni upimaji wa ardhi yetu. Ukipapima ardhi kinachofuata ni kodi. Ikiwezekana, ingewezezana tungepima nchi nzima kila mahali kuwe na hati, lakini mimi maeneo haya nina *special interest*, miji mingi ukiangalia tunafanya kazi sasa hivi ya kurasisimisha makazi kwa sababu, hatukupima kule ambako Mji unapanukia kwa hiyo watu wakajenga kiholela. Tunarasimisha makazi ambayo siyo mazuri ni holela na hayawesi kuboreshwa kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini miji yote katika fedha ambazo tutazipata karibuni tuweke vifaa kwenye Halmashauri au kila Mkoa vyta kupima ardhi kila Mji unaonekana unakua kuelekea wapi, tupime maeneo yale, tutoe hati, watu walipe kodi, hicho ni chanzo cha mapato kizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kukuza uchumi wetu. Miradi mikubwa yote wanapewa Wakandarasi wa kutoka nje, siyo jambo bayu ni mahusiano, lakini ikumbukwe kwamba, wakishamaliza fedha kubwa au sehemu kubwa ya fedha ile inaenda nje. Sasa kama fedha tayari tunazo na tunaogopa kuwapa wakandarasi wetu tunaona kama hawatafanya vizuri, kwa nini tuisitengeneze utaratibu ambao tutawasimamia vizuri zaidi fedha zile zibaki hapa? Hao mabilionea tunaongelea 5,000 wawe 10,000 keshokutwa wafike 1,000,000 kwa kuwasimamia vizuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuwa na miradi mikubwa unaona hela yote inaenda kwa wakandarasi kutoka nje. Yaani kwa mfano sasa hivi hata hao mabilionea ukiwaita, nadhani ukiwaangalia wazawa hasa utaona ni wachache tu watakuwa hapo, lakini hawa waswahili wa kawaiida...

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Priscus pokea Taarifa.

TAARIFA

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba, anachosema ni kweli, mbaya zaidi tuna bodi...

MWENYEKITI: Anachokisema kipi?

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la kuwapa kazi kubwa wakandarasi wa nje, uhakika ni kwamba, tuna Bodi ambayo inasajili Wakandarasi wa ndani na tuna fedha nyingi Serikali inawalipa waajiriwa wa bodi ile, lakini tuna-*entertain* kufanya kazi kwa kutumia *force account* wakati tunajua *value* ya *private sector* katika nchi yoyote ya maendeleo duniani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Priscus unapokea Taarifa hiyo.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante kengele imeshalia. Mheshimiwa Priscus unadhani kuna mabilionea wangapi Moshi pale?

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ngumu kusema maana hatuna *access* ya kujua. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Wanazidi 10? Ahsante tunaendelea Waheshimiwa. Mheshimiwa Shigongo nilishakutaja. (*Kicheko*)

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono hoja na baada ya hapo nitoe shukrani nyingi sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita, Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa mambo ambayo ameyafanya kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa ajili ya miundombinu, niendelee tu kukumbusha kwamba, barabara ya kutoka Sengerema kuelekea Nyehunge - Buchosa bado

inahitaji kutiwa angalao lami ili wananchi wa Buchosa nao waweze kuona lami kwa mara ya kwanza katika maisha yao. kwa hiyo, nilitaka tu kukumbusha hilo kabla sijaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo nitazungumzia maeneo mawili. Eneo la kwanza kama walivyotangulia wenzangu nitazungumza juu ya kilimo cha nchi yetu na baada ya hapo nitazungumzia suala la uweshehaji wa wazawa wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha nchi yetu kama ambavyo tumetangulia kusikia kinaajiri watu asilimia 65. Mchango wa kilimo kwa Taifa letu kama ambavyo tunesikia wote ni asilimia 26.9 ya pato la Taifa. Hii ni dalili kabisa ya kwamba, kilimo chetu kinatoa mchango mkubwa sana kwa Taifa letu. Sasa nimeusoma mpango, nimepitia ndani, sijaona mahali popote ambapo wamezungumza juu ya taasisi zifuatazo: Sijasikia wamezungumza juu ya *TANTRADE*, sijasikia wamezungumza juu ya *TIRDO*, sijasikia wamezungumza juu ya *TEMDO*, *CAMARTEC* na *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazitaja hizi taasisi? Nazitaja kwa sababu ya mfano wa nchi kama Taiwan, ninapozungumzia suala la maendeleo ya kilimo huwa napenda sana kuchukua mfano wa nchi ya Taiwan. Watu wa Taiwan mwaka 1950 walifikia uamuzi ya kwamba baada ya vita ya pili ya dunia walime na wakaamua kulima sana na wakawa wana-export mazao kwa wingi sana kwenda nchi za nje, lakini baadae wakasema haifai kuendelea ku-export mazao ghafi, badala yake ni bora waanze kutengeneza bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichokifanya ndiyo hicho ambacho Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliki-copy na kukileta hapa nyumbani ya kwamba, tunalima halafu tunatengeneza bidhaa ndiyo tunazipeleka nje. Alipokuja hapa Mwalimu alikuja kuanza na taasisi ya kwanza ya *Board of Internal Trade* na baadaye akawa na *Board of External Trade* ambayo kwa sasa inaitwa *TANTRADE*

ambayo kazi yake ni kutafuta masoko ya bidhaa mbalimbali. Kwa hiyo, tulikuwa tunaanza sokoni kutafuta kwanza masoko halafu tukishapata masoko tunakuja hapa nyumbani tunawaambia sasa nyie watu wa Tanga mtalima katani, nyie watu wa Kilimanjaro mtalima kahawa, watu wa Mwanza mtalima pamba kwa sababu soko lipo, hilo ndilo liliikuwa likifanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo taasisi za utafiti kama *TIRDO* ilikuwa inafanya utafiti wa kutengeneza vifaa vya kiwandani, mashine za kiwandani kwa ajili ya kutengeneza bidhaa kutokana na kilimo tulichokuwa tunafanya. *TEMDO* walikuwa wanafanya pia na wenyewe utafiti na *CAMARTEC* wanatengeneza mashine za kutumia katika kilimo chetu huko vijiji. Sasa sijaona kiasi cha fedha ambacho kimetengwa kwa ajili ya taasisi hizi. Ndiyo ninataka kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ni bora akallizingatia suala hili kwa sababu hatuwezi kunufaika na kilimo chetu kama tutaendelea tu ku-*export raw* mazao ambayo ni ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo la muhimu sana ni kuhakikisha kwamba, tunatengeneza *products* na tunazi-*export* kwenda nje. Nilitaka kukumbusha kuhusiana na suala hilo ni la muhimu sana kwa ajili ya kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia suala hilo nataka nizungumzie suala moja muhimu sana juu ya *National Whisper*, yaani mnong'ono wa Taifa. Sisi kama Taifa, kama Tanzania, tunanong'ona nini juu ya wafanyabiashara wetu? Tunanong'ona nini juu ya vijana wa Taifa hili? Tukiwa tumekaa peke yetu sisi wenyewe tunaongea nini juu ya maendeleo ya vijana wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasikitika tu ya kwamba, vijana wetu wa Tanzania walioko katika nchi hii hatuwapi kipaumbele kikubwa linapokuja suala la maendeleo ya Taifa lao. Nasema hivi kwa sababu, wote tunaona kwa macho na wote tunashuhudia kabisa kwamba, vijana wetu tunawapeleka shule, wanasona, wanapata elimu, wakitoka shuleni wanakuwa hawana chakufanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kuanza kufikiria namna ya kuanzisha mfuko wa ubunifu wa Taifa ambao utakuwa na kiasi cha fedha cha kuwasaidia vijana wetu ili waweze kuwa na ubunifu na mfuko huo uwasaidie kuweza kutengeneza bidhaa mbalimbali ambazo zitaweza kuingia sokoni. Hilo ni jambo muhimu sana kwa ajili ya nchi yetu, hatuwezi kuwa na vijana ambao wamesoma, wana elimu, lakini elimu yao haitumiki kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Kwa hiyo, ninaomba sana na ninaomba nisisitize kwa mara nyingine kwamba ni jambo muhimu sana kuhakikisha ya kwamba, kunakuwa na mnong'ono wa Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnong'ono wa Taifa namaanisha nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zote za nchi hii, utajiri wote wa nchi hii uko hapo chini kwenye hivyo viti vyaa hapo mbele vilivyokaa hapo. Utajiri wote wa Taifa hili uko hapo mbele, nikianzia huko kwa Mheshimiwa Mashimba nikaja mpaka huku kwa Mheshimiwa Kipanga, trilioni 33 za nchi hii ziko hapo chini, nani anazipata, ndiyo swali la kujuliza, nani anazipata? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kunong'ona kama Taifa kwamba, tumeamua kama nchi tenda zote za kuanzia kiasi hiki cha fedha ziende kwa vijana wa Kitanzania? Hatuwezi kuongea kama Taifa ya kwamba, fedha hizi akija mwekezaji ye yeyote katika nchi hii lazima ashirikiane na Mheshimiwa Tale? Maana yake nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, kwa kufanya hivyo fedha hizi zitabaki kwa Watanzania wenye zinazunguka hapahapa nyumbani na tutatengeneza mabilionea wengi ambao unawaongelea hapa ndani. Tusipofanya hivyo watakuwa wanakuja hapa watu na begi baada ya miaka mitano ameshakuwa bilionea anaondoka zake sisi tunabaki tunashangaa. Matokeo yake vijana wetu wanajaa chuki ndani ya miyo yao wanaanza kuchukia Serikali yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ni lazima itengeneze mazingira ya kuwawezesha vijana wa nchi hii kutajirika. *The Government must create environment ambayo ina-foster development* ya vijana wetu. Kama hatutengenezi mazingira ya vijana wetu kutajirika hakuna kijana wa nchi hii atakuwa bilionea na mabilionea wataendelea walewale kila mwaka, mwaka huu na mwaka ujao. Kama tuna nia ya kutengeneza mabilionea wengi ni lazima tuseme kwa nia moja kwamba, tumenong'ona kama Taifa ndani ya chumba ambacho hatuzungumzi wala hatuandiki gazetini wala mahali popote ya kwamba, tumeamua kama Taifa vijana wetu ni lazima watajirike. Kwa hiyo, ukiwa kama ni mradi, Rais wetu alizungumza juzi akasema nimeleta fedha hizi zisaidie wawekezaji wa ndani. Ile kauli tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Buchosa kwenda Sengerema itengenezwe na mzawa. Tukifanya hivyo utajiri huu utazunguka kwa vijana wetu hawahawa ambao tunawatazama leo, mwisho wa siku nakuhakikisha mabilionea wataongezeka. Tusipofanya hivyo tutaendelea kushuhudia watu wanakuja hapa Tanzania baada ya muda mfupi ni mabilionea wanaondoka wanatuacha hapa tunalamika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika wa kuhakikisha kwamba, vijana wa nchi hii, vijana wa Taifa hili wananaufalka na utajiri wa Taifa lao ili mwisho wa siku waweze kuanzisha viwanda wao wenyewe waajiri wenzao hapahapa nyumbani. Jambo hili linawezekana, South Africa walifanya, South Africa walikuja na utaratibu wa *Black Empowerment*. *Black Empowerment* ikawawezesha akina Motsepe na Rais wa South Africa wa sasa kuwa mabilionea mpaka leo. Sisi kama Taifa tunashindwa wapi? Tunashindwa nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kama Taifa kuamua kwa nia moja kwamba, tumeamua kutengeneza mabilionea 20 katika nchi hii, tukaenda *TIRDO*, *TIRDO* wanayo *incubation center* ambapo vijana wetu wana *products* nyingi wamebuni lakini hawana mitaji ya kufanya biashara. Wakienda kwenye benki za biashara kukopa wanaombwa

nyumba na kama kijana hana nyumba hawezi kutengeneza *product* yoyote ile. Hatuwezi kama Taifa kusema, Mheshimiwa Waziri unanisikia, sehemu ya tozo hii tuchukue pesa kidogo tuanzishe *National Innovation Fund* ambayo kijana akiwa na *idea* yake yuko *COSTECH* au yuko *TIRDO* awe *supported* atengeneze bidhaa hatimaye aje aajiri wenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanawezekana. Nia ya wazee wetu wa mwanzo ilikuwa ni kuona Watanzania wanatajirika. Hatuwezi kuendelea kukaa hapa tunashuhudia wanatajirika watu, wanakuja wanatajirika wanaondoka, hatutakubali. Tukiendelea hivi baada ya muda utaanza kuona kutakuwa na chuki dhidi ya kundi fulani la watu. Tuwasaidie vijana wa nchi hii wawewe kufanya vizuri maishani mwao na wawewe kufanikiwa kwa sababu, hii ni nchi yao na wana haki ya kutajirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia mpango huu. Nianze moja kwa moja kwa kuishukuru sana Serikali, kuanzia Rais wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu na viongozi wote kwa miradi mingi ambayo imeelekezwa kwenye Jimbo la Ludewa. Wananchi wa Ludewa walikuwa wanaliwa sana na mamba Mto Ruhuhu, hawakuwa na daraja, wamellilia kwa miaka sita, nashukuru sana, sasa daraja lile limekamilika na wananchi wanaweza kufanya shughuli zao na hawaliwi tena na mamba. Kwa hiyo, naishukuru sana Serikali, ni jambo ambalo limewafurahisha sana wananchi wa Ludewa na wameahidi kuiunguza mkono Serikali kwa nguvu zao zote na uwezo wao wote aliowajaalia Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa daraja lile limekamilika, kwa hiyo, wanaomba pia ile meli ambayo inapita Ziwa Nyasa kuanzia Itungi kwenda Nyasa nayo iweze kuanza safari zake. Kwa sababu kwa muda wa miezi mitano sasa, toka mwezi Mei, ilikuwa matengenezo na wananchi

wanatumia usafiri wa mitumbwi na maboti; hivyo, wengi wanazama kwenye maji na kupoteza mali zao. Kwa hiyo, wanaiomba sana Serikali, huu uchumi ambaao tumesemi umekua kwa asilimia 4.8 na robo hii 4.7 nao wanatamani kufanya shughuli ili uchumi wao uweze kukua. Kwa hiyo wanaiomba sana Serikali meli ile ianze safari zake mara moja, maana katika Ziwa Nyasa, Wilaya ya Ludewa ina kata nane; kuna kata ya Kilondo, Lumbila, Lifuma, Makonde, Lupingu, Iwela, Manda na Ruhuhu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata zote hizi nane zinategemea sana usafiri wa maji kwa sababu maeneo haya yana changamoto sana za barabara. Kwa hiyo, jambo hili linarudisha nyuma jithada za wananchi katika kujishughulisha na uchumi ili nao waweze kuongeza kipato chao na kulipa kodi ili uchumi wa nchi yetu uweze kukua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili, upande wa sekta ya kilimo kuna changamoto moja kwamba hizi sheria zetu nyingine zimekuwa kama zinadidimiza wananchi. Kuna Sheria ya Matumizi ya Rasilimali za Maji; Sheria Na. 11 ya Mwaka 2009. Sheria hii imeanzisha utaratibu kuwa, mtu ye yeyote anayetaka kutumia maji, anatakiwa apate kibali ambalo siyo tatizo; lakini sambamba na kibali hicho, kuna tozo ambazo zimeanzishwa. Sasa wananchi wa Mkoa wa Njombe na hasa Ludewa Kata ile ya Madilu na Madope wanalima sana viazi vya umwagiliaji. Sasa sheria hii inawarudisha wananchi kwenye kilimo cha kutegemea mvua, kwa sababu mwananchi ananunua ma-roll yale ya mabomba, anatafuta maji, anachimba mtaro, anaingia gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inamwanzishia kodi ya shilingi 250,000 na gunia moja la viazi unakuta linauzwa shilingi 12,000. Kwa hiyo, ili upate hizo 250,000 unahitaji siyo chini ya gunia 23. Kwa hiyo, tozo hii naiomba sana Serikali, kwani inakuwa inawarudisha wakulima kwenye kutegemea kilimo cha mvua. Hii iko sana maeneo ambayo yana miradi ile ya umeme wa maji. Hizi jumuiya na haya mabonde yanakwenda kutoa elimu, yanaanzisha jumuiya za watumia

maji. Kule kwangu wananchi wanalia sana na hii tozo ya shilingi 250,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwenye sekta hiyo hiyo ya kilimo, Wabunge wengi wamezungumzia changamoto ya mbolea. Nitatoa mfano wa bei chache ambazo ziko kwa Njombe. Mbolea aina ya *DAP* ilikuwa inauzwa shilingi 55,000 mwaka 2020, lakini sasa hivi inakwenda kwa shilingi 97,000 mpaka shilingi 106,000; na hii mbolea ni muhimu sana kutokana na virutubisho ambavyo vinahitajika kwenye udongo. Kwa hiyo, kuna mbolea nyingine ambayo ni muhimu ya *UREA*, nayo imetoka kwenye shilingi 55,000 mpaka shilingi 80,000 au shilingi 90,000. Kwa hiyo, imepanda karibia mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mbolea nyingine ambayo inahitajika zaidi aina ya *CAN*, nayo kwa sasa inauzwa kati ya shilingi 60,000 mpaka shilingi 72,000 kwa Mkoa wa Njombe. Kwa hiyo, kwa hali hii, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Serikali ina kila sababu ya kutoa ruzuku kwenye mbolea ili bei iweze kushuka irejee kwenye hali yake ya mwaka 2020 au pungufu zaidi ili wakulima waweze kulima mazao yao kama kawaida, kwa sababu imekuwa ni kilio kikubwa sana. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukulie katika uzito wa pekee ili tuweze kumnusuru huyu mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwenye sekta hii ya kilimo, naishukuru sana Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa mahindi. Bahati mbaya sana mfumo uliotumika mwaka huu wa kutumia vikundi vyta ushirika umewaumiza sana wale wakulima wenye gunia tano, sita saba au 15, wengi hawajauza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda *Kijiji* kimoja cha Mkongobaki kufanya mkutano, nikajaribu kuuliza pale wakulima mmoja mmoja ambao waliweza kuuza mahindi. Kwa kweli katika Kata ile ya Mkongobaki nilipata mwananchi mmoja tu. Kwa hiyo, zile tani nyingi hazieleweki zilikwenda wapi? Wakulima wanalia mahindi yanaoza, sasa hivi watoto

wanaripoti Vyuo Vikuu, masomo ya mahindi hakuna. Kwa hiyo naomba hapa napo paangaliwe mfumo ule, ama tungeweza kuwaandaa wananchi kwa kuwapa elimu ya kutosha au tungetumia mfumo wa soko la miaka yote, tusingepitia kwenye hivi vikundi. Kwa Ludewa, wananchi; mkulima mmoja mmoja wameumia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niishukuru Serikali kwenye miradi ya umeme. Miradi ya umeme kwa kweli vijana wa kileo wanasesma Serikali imeupiga mwingi sana. Kule kwangu Ludewa kuna vijiji ambavyo havina umeme kabisa ambavyo ni vitatu. Naomba Serikali iweze kuviingiza kwa wakandarasi hawa *REA*. Kuna Kijiji cha Ndoa, Kijiji cha Kimata na Kijiji cha Kitewe. Vijiji hivi havijaingia kwenye Mpango ili wananchi hawa nao waweze kuona wananaufaika na uchumi huu ambaao uko chini ya Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan ambaye ameelekeza fedha nyingi kwenye Mpango huu kwa ajili ya miradi ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, kuna hii miradi ambayo ya umeme ya wazalishaji binafsi. Kuna Kampuni ya Madope, inazalisha umeme kwa ajili ya vijiji 20. Kwa hiyo, umeme huu umekuwa na changamoto ya mgao wa masaa zaidi ya 12 kwa muda wa miaka miwili sasa. Naishukuru Serikali na Waziri wa Nishati, Bodi ya *REA* imekwenda kule na wameona changamoto hizi.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba ile tathmini waliyofanya ya kutatua hizi changamoto ziende haraka ili Kata ya Mlangali, Lubonde, Madilu, Madope, Lupanga na Lugarawa waweze kupata umeme wa uhakika na wa bei nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye kipengele cha uchumi shindani na hii miradi vielelezo, kuna huu mradi wa Mchuchuma na Liganga, nashukuru sana Mheshimiwa Rais alishatolea maelekezo kwamba miradi hii ianze, amechoka sana kuisikia; na ninafikiri ametambua kwamba miradi hii itatoa ajira nyingi sana. Ajira za moja kwa moja zaidi ya milioni nane pale zitapatikana. Wale wote watalipa kodi Serikalini, Serikali itaongeza mapato nao watapata kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hoja unayoizungumza ya mabilionea, sisi pale tuna makaa ya mawe ambapo leseni zake zote zimeshikiliwa na *NDC* halafu uchimbaji haufanyiki. Kwa hiyo, wangepewa wachimbaji wadogo, nina imani (namwona Mheshimiwa Biteko ananisikiliza vizuri) na sisi Ludewa tungezalisha mabilionea. Naomba wananchi wale waweze kulipwa fidia wakati Serikali inaendelea na majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu wa mawazo kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023. Ni ukweli usiopingika kwamba suala la mafanikio ya Mpango wowote ule ni uhakika wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia mpango husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Waziri ameonyesha kabisa kwamba Mpango huu utagharamiwa na vyanzo vingi ambavyo vimetajwa ikiwemo mapato ya ndani, mikopo, misaada na kadhalika. Sasa ni vema Serikali ikajipanga kuhakikisha mapato ya ndani au makusanyo ya ndani yanaimarishwa na ili tuondokane na mawazo ya kukopa kupitiliza, tafsiri yake ni nini? Ni kwamba kukopa hakukatazwi, ni kawaida, lakini tusikope kupitiliza mwisho wa siku mzigo unauelemea Serikali na wananchi kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kwamba ni lazima tuweke mikakati ya kuimarisha mapato ya ndani kudhibiti mianya ya ukwepaji wa kodi, kuhakikisha ulipaji wa kodi unafanyika kwa uhakika na kuondoa misamaha ya kodi isiyokuwa ya lazima. Kwa kufanya haya na engine mengi, tutaenda kuimarisha makusanyo ya

ndani na hatimaye haya ambayo yametajwa katika Mpango yatafanikiwa kutekelezwa kwa kutegemea kiwango kidogo cha mikopo, lakini kikubwa kitatokana na uhakika wa mapato yetu ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ripoti ya *CAG* na tafiti mbalimbali zilizofanywa, hapa Tanzania tuna upotevu mkubwa wa mapato katika mambo tisa kwa uchache nikiyataja. Jambo la kwanza, kwenye sekta isiyo rasmi au wengine wanaita uchumi holela, tunapoteza takriban shilingi trilioni 2.8. Hoja ya pili, kukosekana kwa ufanisi kwenye Serikali za Mitaa katika ukusanyaji wa mapato, tunapoteza shilingi bilioni 50. Mamlaka za Umma kushindwa kutoa risiti za kielektroniki tunapoteza shilingi bilioni sita. Kama haitoshi, upungufu katika kufuata taratibu za kodi kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa na sekta za Umma, tunapoteza shilingi bilioni 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyininge ya tano ni kutokulipwa kwa malimbikizo na madeni mbalimbali, inaifanya Serikali ipoteze shilingi bilioni 113. Hii ni kwa mujibu wa ripoti za *CAG* na *research* zilizofanywa *Action Aid* ambao wametumia takwimu mbalimbali ikiwemo *NBS*. Kama haitoshi, kuna rufani za kodi ambazo hazijaamuliwa. Kuna hizo ambazo ziko za *Barrick* na wengineo, lakini mbali na hiyo, kuna shilingi trilioni tatu ambayo tunapoteza ambayo maamuzi yake hayajaamuliwa. Kama haitoshi, kuna marupurupu ya kodi yenye madhara ya shilingi bilioni 153 ambayo nayo hayakusanywi. Kama haitoshi kuna mzunguko wa fedha haramu au *illicit financial flows*, tunapoteza shilingi trilioni 2.7 na la tisa, ni mapungufu ya makusanyo ambapo tunapoteza shilingi trilioni 1.4. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa takwimu hizi na *figure* nilizozitaja, ni kwa hakika kama Serikali ingeweka mkazo katika maeneo haya na mengine mengi ambayo sijayataja, kwa hakika suala la kukopa ili kuhakikisha mipango yetu inatekelezwa, tusingeliona kama ni jambo kubwa au la muhimu sana. Ni kwa kufanya mipango madhubuti, mipango sahihi sera sahihi, sera rafiki mambo yote ambayo

yatahakikisha makusanyo ya ndani yanafanyika ipasavyo na haya ambayo tumeyaweka kwenye mipango na ugharamiaji wa Mpango kwa ujumla wake, unafanikiwa kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yanasemwaa muda mrefu hapa Bungeni na sijui kwa nini Serikali inakuwa nzito kutekeleza au kuyasimamia baadhi ya mambo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Halima.

TAARIFA

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa Mheshimiwa Paresso taarifa tu kuwa hoja yake hiyo ya mapato na kutoa ushauri kwa Serikali kuweza kupata vyanzo vingine mbadala; kwa taarifa ya Wizara ya Fedha kwa mfano, inasema kwa mwaka 2020/2021 huu mwaka ambao ndiyo tunamalizia, Serikali imeweza kukusanya kwa vyanzo vyote yaani ukizungumzia *TRA*, ukizungumzia Halmashauri zetu, ukizungumzia makusanyo yasiyo na kodi, yote yaani lile kapu lote, ni shilingi triliioni 20 tu ambazo zinaweza zikafanya mambo *basically* matatu; kulipa deni la Taifa shilingi triliioni 10, kulipa mishahara shilingi triliioni nane na vipesa vile vi-*OC* vile *Other Charges*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, anachokizungumza ni sahihi kwamba *basically* miradi yetu yote ya maendeleo pamoja na kununua yale madege tunanunua kwa pesa za mikopo. Kwa ushauri wako, inakupa taarifa ili u-*boost* pale ambapo unashauri, vyanzo vingine tunaweza tukapata wapi? Ni hilo tu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ilikuwa ni taarifa Mheshimiwa Cecilia, unaipokea?

MHE. CECILIA D. PARESO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naipokea taarifa hiyo. Naamini kabisa kwamba...

MWENYEKITI: Ngoja kidogo Mheshimiwa Cecilia, unapewa taarifa nyingine pia.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Nilitaka niwape taarifa kwamba ni utaratibu wa uendeshaji wa kiuchumi hata ngazi ya familia; unachukua kipato chako kile, unakifanyia *simulation*, unakichukua kwa mkupuo, halafu unatekeleza jambo kubwa; unaanza kurejesha kupertia jambo kubwa ulilotekeleza na jambo kubwa lile ambalo unakusanya. Kwa hiyo, siyo jambo la kwamba hakuna mapato ndiyo maana tunakopa. (*Makofii*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cecilia ndiyo mchangiaji, endelea. (*Kicheko*)

MHE. CECILIA D. PARESO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa yake siipokei. Ni hivi, yaani kukopa siyo dhambi na wala haikatazwi, lakini unakopa kwa ajili ya nini? Unakopa uende kufanya nini ili utakachokopa kirejeshe *on time* na ili uendelee kukopa na hicho utakachokifanya, matokeo yake yaonekane? Mbona ni kitu rahisi tu hiki na kinaeleweka tu. Mimi sio mchumi, lakini naielewa tu kwa namna hiyo, kwamba ni kitu ambacho kinaeleweka tu. Sasa... *anyway*, usinitoe kwenye hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi, mambo yote ambayo nimeyashauri hapa, ya kuimarisha makusanyo ya ndani na yawe endelevu, kudhibiti upotevu wa mapato, kuiweseha *TRA* kwa maana ya rasilimali watu na vyote vinavyowezekana ili waweze kwenda kuhakikisha ukusanyaji wa kodi na mambo mengine yanafanyika, lakini pia kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara. Kwa sababu ukiweka mazingira rafiki, mwisho wa siku kodi inalipika bila kuwa na nguvu au kushurutishana, bila kuwa na hiyo kwamba nikupe risiti au nisikupe risiti. Haya yote yanafanyika kwa kuhakikisha kwamba huu udhaifu tuliuataja unaenda kuimarishwa ili

tukuze ukusanyaji wa mapato ya ndani tuepukane na kukopa kunakopitiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo napenda kuchangia kwa haraka haraka ni suala la deni la Taifa. Hapa tunapoongea, mpaka Septemba mwaka huu 2021, taarifa za *BoT* zinaonyesha kwamba kuna ongezeko la deni la Taifa ambapo mikopo kwa deni la Taifa la nje imefikia shilingi triliioni 59 na deni la ndani imefikia shilingi triliioni 18. Kwa hiyo, jumla yake inafanya deni la Taifa kufikia shilingi triliioni 78. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hali ambayo inatisha, ni lazima tuhakikishe tunakopa kwa vitu ambavyo kwa kweli ni lazima sana tukope na siyo vinginevyo. Kwa sababu tunakoelekea sasa hivi, hii mikopo yote ikiiva, maana yake makusanyo yote tutakayoyapata ya kwanza tunaanza kulipa madeni. Tutafika mahali hata mishahara tutashindwa kulipa kwa sababu madeni yameiva kila kona tulikokopa. Hii ni hatari sana kwa uhai wa nchi na wananchi kwa ujumla. Sasa Awamu ya Tatu illacha deni la shilingi...

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

SPIKA: Taarifa, nakuruhusu mtoa taarifa.

T A A R I F A

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpe taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Paresso kwamba usiwe na hofu na kukopa. Tunapanga kukopa ili kuwekeza na kutokana na kuwekeza tupate na matokeo yake. Unapozungumza miundombinu wezeshi na saidizi inaleta tija kwa maendeleo ya nchi. Wale wasiozijua ndege wanaweza kuzibeba, lakini sisi tunaosafiri na ndege, tunajua maslahi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ya Ardhi inaandika *paperkuja* Serikalini, tunataka Serikali ikope shilingi

triliuni mbili iweke kwenye sekta za kiuzalishaji, *the productive sectors* tuweze kuuza chakula dunia nzima na kufuga samaki na kuuza dunia nzima, ambapo soko la samaki ni dola bilioni 235. Tunataka tuingie kule. Kwa hiyo, kama fursa ipo, usiogope kukopa. Kampuni zote zinakopa na nchi zinakopa. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Taarifa hiyo Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Taarifa yake siipokei na narudi kule kule na napenda anielewe vizuri na Serikali inielewe, kwamba kukopa siyo dhambi na haikatazwi, lakini unakopa ufanye nini ili kuwepo na mapokeo ambayo utaweza ku- *service* mkopo ule ili mambo mengine yasikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongelea habari ya Deni la Taifa na tena nafikiri mliite Deni la Taifa siyo la Serikali, kwa sababu kwenye vitabu humu wameandika Deni la Serikali, ni Deni la Taifa ili Watanzania wajue. Deni la Taifa leo tunapoongea ni shilingi trillioni 78, sijui ni bajeti za Wizara ngapi tulizonazo, sijui ni bajeti ya nchi yote kwa ujumla.

Sasa ninachoshauri ni kwamba, tuangalie tunakopa kwa ajili ya nini, kwa masharti yapi, kwa kufanya nini na kwa matokeo yapi? Haya ni mambo ambayo tunayasema, tutashauri, na tutaendelea kushauri utekelezaji... (*Makofii/ Kicheko*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili, Ahsante sana.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji na kufanya maamuzi kwenye mambo haya siyo Biblia wala siyo *Qurani* mambo ambayo yanabadilika kulingana na wakati na kulingana na uhitaji husika. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Mwanyika, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka.

MHE. DEO P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Mpango na Mapendelezo ya Mpango ulio mbele yetu wa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nijikite kwenye maeneo mawili; eneo moja ni eneo la uwekezaji kwa maana ya Mradi wa Liganga na Mchuchuma na muda ukiruhusu niweze kuangalia Sekta ya Kilimo kama wenzangu ambavyo wameangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu unajaribu kujikita kutoa msingi wa maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa 2022/2023 na umeainisha maeneo muhimu ya vipaumbele. Katika maeneo haya kuna maeneo ya miradi ya kielelezo. Kwenye maeneo haya kuna eneo la Liganga na Mchuchuma; nipende kusema na mwenzangu Mbunge wa Ludewa ameliongelea, lakini mimi nitaliongelea kwenye *angle* tofauti kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kuelewa kinachoelezwa katika Mpango, kuhusiana na mradi huu ni kwamba, majadiliano yanaendelea na tunakubali, lakini tuishauri Serikali kwamba mradi huu ni mradi mkubwa, ni mradi ambao unaweza ukawa *game changer*. Leo nataka nitoe takwimu kidogo tu hapo baadaye za kwa nini Mpango unaokuja ni lazima uzingatie kuona matayarisho ya Mradi huu wa Liganga na Mchuchuma kwa maana ya makaa pamoja na chuma uweze kuanza kuonyeshwa na kuandaliwa wakati majadiliano yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano hayo ambayo hayaishi hatuelewi ni majadiliano gani. Tunaelewa kwamba pengine kuna ugumu kwenye kujadiliana, lakini tufike mahali maamuzi yafanyike na *option* za uwekezaji katika sekta hizi za madini kama chuma ni muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachumi wanasema kuna gharama au kuna hasara ya kutofanya jambo fulani kwa wakati fulani, wao kitaalamu wanaita *opportunity cost*. Sasa tukiangalia sasa hivi bei ya chuma ndani ya miezi 24 imefika dola za Kimarekani kwa tani 400 ni ongezeko kubwa la asilimia 200. Wachina peke yao ndiyo wanao-*dominate* soko hili la chuma kwa sasa. Wanazalisha karibu asilimia 56.5 ya chuma chote duniani. Afrika peke yetu tunazalisha kama asilimia 17, Tanzania ni sifuri, lakini tuna chuma hapa na tuna *resource* hapa kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kusema kuna *research* imefanyika na *Institute* ya *Global for Development Studies* ya *Boston University* ambayo inaonesha katika kipindi cha 2008 mpaka 2019 Wachina peke yao wametoa mikopo ya *financing* ya maendeleo duniani ya karibu dola za Kimarekani billioni 462. Ndani ya hizo dola billioni 462 asilimia 80 imeenda kwenye miradi ya *infrastructure*, maana yake unaongelea bandari, reli, madaraja na kadhalika. Afrika peke yetu tumepata dola billioni 106 katika hizo dola billioni 462.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema ni nini? Hizo dola billioni 106 ni karibu trilioni 230 za Kitanzania. Hoja hapa ambayo Mpango lazima uangalie ni kwamba tuna kila sababu ya ku-*take advantage* ya uchumi wa makaa ya mawe na chuma sasa hivi ili tuweze ku-*benefit* huko tunakokwenda. Kama Tanzania peke yetu tungeweza kupata, maana yake katika hii *80 percent infrastructure* na Afrika ni dola billioni 106, sisi tuna chuma, kama tungekuwa tumeanza uzalishaji hata tukapata asilimia 50 tu ya hiyo biashara ya ujenzi wa *infrastructure* katika maeneo ambayo yanahitaji chuma sana madaraja, *SGR*, barabara, *ports*, zote zinataka chuma, tungepata asilimia 20 tu ya hiyo biashara ya kuzalisha hiyo chuma, bajeti yetu nzima yote trilioni 39 ingeweza kutoka katika biashara ya chuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ipo haja tuone kwamba tuna haja na tuna kila sababu ya kuhakikisha haya majadiliano yanafika mwisho ili tufanye huu uwekezaji katika hili eneo la chuma pamoja na makaa ya mawe. Tuliangalie

vile vile pengine nje ya *box*, kama tunaona maana yake hapa hatuhitaji pesa ya Serikali, pesa ya uwekezaji kwenye maeneo haya ipo duniani na wawekezaji wapo duniani. Kama tuna mwekezaji ambaye hatuwezi kwenda naye anatuchelewesha, tujue kwamba hiyo *opportunity cost* inakula kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa niombe sana sana Mpango huu, ukiangalia kwa mfano katika Mpango, matumizi ya mwaka jana katika robo ya kwanza hata wachukue robo mbili, matumizi ya Serikali kwenye maandalizi ya mradi huu huwezi kuamini wametumia shilingi za Kitanzania milioni 3.7, nadhani ni kuwalipa walinzi wanaolinda yale maeneo. Kwa hiyo ni kwamba hakuna uwekezaji wa aina yoyote kwenye eneo hilo na kwamba ni kama hatuoni umuhimu kwenye hii mradi huu wa kielelezo, ambao ni muhimu. Nchi yoyote ambayo ina chuma leo na ikaanza kuchimba itakuwa na bajeti nzuri, itakuwa na chanzo kikubwa sana cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuliongolea hilo, kwa hiyo nisema maandalizi ni pamoja na kuhakikisha kwamba hizo fidia zinalipwa kutengeneza hilo eneo ili mambo yakikamilika haya ya majadiliano, uwekezaji uanze, siyo tena tuenze kuhangaika kwamba kwenye bajeti hakuna *compensation*, hakuna hela za kulipa. Kwa hiyo Mpango ujaribu kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala pia ya miundombinu, *project* hii ita *entail* vilevile kuendeleza *SGR* kutoka Mtwara mpaka Mbamba Bay mpaka kwenye Mchuchuma. Kwa kweli kwenye Mpango inaonyesha kwamba bado wanaendelea kufanya tathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba haya mambo yaharakishwe kwa sababu si lazima Serikali itumie pesa kujenga *SGR*, tufanye hii kitu tofauti na tulivyofanya kwenye *central line*, kuna watu wanaweza wakajenga kwa pesa zao tu-negotiate nao ili tuweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee haraka haraka kilimo, wengi wameongelea, suala zima la tija katika kilimo tulilliongelea hapa na tumeliongelea muda mwingu kwamba tunahitaji kupata mbolea kwa wakati na mbolea ambayo ni *affordable*. Hali si nzuri wote tunaelewa, tunajua kwamba Serikali itakuja na maelezo hapa kabla Bunge halijaisha kutuambia kuhusu suala la mbolea. Hata hivyo, nipende kusema, tunashukuru Serikali imefanya jitihada za kuona namna gani itashusha bei ya mbolea au itawapa nafuu wakulima. Ukweli wa mambo ni kwamba bado hakuna nafuu, tuiombe Serikali na Kamati imejaribu kuongea na imesema ni vizuri Serikali ikaangalia uwezekano wa kutoa ruzuku katika suala hili la mbolea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuongelea zao la parachichi, kwa sababu nalo ni chanzo kingine kizuri sana cha mapato. Zao la parachichi ukiangalia kidunia Watanzania tumezalisha kama asilimia 0.2 ya mazao yote ya parachichi duniani. Ukweli ni kwamba, Tanzania ndiyo nchi pekee yenye *potential*/kubwa sana ya kuendelea kukamata soko la parachichi katika dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaweza tu kufanya hiyo iwapo tutahakikisha kwamba sasa hivi Serikali ina-*invest* katika kilimo kwa maana ya kuhakikisha kwamba wakulima wote kwenye masuala ya mbegu, ubora wa mbegu, yanaangaliwa kwa umakini sana, kwa nini? Kwa sababu unalima parachichi leo, unaanza kuzalisha baada ya miaka mitatu, lakini *full production* inaanza baada ya miaka saba. Kama mbegu tunazotumia hazina uhakika, hazina ubora tutafika kule mwisho hatuta-*realize* hayo tunayotaka kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana tulikuwa na *promise* ya Serikali ya kuweka mamlaka ya kusaidia...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele ya pili.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba niunge mkono hoja. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Deo Mwanyika na hasa kwa kutukumbusha kuhusu chanzo kikubwa cha fedha tunachowea kukipata kupidia Mchuchuma - Liganga. Hili la Mchuchuma - Liganga limesemwa miaka mingi kweli, yaani miaka, sasa sijui, ngoja tuone mpaka itakapofika bajeti inayokuja kwa kweli kama Serikali hajasema chochote itabidi sasa tusukumane kidogo. (*Makof*)

Tumenyamaza karibu sijui mwaka wa tatu, wa nne tunaiachia Serikali ifike mahali ije ituambie kitu, lakini mpaka sasa hatujui kinachoendelea *exactly* ni nini. Kwa hiyo tungependa wenzetu hawa *Negotiation Team* au nini tujue, maana Wachina wao yule mtu aliyeingia mkataba na hii kampuni walishanyonga siku nyingi pamoja na habari za mtaani, pamoja na wale *line managers* wote wale kwa sababu ya *corruption* kubwa waliokuwa nayo. Hata sijui kwanza tuna *negotiate* na nani kwa sasa.

Kwa hiyo tunahitaji kidogo kujuu habari fulani *critical* kuhusu hili jambo, kwa sababu ni ukombozi wa nchi yetu. Kwahiyohaliwezi kukaa tu pembeni kimya kimya wakati ni ukombozi wenyewe wa sisi kutoka hapa tulipo ni Mchuchuma - Liganga. Kwa hiyo Bunge hili litafika tu mahali ambapo lazima tujue, tatizo nini na liko wapi? Hata kama ni kamati fulani ndogo ili tuweze kushauri na sisi namna ya kwenda mbele. (*Makof*)

Kwa sasa tuwaamini, tuwaachie wenzetu kama ilivyo kawaida, lakini nao hebu *wa-speed up* hawa *Government Negotiation Team*, kwa sababu huenda ni ma-*lawyer* tu hata Wachumi hamna, yaani kuna jambo la uchumi hapa. (*Kicheko*)

Wenzetu hawa ni sentensi, nukta, nini! Hapa uchumi hapa, tunataka kuwahi, uchumi wakati soko la dunia lina

kwenda, lipo juu hivi sasa, tunatakiwa tuwahi hapa mahali, ili nchi yetu iweze kubadilika kabisa kutoka hapa ilipo. Mataruma haya tunayojenga, sijui reli, nini, yote yangetoka Mchuchuma hapo, ni fedha ngapi tungepata, tungepata fedha nyangi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Zuberi nilishakutaja atafuatiwa sasa na Mheshimiwa *Engineer Tumaini Bryceson Magessa*.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango ulio mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa wasaa kwa kusimama mbele yako kuchangia Mpango huu. Vile vile kama ilivyo ada nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa anayolitendea Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili niende nalo mbali kidogo kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna anavyolipendelea Taifa letu. Huu uongozi wetu sasa ni Awamu ya Sita, lakini katika Awamu zote hizo Mwenyezi Mungu amekuwa akituletea viongozi ambao kwa kweli wana kiu kubwa kuliona Taifa letu linatengemaa na linasonga mbele. Kwa hiyo tushukuru sana kwa Mwenyezi Mungu kwa karma hiyo ambayo ametupa sisi Watanzania, kutupatia Viongozi ambao kila kiongozi anayesimama, anasimama kwa ajili ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani hii haitakamilika kama hatutakishukuru Chama chetu Cha Mapinduzi kwa kulea viongozi, kwa sababu hawa viongozi wote wanapikwa ndani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo chama kiendelee kupika viongozi ili Taifa letu liendelee kutengemaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea kwenye Mpango asilimia 90 kama siyo 95 ya waliochangia kuanzia jana mpaka leo wanazungumzia suala la kilimo, hii ni kuona namna gani kuna umuhimu wa kilimo kwenye Taifa letu. Kwa mtazamo

wangu nasema bado kama Taifa hatujaamua kuwekeza kwenye kilimo. Hatujaamua kuwekeza kwenye kilimo kama ambavyo tunawekeza kwa maneno kuipa kilimo hizi semi mbalimbali; siasa ni kilimo, kilimo uti wa mgongo, kama haya maneno yangelingana na matendo yetu, leo kilimo kisingefika hapa tulipofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika mahali ambapo Bodi zetu za Mazao zinaendeshwa na wakulima. Leo tunazungumzia mfano mmoja kama Bodi ya Korosho inaendeshwa na wakulima wa korosho. Kila mkulima wa korosho anapouza korosho yake Sh.25 inapelekwa Naliendele kwa ajili ya kuimarisha utafiti. Kila mkulima anapouza korosho yake Sh.25 inakwenda kwenye Bodi ya Korosho.

Kwa hiyo, mtaangalia taasisi zetu za kilimo zinaendeshwa na mkulima, Bodi zetu za Mazao zinaendeshwa na wakulima, Taifa linafanya nini kuhakikisha hivi Vyuo Vyetu vya Utafiti wanavitengea fedha za kutosha, tuweze kufanya utafiti wa kutosha ili tuweze kuzalisha vya kutosha na kufanya kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, Serikali kwenye Mpango huu napendekeza ije na Mpango mahsusituonyeshe ni wapi tunakwenda kupata mbolea, kipo kiwanda pale kinazungumzwa muda mrefu sana cha *LNG*. Kile kiwanda kingefanya kazi kutupatia malighafi nzuri sana kwa ajili ya kutengeneza mbolea, lakini leo hii tunakwenda kwenye uhuru wa miaka 60 hatuna kiwanda chochote kile cha mbolea chenye uhakika cha kuweza kukitegemea. Hapo utaona kabisa kwamba bado hatujaamua kuwekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu; Mpango huu utakapokuja utuainishie kuna mkakati gani kwa ajili ya kuinua kilimo chetu. Kikubwa ambacho nakiona kwamba hii mipango tunayokuja nayo huwa hatujaifanyia tathmini kila baada ya mwaka. Tunapoletewa Mapendekezo ya Mpango huu, vile vile tuambiwe mwaka jana kwenye kilimo tulikuwa tumepanga nini na tumefikia wapi? Kwa nini hatukufikia

tulipokusudia kufika na kama tumefika, tumefika kwa nyenzo zipi. Kwa akili yangu ya kawaida nasema hatujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala lingine, suala la utalii. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan, ameamua kukuza utalii nchini. Sasa ombi langu kwenye Mpango utakaokuja tuone ni namna gani tunakwenda kupokea hao watalii, tumejiandaa vipi kupokea hawa watalii. Kwa taarifa nilizonazo, hawa wamiliki wa ndege zetu hizi ndogo ndogo ukiachia *Air Tanzania*, kwanza ni wachache, halafu uwekezaji kwa hapa nchini wanasema ni ghali mno na hizi *Regulatory Authorities* nazo ni nyingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo hii mtalii gani atakuja, ambaye anaambiliwa kutoka Dubai kuja Dar es Salaam ni rahisi zaidi kuliko kutoka Arusha kwenda Mikumi, kweli *are we serious?* Kama mtu anatoka nje, anakuja kutalii analipa fedha kidogo, kuliko fedha atakayolipa kutoka Arusha kwenda Ngorongoro. Hili jambo naomba mpango utakapokuja watueleze, mama anahangaika huko kuimarisha utalii na huku Mawaziri watuonyeshe kwamba tumejiandaa, tunazo ndege kiasi gani za kupokea hawa watalii kupeleka kwenye hizo hifadhi zetu na kwenda kwenye vivutio vyetu. Tuna ndege kiasi gani? Tuna watoa huduma wangapi? Jambo hili naomba watakapokuja nalo lizungumzwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo hapa kama nimeanza kulisikia sikia kuna azimio la anga la Jumuia Afrika Mashariki, anga huru la Jumuia Afrika Mashariki, mpango huu utakapokuja utuambie ikitokea azimio hili kweli likaletwa hapa Tanzania tumejiandaa vipi kulipokea, maana inawezekana mkafungua hili anga mkifungua mnawafungulia watu tu ninyi mna ndege tano wengine wana ndege 1,000 unaingiaje kwenye utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mpango utakapo kuja naomba utuelekeze mpango huu utakapoletwa utuambie tumejiandaa vipi kukabiliana na janga hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nijielekeze kwenye sera mara nydingi tunazo sera ambazo zinamipaka yake labda niseme miaka mitano, miaka miwili lakini tunazo sera zingine ambazo hazina *limit* na utekelezaji wake umekuwa ni mgumu sana kwa sababu hatuna kipimo. Mfano tumekuja na sera kuunganisha barabara zetu za mikoa na kila mkoa hatujasema mpaka lini, matokeo yake sasa hivi tumehama tunaenda kuunganisha wilaya wakati bado kuna mikoa bado hatujamaliza kuiunganisha na hii ni kwa sababu hatujajipa muda ifikapo mwaka fulani tutakuwa tumemaliza kuunganisha mikoa tuingie kwenye hatua nydingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sera ambazo zinakuja bila kuwa na muda maalum ndiyo hizo zinakuwa zinatubabahisha tunakuwa hatujui nini tunafanya matokeo yake tunaruka kwenye hatua moja tunaenda hatua nydingine kabla hatua ya pili hatujamalliza, leo hii kuna mikoa bado hatujaweza kuiunganisha lakini tayari tumeshaanza kuunganisha Wilaya kwa Wilaya. Sasa zile Mikoa sijui tumeacha au sera imekufa sijaelewa hapo.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa mfano tuko na sera nydingine kwamba kila kata iwe na kituo cha afya, nashukuru mwaka huu Serikali imekuja na Sera nydingine kwamba siyo kwamba kila kata itajengwa kituo cha afya badala yake tunakwenda kujenga kituo cha afya kwa kimkakati kulingana na uhitaji na mazingira yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini je, tumeshaletewa tathimini tunapokwenda kuiacha ile sera tunakuja na sera nyinge tumeshaletewa tathimini hapa Bungeni kwamba tuonyeshe kwamba ile sera tuliyokuja nayo ya kila Kata na kituo cha afya imetufikisha wapi? Ina shida gani? Na kama ilikuwa na mafanikio kwa kiwango gani? Kwa hiyo, ninaiomba Serikali kwa hayo machache ilikuwa mchango wangu kwa hayo mambo mawili tu Kilimo, Utalii na hii ya Sera. Ahsante sana kwa kunipa nafasi. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka Mbunge wa Liwale. Nilishakutaja

Tumaini Magessa na atafuatiwa na Josephine Johnson Ngezabuke.

MHE. ENG. TUMAINI B. MAGESSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii niliyopatiwa ya kuzungumza leo lakini nakushukuru sana Mwenyekiti kwa nafasi vile vile ambayo umenipatia kuweza kuchangia kwenye mapendekezo ya mpango huu wa mwaka mmoja 2022/2023. Binafsi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa Kazi kubwa anayoifanya na kwa mambo mengi ambayo ameyatoa ikiwemo bajeti ambazo zimekwenda kwenye majimbo yetu matokeo tunayaona tunaamini kwamba kazi inayoendelea kufanya ni nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kutuletea mpango huu mpango ambao tumeupitia na kuusoma unatupeleka mahali fulani kwenye maendeleo tunayoyatarajia, lakini nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati ambaye naye alishauri mambo mengi katika hotuba yake ikiwemo sehemu kubwa ambayo nitachangia ya Kilimo. Binafsi ni muhumini wa Kilimo leo na ninaona kilimo bado kuna kazi kubwa ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Kilimo mwaka jana ilitolewa fedha ya bajeti kama bilioni mia mbili na kitu hivi ambayo kwenye hesabu bilioni mia mbili kati ya tirioni karibu 33 ni fedha kidogo haifiki hata asilimia moja na bado nimeona michango mengi mwenyekiti wa kamati anapendekeza ikiwezekana wapewe bilioni mia nne inaweza ikaleta mchango fulani kwenye maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini kwamba kutoka uhuru sasa tunaingia miaka 60 hivi karibuni baada ya mwezi mmoja tutakuwa tunasherekea miaka 60. Tumekuwa na *slogans* nyingi Kilimo kwanza, uhuru yaani yako maneno mengi ambayo tumeyasema lakini bado Kilimo hiki kinaonekana hakiendi maana yake ni kwamba hatujaamua kufanya kudhamiria kuingia kufanya kazi kubwa kwenye kilimo hiki. Nami nimependekeze tu kwanza hata kabla

sijasema kwamba ni vizuri kabisa kwenye bajeti yetu asilimia kumi ishughulike na kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana bahati nzuri ni mhandisi hatuwezi kupanda mlima kwa *gear* namba tatu lazima tuondoe namba 1 ikiwezekana mahali fulani tuweke hata hiyo *gear* ndogo ili tuweze kupanda vizuri sasa tumekuwa tukienda tunakwenda kwa mwendo wa pole pole ambaao ninaamini hauwezi kututoa. Kwa mfano, tuna hekta ambazo zinfaaa kwa umwangiliaji milioni 29.4 sisi kama nchi tuna *scheme* ambazo zime-cover 0.4 milioni hekta yaani hatujafika hata milioni moja kwenye zile 29 na bado tunajinasibu kwamba watu asilimia zaidi ya 66 wameajiriwa kwenye sekta hii ya Kilimo hatuwezi kufanya kitu, hizi sekta za uzalishaji lazima zipewe fedha za kutosha tudhamirie kufanya hiki kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia wenzangu wanachangia wanaogopa hata kukopa na nini, kukopa hatuna haja ya kukopa bado deni letu stahimilivu hatuna haya ya kuogopa kukopa, tukope tuingie kufanya kazi hii ya kilimo ionekane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo kadhaa ambayo nafikiri tunatakiwa kuyafanya kwa mfano; tunatakiwa kuhakikisha kwamba tunaporesha hafua za mifugo Kilimo na Uvvi ambazo ni sekta za uzaliishaji lazima ziboreshw, lakini tunatakiwa tuboreshe hafua zinazo husika na upatikanaji wa vyakula lakini malisho vile vile na maji, tunatakiwa tuboreshe hafua za huduma za afya za mimea, mifugo na viumbe maji, lakini tunatakiwa tuboreshe hafua za huduma za ugani na usafiri na mafunzo kwa hawa watu wanaoenda kushughulika na kilimo, tunatakiwa tuboreshe hafua za usindikaji na masoko kwa maana na masoko na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile, tunatakiwa tushughulike kuhakikisha kwamba tunaporesha *M and E Monitoring and evaluation* ufuatiliaji wa hii miradi. Sasa siku zote tumekuwa tunazungumza tunataka tuweke milioni mia

nne je, ukifikiria sekta ya maziwa peke yake mpaka leo ninavyozunguza hakuna tone la maziwa nchi hii zinazouzwa nje ya nchi hata lita moja haiuzi, lakini ndani ya nchi bado yako maziwa yanamwagwa huko maporini kwenye maeneo tunayotoka kwa sababu gani hakuna mahali pa kwenda kuyatunza yale maziwa hayawezi kukaa siku nne wala siku tano na sisi tunasema tutaweka bilioni mia nne mwaka jana tuliweka bilioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu ukifungua mapendekezo ukurasa namba 63 utagundua tulivyokwenda kwenye kilimo tumepima *sample* 1,858 kwenye nchi nzima unaweza kupima sample 1,858 za udongo halafu unataka kulima utafiti gani huu tunaufanya siyo kwamba wataalam hatuna namna ya kuwawezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiria nisiseme maneno mengi sana tukubali kwamba sasa Serikali inakwenda kukopa fedha na kuingiza kwenye Kilimo Mifugo na Uvuvi. Niwapongeze Serikali wanaonyesha kabisa kwenye ukurasa namba 18 kwenye kipengele namba 15 ambacho ni XXV kwamba kwenye fedha za covid 19 wamekwenda kuweka bilioni 5 kwenda kusaidia wajasiilamali wadogo wadogo kuboresha vibanda vyao sijui kama itakuwa imeonekana vizuri hii, watu wanaona kama wajasiilamali wadogo wameguswa kwenye hii hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo napo nataka iongezwe kwa sababu wajasiilamali hawa wadogo ndio wakulima wetu, ndio wanaofanya shughuli zote huko tuliko iwekwe fedha bili uoga ukidhamiria kumsomesha mwanao ukaanza kuogopa kila siku hata maliza shule ndiya sababu tumekuwa na miaka 60 lakini bado sekta hizi ambazo zinatakiwa ziwezeshwe ili uchumi uchangamke bado hauchangamki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote ni mashahidi kwamba pato la Taifa linachangiwa kwa asilimia 26.4 na Kilimo. Sasa tunaogopa nini yaani unajua kabisa kwamba huyu ndiye anayeleta maziwa mengi kwanini usimlishe majani

ya kutosha ili atowe maziwa mengi wasiwasi wetu ni nini kama Serikali. Hatuna haja ya kuogopa tuingize fedha kwa sababu hii ni *production sector* tunaamini kabisa fedha ile itarudi kwa sababu hii itakuwa kama biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme wazi kwamba hoja yangu ya leo nataka nijikite hapa tunaanzisha vikundi vidogo vidogo huko tulipo vya wakulima, vikundi vidogo vidogo vya wavuvi, vikundi vidogo vya wasindikaji. Niseme taarifa njema leo nilikuwa kwenye tamasha la *wine* pale ni *NMB* wamesema wasindikaji wale *processors* wote wanakopa kwa asilimia 10 tu humu nasikia wanasema riba itakuwa asilimia 30 wasindikaji imeshatolewa wanakopa kwa asilimia 10 tu. Kwa hiyo tunauwezo wa kufanya usindikaji *processing* ya kwetu kwa asilimia 10 hiyo. Kwa nini tunakuwa na mashaka, Serikali ikope tuingie huko tufanye hivi vitu. Maziwa yakatunzwe, maziwa yakasindikwe, maziwa yakawe processed tuanze kufanya biashara na soko la nje. Nina amini kabisa tukichangamsha hizi *sector* za uzalishaji uchumi wetu utaamka na utakuwa mkubwa kuliko ulivyo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, ahsante sana Mheshimiwa *Engineer Magessa* kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge *actually by the way* niwakumbushe ni kweli alichosema Mheshimiwa Magessa kuna *wine festival* ya Dodoma inaendelea ni vizuri kufika pale yaani *wine* ni bure tu pale, unapiga *wine* sawa sawa kabisa. Kwa hiyo, msikose kufika kufanya *sampling* ya *wine* ya Dodoma ambayo ni *the best in East Africa*. Karibuni sana kwenye maonyesho yale. (*Makofi/Kicheko*)

Nilikwisha kutaja Mheshimiwa Genza halafu utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nami niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mpenzi Mama Samia Suluhu kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya watanzania. Lakini nimpongeze sana kwa kuweza kutuletea chanjo ya UVIKO-19 na kututoa woga tukaweza kuchanja. Mwenyewe tayari nimeshachanja mwanzo nilikuwa na wasiwasi, lakini sasa hivi nimechanja, lakini na wewe nakushukuru kwa kutuhamisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuwashukuru vilevile wasaidizi wake; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mpango, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya wanapita huku na kule kwenda kuwahamasisha watanzania na kuangalia shughuli zinazofanywa nchi nzima nawapongeza sana na Mawaziri pia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa fedha nyingi ambazo amepeleka Tanzania nzima fedha kwa ajili ya barabara kila Jimbo, fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya na fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa madarasa. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa madarasa yanajengwa na nyumba za walimu nazo ziweze kujengwa na niipongeze Serikali kwa kuwa tayari ilishaanza kuajiri walimu, iendelee kuajiri walimu ili madarasa yanapojengwa, nyumba za walimu zinapopatikana na walimu vilevile waweze kuwa wengi na waweze kufanyakazi ya kufundisha vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea maeneo ya wakulima na wapiga kura wangu ni wakulima ukiangalia wakulima wengi wamejajiri kwenye kilimo wakiwemo wanawake na vijana. Nilikuwa naomba Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya kilimo, kwa mfano; ukiangalia mwaka tumekumbana na changamoto ya mbolea kupanda na kufikia mfuko mmoja shilingi 120,000. Ninaomba tuweze kuita wawekezaji waweze kujenga viwanda hatimaye mbolea

iweze kushuka bei na wakulima wetu waweze kulima kilimo chenye tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu umeme; ipo mikoa ambayo haijaunganishwa kwenye *grid* ya Taifa, Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Rukwa. Nilikuwa naomba mikoa hiyo iweze kupewa kipaumbele na yenye we iweze kuunganishwa kwenye *grid* ya Taifa, kwa sababu ukiwaunganisha kwenye *grid* ya Taifa mikoa hiyo wawekezaji wataweza kwenda kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; Mheshimiwa Waziri Mkuu kila siku unakuja Kigoma kuja kuhamasisha kilimo cha mchikichi, lakini kama hakutakuwepo na umeme wa *grid* ya Taifa wananchi wakizalisha michikichi watakosa kiwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa naomba kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kabisa umeme wa *grid* ya Taifa uweze kufika kwenye mikoa hiyo minne niliyoitaja ikiwemo na Kigoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari upo mradi ambaou ulishaanza kuanzia Tabora, Uvinza mradi huo unaendelea naomba Serikali iongeze pesa ili mradi huo uweze kukamilika. Mheshimiwa Makamu wa Rais alipokuja mwezi wa nane alielekeza mradi huo uweze kukamilika Oktoba 2021. Kwa hiyo, naiomba Serikali katika Mpango tunao upanga sasa ipeleke pesa kusudi umeme wa *grid* ya Taifa uweze kufika Kigoma hatimaye wawekezaji waje kuwekeza Kigoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini si hivyo tu hata hospitali zitaweweze kunufaika kwa sababu kwa sasa hivi si wa uhakika hatuwezi kuwa na vifaa kama *MRI*, *ST-Scan*, *X-Ray* na *Ultra Sound* umeme wa uhakika ukiwepo vifaa hivyo vitakuja na wananchi wataweza kurahisishiwa maisha kwa sababu sasa hivi wanafuata matibabu wengine wanaenda Mwanza, wengine wanaenda Dar es Salaam na kutokana na kipato

chao kidogo wengine wanapoteza maisha. Kwa hiyo naendelea kuomba umeme wa *gridya* Taifa uletwe Kigoma na maeneo mengine mikoa ile ambayo sikuweza kultaja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu, naendelea kuishukuru Serikali ya *CCM* katika Mkoa wetu wa Kigoma ujenzi wa barabara wa kilometra 260 wa kutoka Nyakanazi – Kibondo – Kasulu mpaka Buhigwe unaendelea. Tunaomba pesa zipelekwe ili barabara hiyo iweze kukamilika barabara ambayo inaunganisha mikoa, lakini vilevile inatuunganisha na nchi za jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwenye sura ya pili kuhusu hali ya uchumi; nikupongeze wewe mwenyewe kwa sababu kwanza umeendelea kuwaelimisha wananchi na kutuelimisha sisi Wabunge kwa kusema kwamba zipo sheria ambazo wakati mwingine zinahitajika kurudi Bungeni ili zifanyiwe marekebisho kusudi ziweze kuwasaidia watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari yetu ya Dar es Salaam inapitisha mizigo mingi sana, mizigo hiyo inapita inaenda nchi za jirani na mizigo hiyo inarudishwa tena kuja kuuzwa ndani ya nchi yetu. Nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri aangalie kipengele hicho ambacho kitawasaidia wazawa waweze kufanya blashara katika nchi yao. Tofauti na sasa hivi mizigo inapitishwa nchini mwetu inaenda nchi za jirani halafu inakuja kuuzwa nchini kwetu. Kwa hiyo, wazawa hawawezi kushindana na wale ambaowamepitisha mizigo nchini kwetu wanaenda kuuza kwa bei ya chini halafu sisi tunauza kwa bei ya juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Josephine Genzabuke, nakushukuru kwa mchango wako kwenye sekta mbalimbali ikiwemo za nishati, ujenzi, elimu nakadhalika. Nimepata karatasi nyingi Waheshimiwa Wabunge wala

hamna haja kuendelea kuniandikia. Mheshimiwa Waziri Mkuu wanalalamikia kwamba Waheshimiwa Mawaziri wengi na Manaibu hawapo na wengi wao wanaoguswa na michango iliyo mingi ya Wabunge ikiwemo wa Kilimo na Naibu wake, uwekezaji, nishati, viwanda, biashara sijui miundombinu nakadhalika wanawaorodhesha wao wenyeewe makaratasi kibao hapa. (*Makof!*)

Leo Ijumaa jamani, Ijumaa jioni, kwa hiyo, huenda mambo mengi wikiendi wengine hawawezi kukaa wikiendi hapa lazima waende Dar es Salaam.

Tunaendelea Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusekengile. Karibu Mheshimiwa.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Mapendekezo na Mwongozo wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujikita katika maeneo mawili ambayo ninafikiria ni vizuri na mimi nikatoa mchango wangu, nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia, kwa kazi kubwa anayoifanya kuhakikisha kwamba anatuletea maendeleo na kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hivi karibuni amekuwa akisafiri huku na huku kuhakikisha kwamba Watanzania tunaendelea kunufaika na mambo yote mazuri ambayo yako duniani, hasa katika suala zima la janga ambalo lilikuwa limetupata la UVIKO-19. Tumeona ni jinsi gani ambavyo ameweza kutafuta fedha na kupata zaidi ya trilioni 1.3 kwa ajili ya kupambana na UVIKO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iakini hakuishia hapo, alifikiria mbele zaidi akaona fedha hizi ni vizuri kuzipeleka kule ambako ndiyo kuna chanzo cha tatizo. Zimekwenda kujenga

shule, kupunguza msongamano, lakini zinakwenda kujenga vituo vya afya kuhakikisha kwamba huduma zote za kukabiliana na UVIKO-19 zinaimarika. Haitoshi, tunajua chanzo na njia moja wapo ya kujikinga na UVIKO ni kunawa mikono, ameimarisha mfumo mzima kupeleka fedha kwa ajili ya kupata maji safi na salama. Kwa hiyo, ninapongeza sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujikita katika suala zima la kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Uchumi bila viwanda haiwezekani, itakuwa ni ndoto. Ninapongeza sana Wizara kwa kuona kipengele hiki kuhakikisha kwamba inajenga uchumi shindani na maendeleo kwa watu. Lakini maendeleo kwa watu hayawezi yakaja kama viwanda vyetu nchini haviongezeki au vilivyopo havifanyi kazi kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Shinyanga kuna kiwanda cha nyama kimejengwa mwaka 1951. Toka kilipojengwa hakijawahi kuzalisha hata kilo mbili za nyama, kina eneo kubwa sana la uwekezaji, Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kwamba inaomba lile eneo kwa ajili ya kutengeneza mazingira ya uwekezaji, kuwavutia wawekezaji wengine ambao wanahitaji kuja katika Mkoa ule kuwekeza ili waweze kupata ardhi na kuweza kujenga viwanda vingine au kuboresha kiwanda kilichopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo liliopo ni kwamba lile eneo la kiwanda cha nyama liko chini ya Wizara ya Mifugo pamoja na Wizara ya Fedha. Tumekuwa tuki-struggle sana tuweze kupata lile eneo ili wanapokuja wawekezaji Mkoa wa Shinyanga ardhi ipatikane bure, wenye waweze kujenga viwanda, waweze kulipa kodi, lakini waweze kuajiri vijana ambao ni vijana wengi sana hawana ajira sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imefanyaika Kahama, kulikuwa kuna eneo Kahama linaitwa Zogomela, lina hektaa zaidi ya 2,000. Halmashauri iliomba Wizara ya Mifugo – lilikuwa eneo la Wizara ya Mifugo, likatolewa kwenye Halmashauri

ya Manispaa ya Kahama, wameweza kuweka uwekezaji. Sasa hivi mwekezaji anapofika Tanzania akitaka kuja kuwekeza katika baadhi ya Halmashauri ambazo zina fursa ya kuwekeza moja wapo ni Kahama, mwekezaji anapewa ardhi, anajenga kiwanda, analipa kodi zote za Serikali za ardhi na kadhalika lakini anazalisha ajira nyingi kwa wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Wizara ya Mifugo na Wizara ya Fedha zisitoe lile eneo ambalo liko *Tanganyika Packers* pale Shinyanga na eneo lingine la Chibe ambalo lina zaidi ya hekta 8,000, limekaa tu halina kazi, Wawekezaji wanapokuja wakitaka ardhi kwenda kulipa fidia kwa wananchi wa kawaida inakuwa ni gharama kubwa sana. Anaangalia mkoa mwingine ambaao una fursa ya ardhi ambayo haina masharti makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ninaomba katika suala zima la kutaka kuhakikisha kwamba uwekezaji wa viwanda kwa maendeleo ya watutuangalie na maeneo ambayo tuna ardhi kubwa, iko chini ya Serikali, wawekezaji wanakuja wanahitaji kupata lile eneo ili waweze kuwekeza, basi kusiwe na milolongo mingi ya kuweza kutoa lile eneo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia kuhusu suala zima la kilimo. Kila Mbunge anayesimama hapa anaongea kuhusu suala la kilimo, na wengine wataendelea kuchangia sekta ya kilimo kwa sababu ndiyo uti wa mgongo. Suala zima la kilimo tumeona kabisa kwamba katika mpango huu sekta ya kilimo inachangia Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 26, lakini huu ni ule ulimaji wa kawaida wa kutegemea mvua, na tumesha ambiwa kabisa mwaka huu mvua zinaweza zikawa siyo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali Tanzania tunajipangaje kwa mpango wa muda mrefu kuhakikisha kwamba nasi tunabadilika kama nchi ya Israel ilivyobadilika, kama jinsi ambavyo Dubai imebadilika. Nchi zile ni majangwa lakini wameweza kuhakikisha kwamba wanaboresha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku kwenu Kongwa huku, kipindi cha masika kuna maji yanapotea hovsky, ukishavuka sehemu moja ya Chamwino huku kama unakwenda Dar es Salaam masika maji yanajaa sana mpaka magari yanachukuliwa na maji.

Ukienda *Bahi Road* huku kama unakwenda Shinyanga kuna eneo pale la Bahi, maji yanajaa mpaka yanapotea, Serikali ije na mpango wa kuhakikisha kwamba na sisi tufike hatua Tanzania tuweze kuvuna maji. Mbona nchi nyine wameweza? Hawakuanza mara moja, ni mpango wa muda mrefu, ni ambao unatumia fedha nydingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tufikirie sasa kwamba kwa miaka ijayo tuhakikishe kwamba tunatafuta fedha za kuweza kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji ili sasa tutoke pale kwenye Pato la Taifa la asilimia 26 tuweze kwenda juu. Tumeona kabisa kwamba kuna uhitaji lakini mbali na suala zima la umwagiliaji bado kuna tatizo la bei kubwa za pembejio.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana, ni kengele ya pili Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava. Nilikutaja Mheshimiwa Simon Songe.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru nami kwa kunipa nafasi kuchangia Mpango wa Bajeti 2022/23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kipekee sana nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya kwa ajili ya Watanzania. Kipekee pia nimshukuru kwa fedha ambazo ametupatia hivi karibuni kwenye majimbo yetu, trilioni 1.3 katika sekta mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchomekea hapo eneo la elimu. Ni kweli kuna kazi zinafanyika kubwa kwenye Majimbo sasa, madarasa yanajengwa, tunamshukuru sana. Lakini ukweli lazima tukubaliane kujengwa kwa madarasa lazima kuwe *directly proportional* na upatikanaji wa Walimu. Kwa hiyo mimi niishauri Serikali ije na mpango katika Bajeti ya mwaka 2022/23 wa namna gani tunakwenda kuajiri walimu ili wakabiliane na wanafunzi wengi ambao wanakwenda kutumia madarasa haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunavyokuwa tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia madarasa pia tunamshukuru kwa sababu ni imani yangu kwamba tunakwenda *ku-create ajira* kwa ajili ya Watanzania na Walimu ambao bado hawajapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie maeneo machache sana ya mpango huu. Taarifa ya Kamati ya Bajeti pamoja na taarifa ya Mheshimiwa Waziri imeonesha kwamba mwenendo wa Shilingi yetu ya Tanzania unazidi kuimarkika. Lakini niseme tu kwamba ili shilingi yetu iendelee kuimarkika zaidi ni lazima tufikirie *ku-export final product* kuliko kuwa na *importation* kubwa ya *raw material* kwa ajili ya viwanda vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tunazungumza hivi? Ni lazima tuimarishe viwanda vyetu vya ndani na kuendelea kujenga viwanda mbalimbali ambavyo vitatoa *final product* kutokana na malighafi ambayo sisi wenyewe tunatengeneza hapa, malighafi nyingi zipo zinatokana na kilimo. Tuchukulie mfano kule kwetu Mkoa wa Simiyu na Mikoa ya Tabora, Mara na Mwanza, tunalima sana pamba, lakini pamba bado haina thamani kwa sababu hatutengenezi *final products* zinazotokana na pamba, isipokuwa tunafanya *exportation* ya *material*/ambayo kule wenzetu wanakwenda kutengeneza *final product*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeishauri Serikali, kuna andiko lilishaletwa Wizarani, Wizara ya Fedha na Wizara ya Viwanda, kujenga kiwanda Mkoa wa Simiyu ili uweze

kuhudumia Mikoa ya jirani, na kiwanda hiki kitakuwa cha vifaatiba vitokanavyo na pamba. Tunajua tunaweza tukapata gozi, tunaweza tukapata mashuka. Tutaokoa fedha nydingi za kigeni ambazo tunakwenda kununua vifaa hivi nje, vitaendelea kupatikana kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki pia kitatoa ajira kwa Watanzania, zaidi ya Watanzania 1,000 wataajiriwa kupitia viwanda hivi. Kwa hiyo tunapokuwa tunazungumza habari ya viwanda tunazungumza habari ya *ku-maintain* fedha yetu ili isiendelee kushuka thamani yake bali iendelee kupanda kwa kuwa na *products* ambazo zinapatikana kwenye nchi yetu. Mfano umeutoa, hata hivi vyuma ambavyo vinatengeneza reli tungekuwa tumetengeneza kupitia Liganga huko wataalam wanasema wala tusingekuwa na haja ya kuagiza. Maana yake fedha yetu ingeendelea kuimarika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye kuimarika kwa fedha mimi huwa najifikiria swali moja, sijui wataalam wanasemaje, lakini huwa nawaza kwa nini mimi niko kwenye nchi yangu Tanzania ninakwenda hotelini naambiwa *charge* ni dola 200. Sasa nawaza kwa nini naambiwa dola 200 kwenye nchi yangu, si niambiwe tu laki nne ya Tanzania nijue? Kwa nini, kwa sababu *demand* ya dola itakuwa kubwa kuliko *supply* na *demand* ikiwa kubwa maana yake fedha yako ya Tanzania ina-depreciate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najua wataalam haya wanashauri na mimi naomba niseme kama ambavyo amepiga marufuku Mheshimiwa Simbachawene hivi karibuni kutupa pesa chini wakati wa kutunza vikundi mbalimbali, kuna haja sasa Mheshimiwa Waziri kuja na sera ya kukataza *charges* zozote ambazo wana-*charge* katika fedha za kigeni. Hakuna sababu ya kwenda kwenye hoteli ukaambiwa dola, maana yake itabidi ukatafute dola ili uende ukalipe hiyo *charge* ambayo utakuwa umeambiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda siku moja pale...

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Kabla ya taarifa, Wasukuma mtaipata, mlizoea kutupatupa hela chini sasa mtakamatwa wote. Taarifa inatokea upande gani? Mheshimiwa Ester.

T A A R I F A

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa taarifa Kaka yangu, jirani yangu pale Mbunge wa Busega, kwamba ukienda nchi zingine ukifika *airport* lazima utabadiilisha dola ili uweze kutumia kwa pesa za nchi husika, kwa hiyo ni jambo zuri.

MWENYEKITI: Unapokea taarifa Mheshimiwa Lusengekile.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea kwa mikono miwili kwa sababu nilienda hoteli moja hapa Dar es Salaam nikanywa soda nikaambiwa dola moja, yaani nikawaza kwa nini naambiwa dola moja, si aniambie tu elfu mbili njue. Lazima tuheshimu fedha yetu, tukiheshimu fedha yetu itakuwa na thamani, hakuna sababu ya ku-undermine fedha yetu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha liangalie hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kwa hiyo Musukuma wewe unakwenda kwenye hoteli hujui hata malipo yatakuaje? Endelea mtani. (*Kicheko*)

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* hapa siyo kujua ni shilingi ngapi, *issue* hapa ni kuniambia anani-charge kwa dola hiyo ndiyo *issue* yangu. Mimi hata kama angesema 5,000 sina tatizo mtani, lakini shida ni kuni-charge kwa dola. Kwa hiyo, nataka tuimarishe shilingi yetu kwa namna ya pekee sana ya kuiheshimu fedha yetu. Mtu akifika *airport* pale ana dola zake atafute benki ilipo abadilishe achukue fedha zetu za ndani aende akaanze kutumia, hapo tutaimarisha shilingi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la riba, tumeona kwenye taarifa ya Kamati ya Bajeti. Wastani wa riba za mabenki kwenye kukopesha sekta binafsi tumeona ni asilimia 16.6. Ni kweli riba hizi ni kubwa na tunatamani mabenki yetu yapunguze riba.

MWENYEKITI: Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ya kwanza.

MWENYEKITI: Hapana, kengele ya pili.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Busega. Mheshimiwa Kiswaga. Mjitätahidi sasa kwenda kwenye pointi moja kwa moja kwa sababu dakika za mwisho mwisho, najaribu kupata wote ambaao walikuwa na nia ya kuchangia ili angalau waseme kidogo. Mheshimiwa Kiswaga, endelea.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru hata na mimi kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo katika mapendekezo haya ya mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa ufupi tu kumshukuru Rais kwa kazi kubwa anayoifanya, tumtie moyo kwa hatua kubwa ambazo ameweza kuzifanya, hata pia kukaribisha uwekezaji na kufungua milango, najua nchi itakwenda kufunguka kwa mapana yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuchangia sehemu ya kilimo, kama ulivyosema twende moja kwa moja. Kwa kweli na mimi ninataka nizungumzie kidogo habari ya kilimo. Tukiangalie kweli kilimo, kama Serikali kwa kweli tumekuwa na mipango mingi lakini tumeitawanya mno, kama tunasema kwamba kilimo kinachukua asilimia 66 ya

Watanzania wote, basi kwa kweli tuwe na mikakati ambayo baadae itaweza kutuletea matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia habari ya ruzuku bado na mimi naona kuna umuhimu wa Serikali kuweka ruzuku kidogo kwa sababu nkiangalia hali ilivyo huko sokoni kwa maana hasa ya pembejeo, kuna sababu ya Serikali kuangalia katika mpango huu. Ruzuku siyo jambo geni, ukiangalia nchi ambazo zinaongoza duniani kwa ruzuku, kwa mfano anasema Ufilipino na Indonesia wao kwenye Pato lao lile la Taifa wanaweka asilimia 3.1. Lakini ukiangalia kwa mfano India asilimia 25.1 ya fedha zote zinazokwenda kwenye ruzuku kwa maana ya kwenye madini, ujenzi, miundombinu, wao asilimia 25 inakwenda kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Marekani pia kwa miaka minne tangu mwaka 2017 mpaka kufika 2020 walianza na dola Milioni Nne na sasa wamefika dola Milioni 20 wakiongeza ili kuweza kufidia yale mapungufu ambayo yametokea kwenye kilimo na sababu ni kwamba ni lazima kuweza kuboresha uchumi wa nchi unaotokana pia na kilimo kwa sababu pia ni lazima tule, lakini pia inasaidia kuweza kuboresha bei, kuhakikisha kwamba bei zinaendelea kuwa imara na wakulima wanapata kipato chao. Kwa hiyo, Serikali hili iliangularie kwa huruma yake. Najua inafanya mambo mengi lakini na hili la ruzuku iangularie ili mwakani tusiingie kwenye baa la njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi haina shida ya chakula, kwa mfano ukiangalia sasa mahindi ni mengi, lakini shida tuliyonayo ni masoko. Sasa suala la masoko hili ni muhimu sana. Ukiangalia Nchi ndogo kama ya *Swaziland* ambayo wana ng'ombe kama laki sita, unakuta wao wana mikataba na nchi za Ulaya, wanauza nyama nyngi kuliko sisi ambao tuna ng'ombe milioni karibu 33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa walichofanya ni nini ni kusiani *bilateral agreements*, yaani mikataba ya nchi na nchi ya kufanya biashara, lakini sisi ni nchi kubwa tumeshindwa kusaini mikataba ile fungamanishi na nchi mbalimbali

ambazo tunaweza tukafanya biashara kubwa zinazotokana na kilimo. Kwa hiyo hilo nalo ni la kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo nilitaka kuangalia ya kuongeza mapato kama ulivyo sema, nilikuwa nafikiria hapa kwenye upande wa *transfer* ya *properties*, hasa majengo na viwanja. Eneo hili unakuta kwamba kuna pesa nyingi sana ambazo zimeendelea kushikiliwa. Ninaishauri Serikali kwamba ikiona inafaa tunaweza tukapunguza ile asilimia 10 ya *transfer* ikaenda asilimia tano, siyo lazima iwe ya kudumu, inawezekana tukafanya kwa mwaka mmoja wa bajeti, labda mwaka tu mmoja wa bajeti tukasema kwamba tunapunguza asilimia tano ili tuchochee watu ambao wana mali ambazo hazihamishiki wakahamisha maana ni eneo lingine ambalo pia Serikali inaweza kupata mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia habari ya kuongeza gati, kwa mfano pale bandarini. Sasa uchumi wa mbogamboga, matunda, ni uchumi ambao unakua sana duniani. Sababu kubwa ambayo Tanzania tumekuwa tukishindwa kupata soko kwenye hili eneo la uchumi ni mazingira yetu katika bandari zetu. Kwa mfano, ukiangalia Bandari ya Mombasa, wao wana *cold rooms* - hivi vyumba baridi, zaidi ya 1,000 kama 1,200 na kitu. Lakini ukiangalia kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam nimesikia kuna mia na kitu, yaani hata mia mbili hatufiki. Sasa eneo hili pia Serikali ni lazima tuliangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka huu uchumi wa mbogamboga na matunda uweze kukua, na ni eneo kubwa linalokuwa duniani, ni lazima tuangalie namna gani tunavyopanua bandari zetu, basi na hizi *cold rooms*, hivi vyumba baridi vya kuhifadhi mazao vijengwe kwa wingi kulingana na hali halisi ya soko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hatuwezi kujenga, kuweka mipango ya maendeleo ya uchumi bila kuangalia mazingira. Tukiangalia mazingira duniani hali ya mazingira imekuwa mbaya, yaani hata hapa Tanzania mazingira

yameharibika sana, nimemsikia Mheshimiwa Rais akiwa Glasgow kwenye mukutano wa mazingira anasema kila mwaka tunapanda miti Milioni 276 ni taarifa nzuri Watalaan wanampatia lakini Je, nikiangalia *reflection* ukitembea huku Dodoma na Iringa ukiangalia kwa macho yako hiyo miti Milioni 276 kwa mwaka unaiona? Kwa hiyo, inawezekana wakati mwagine hawa Watalaan wanaotoa ripoti, sisemi wanaandika siyo zenyewe lakini ukiangalia misitu inavyoteketea, Je, misitu uteketeaji wake na hii miti tunayopanda vinawiana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mnavyokwenda kuangalia suala la maendeleo lazima suala la mazingira tuliangalie kwa ukaribu sana, ni muhimu sana na hili mimi kwa vile pia ni mpenzi wa mazingira siku zijazo nitakuja...

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ni kengele ya pili.

MHE. JACKSON G. KISWAGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Basi naunga mkono haja. Nilijaribu kwenda haraka, nilifikiri nitamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye haya mapendekezo yaliyoletwa ya Mpango wa Serikali wa Miradi itakayoteklezwa mwaka unaokuwa wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nitoe shukrani za pekee kwa niaba ya wananchi wa Longido, kwa ile ziara ya Rais aliyokuja Longido. Imeongeza hamasa kubwa

sana, wananchi wamejenga imani kubwa na kiongozi wao na pia kauli alizoziacha pale zimeacha hamasa kubwa na kuwafanya wananchi wa Longido wajue kwamba Rais wao anawapenda, anawajali; na hasa alipokuja kuwakabidhi ile miradi miwili; mradi wa majisafi na salama kutoka Kilimanjaro shilingi bilioni 15 za Serikali zimeleta maji kwenye Tarafa ya Longido karibu yote inakwenda kufikiwa. Ukipikia naongea habari ya shida ya maji, ni kwa sababu wilaya ni kubwa na Tarafa tatu zilizosalia bado zina shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye kile Kiwanda cha Nyama, alipotambua kwamba kuna kero ya tozo, ameacha maagizo kwamba zifanyiwe kazi ili viwanda vyetu viweze kuzalisha kwa tija na wafugaji nao waweze kupata mapato mazuri. Namshukuru sana Rais, nampongeza na Waziri wa Fedha na timu yake yote kwa kazi nzuri waliyoileta mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujikita zaidi katika eneo moja tu katika mchango wangu; eneo la sekta ya mifugo. Kabla sijaingia katika hiyo hoja, naomba nitoe angalizo katika moja ya maeneo ya vipaumbele vyta huu mpango kwenye miradi yetu ya kimkakati. Nimekuwa nikifuatilia huu Mkutano wa Mabadiliko ya Tabia Nchi unaoendelea kule Scotland, gazeti la *The Times* la Marekani nadhani kama siku mbili zilizopita, liliandika *article* iliyosema kwamba, kuna Mataifa 18 na baadhi ya Mabenki na Taasisi wanakwenda kutengeneza *deal* la kufanya mchakato wa kusitisha matumizi ya nishati inayotokana na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ikanifanya nifikirie kuhusu moja ya miradi yetu ya kimkakati hapa nchini ambao ni Mradi wa Mchuchuma na Liganga. Nikasema kwamba basi nitashauri katika kuratibu hii miradi ya kimkakati, basi tuangalie namna ya kuwekeza katika miradi ambayo itakuwa na uendelevu mkubwa na sina shida kama huu mradi wa makaa ya mawe utakuwa *viable* kwa muda gani, lakini ni vizuri kutathmini. Tusije tukawekeza fedha nydingi katika mradi ambao labda miaka mitatu au minne ijayo dunia itasema makaa ya mawe hayatakiwi tena kwa sababu yanachafua

halii ya hewa ,ni moja ya *polluter* kubwa ambayo inayoleta shida ya mabadiliko ya tabia nchi kwa maana inatoa sumu nyngi inayoingia angani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikasema kwamba basi nishauri tu kwamba katika tu kwamba katika kupanga, mwangalie hilo suala kwa makini, tujue jinsi ya kuiendea hiyo miradi ya kimkakati kwa upande wa makaa ya mawe na ninafahamu pia pale kuna madini ya chuma. Kwa hiyo, pengine tunaweza kuongeza mtaji mkubwa katika kuvuna chuma badala ya kuhangaikia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiruswa pale nchi jirani Kenya, nadhani Lamu, hivi sasa wanajenga kiwanda kikubwa kitakachotumia Makaa ya Mawe ambacho kitazalisha karibu nusu ya umeme unaohitajika Kenya. Hivi sasa, *they are doing it*. Hata hivyo, *point yako noted*. Haya mambo ya dunia wanasema tu, lakini sisi tupo sahihi.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nilitoa tu *concern* ya kitu nilicho-*observe* kwamba isije ikatokea ikafika mahali...

MWENYEKITI: Wala, hiyo itawafuata wao, lakini sisi tusonge mbele.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hii Sekta ya Mifugo, pia nimeangalia kutokana na uzoefu ambaao sasa tunao nikaona kwamba sekta ya mifugo haikui kwa kasi inayostahili na nikaona pengine kuna jambo ambalo lingeweza kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango uzingatia katika hilo ili na yenyewe iweze kunyanyuka ichangie katika uchumi wa Taifa kwa zaidi ya hii asilimia saba ambayo tunayo sasa hivi, iwepo na kilimo ni asilimia 26, nikasema basi ungeanzishwa Wakala wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala huu hautakuwa tofauti na Mawakala wengine ambao tayari tunao. Kwa mfano, tuna *REA* na mnajua mapinduzi ambayo wimeleta katika nchi yetu katika kusambaza umeme. Tuna Wakala mwingine wa *TARURA*, mnajua pia kwa kiasi gani imefungua barabara katika nchi yetu. Tunayo *RUWASA*, tunao umwagiliaji; wameleta mapinduzi makubwa katika sekta ambazo wamesimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na Wakala wa Mifugo ambayo itaenda kusimamima, kutengeneza mifuko kama ilivyo katika haya Mawakala mengine, mifuko ambayo itatusaidia sasa kunyanya Sekta ya Mifugo na kusimamia miundombinu mingi. Naomba nikutajie baadhi ya miundombinu ambayo huu Wakala ungeweze kusimamia kama utaanishwa. Kuna majosho ya kuogesha mifugo, kuna mengine yamekufa tangu zamani, kumbe wakala ukiwekwa *in place* itatusaidia sana. Kuna mabwawa na visima vyta kunyweshea mifugo, tuna masoko ya mifugo ya awali, ya upili na ile masoko ya mipakani; kuna machinjio, kuna vituo vyta kukusanya maziwa, kuna miundombinu ya usafirishaji wa mifugo na bidhaa zake. Kama kwenye minada, utakuta minada mingi haina *rampile* ya kupakilia na kupakua mifugo. Nyingine, tunahitaji hata kwenda zaidi katika mazao yanayouzwa nje. Kwa hiyo, kuna *code chain* inayoangalia mazao ya mifugo kule bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine ambayo sasa hivi nchi ina-*focus* katika kuanzisha *industrial packs*. Tungekuwa pia na eneo la *industrial packs* kwa ajili ya mazao...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Hiyo ni kengele ya pili Mheshimiwa Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi wakala huo uanzishwe, nami naungana na wenzangu

katika kusema kwamba Sekta ya Uzalishaji Kilimo na Mifugo ipewe kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa ninao Mheshimiwa Venant, yupo?

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, nipo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Venant na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana nitawaomba tutumie dakika tano tano. Tuanze na Mheshimiwa Venant halafu atamalizia Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana. Dakika tano.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia angalau dakika tano nami nitoe mchango wangu katika Mpango huu wa Serikali. Awali ya yote nianze kumshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kupambana kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma nzuri. Fedha hizi zilizoletwa katika historia nilikuwa naona mikopo mingi inakwenda kwenye miradi ya Kitaifa, lakini mkopo huu umekwenda kuwagusa wananchi wa chini zaidi hasa wa vijijini. Tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi nydingi, tunakwenda kujenga madarasa, shule na mbiundombini mbalimbali ya afya; lakini tujiandae na mambo mengine ambayo yatajitekeza hususan kwa watumishi wetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali katika mpango wao ambao utakuja kwenye bajeti ijayo, iangalie namna gani ya kutusaidia kuongeza watumishi hasa katika Sekta ya Elimu. Madarasa ni mengi, idadi ya wanafunzi ni kubwa lakini idadi ya walimu ni ndogo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ije na mpango huo wa kuweza kuongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye kuchangia Mpango. Serikali yetu katika Mpango wake ambao ulikuja mwaka 2020, wa miaka mitano, ilituelekeza itakwenda kujikita

kwenye Sekta ya Kilimo, nami wananchi wangu wengi ni wakulima. Mpaka sasa hivi, Serikali imekaa kimya, haijatoa mwongozo wa nini kinakwenda kutokea juu ya ongezeko la bei ya mbolea. Tumekuwa na kigugumizi, hatujapata bei elekezi mbolea ni shilingi ngapi? Tunakwenda kwenye msimu ambapo mvua kwenye baadhi ya mikoa imeshaanza. Leo hii tunapokea simu kutoka kwa wananchi, wanauliza nini kilichotokea? Nasi hatuna majibu.

Naiomba Serikali isimame mbele, itoe mwelekeo na dira kwa wakulima kwa sababu msimu umeshaanza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mbalimbali ya kuisaidia Sekta ya Kilimo, naishukuru Wizara ya Kilimo inaendelea kupambana, lakini kuna mpango walikujanao wa kuwakopesha wakulima matrekta. Katika mkao wangu na Jimbo langu wapo wananchi ambao walikopa. Ile mikopo ilikuwa ni kichefuchefu. Yamekwenda matrekta hayalimi hata nusu eka kwa siku, lakini wamekwenda kukopeshwa, na wale waliowakopesha kuitia Wizara ya Kilimo hawafuatilii changamoto gani wanazopata kwenye kukusanya madeni. Wamekwenda TAKUKURU, eti TAKUKURU wakakusanye madeni. Sijawaji kuona aliyekopesha ni mwingine, anayekwenda kukusanya ni chombo kingine cha Serikali tena kikubwa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, yale matrekta ambayo yalikuja kule, wananchi wameyapaki. Agizeni vyombo vyenu mkachunguze.

MWENYEKITI: Aina gani Mheshimiwa, hayo yanayolipa nusu eka kwa wiki.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Mwenyekiti, yanaitwa Ursus yametoka *NDC*. Yale matrekta nusu eka hayalimi. Kwa hiyo, naiomba Serikali, wananchi wangu wameyapaki, hawayatumii tena, wanahitaji wavunje mkataba. Wale jamaa wanapigiwa simu hawapokei. Nendeni mkachukue trekta zenu, mkataba uishe. TAKUKURU hawataki kuwaona huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tusaidie wakulima wetu katika maeneo yetu, lazima kama Serikali tuone namna gani ya kuweza kuwasaidia hususan kuwaletea zana bora za kilimo. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Wanyamwezi washamba kweli! Mimi mwenyewe nina trekta Ursus inalima siyo kawaida. (*Kicheko/Makofii*)

Kabisa! Nilikuwa napata shida hiyo hiyo, lakini nikampata kijana ameenda kui-set; ni *setting* tu. Hamjui namna ya kuzi-set, inalima kweli kweli. Shauri yenu na ushamba wenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Pindi Chana. (*Kicheko*)

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naanza na pongezi kwa Rais wetu, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kumshukuru sana Waziri na Baraza zima la Mawaziri kwa kutuletea mapendekezo haya ya Mpango na vile vile naunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Njombe, kwa kweli wanatoa shukrani nydingi sana kwa mambo mengi makubwa ambayo Serikali hii imekuwa ikiyafanya, hususan suala zima la ununuzi wa mahindi na kuboresha upande wa kilimo. Wananchi hawa pamoja na shukrani hizi, jana na juzi nimekuwa naongea nao wa Makete, Ludewa, Wanging'ombe, Njombe Mjini, Lupembe, Makambako, wanasema Mheshimiwa pamoja na mambo mazuri haya, hivi kwa nini bei ya mbolea ipo juu? Nikawa nawaelezea kwamba mbolea hii inaagizwa kutoka nje. Wakasema bee Mheshimiwa, yaani mpaka leo tangu Uhuru karibia tunakwenda miaka 60 ya Uhuru bado tunaagizaga tu mbolea Nje! Kwa nini tusizalishe wenyewe mbolea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mjumbe hauawi, nafikisha. Wananchi wanaauliza, lini tutazalisha mbolea ya kujitosheleza? Wanasema siyo tu mbolea, zana zote za kilimo; iwe ni majembe, *power tiller*, iwe ni trekta, wakati umefika sasa Tanzania tuzalishe bidhaa zetu. Maana asilimia 60 tumejkita kwenye kilimo, sasa utaratibu huu wa kuagiza zana za kilimo nje watakuwa wanatupangia bei na tutakuwa tunaendelea kusema bei imekuwa kubwa, bei imekuwa kubwa. wa kweli tuzalishe zana zetu za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyo viwanda mbalimbali vya mbolea. Tukae nao tuwaambie, mahitaji ni haya, sasa hapa tunasaidiana vipi wazalishe mbolea ya kupandia, mbolea ya kukuzia ya kutosheleza? Kwa hiyo, naomba nilete salamu hizi kutoka Mkoa wa Huzunze, wanaomba sana hili suala la mbolea tuone jinsi ya kuzalisha na litosheleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima niendelee kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan. Upande wa Diplomasia, ziara za Mheshimiwa Rais zimeijengea heshima sana nchi yetu. Mheshimiwa Rais amefanya ziara katika Mkutano ule wa *United Nations General Assembly*na alihutubia pale Marekani na vile vile Mkutano wa *Cop 26*. Mikutano hii, imekuwa inazaa matunda mengi sana. Tanzania tunaendelea kuwa kwenye ramani ya Kimataifa, kwa kweli niendelee kushukuru sana, ziara hizi zinasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mapendekezo haya ya Mpango tumeona kwamba baadhi ya Balozi zimeendelea kufunguliwa na *last time* wakati nachangia nilombwa sana tuendelee kufungua Balozi pale Vienna tumefungua, tumefungua pia pale China, Guangzhou na maeneo mengine.

Sasa wakati ni huu wa kuendelea kufungua Balozi. Tuendelee kuwaalika nchi nyininge pia waje wafungue Balozi hapa Tanzania na kutokea Tanzania waendelee kuhudumia nchi za *SADC* na Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mchuchuma na Liganga kwa kweli ni la kulitia maanani. Wengi wamesema, lakini hivi karibuni tumeanza kupeleka Makaa ya Mawe India. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuanza kupeleka Makaa ya Mawe India kupitia Bandari yetu ya Mtwara. Nasi wananchi wa Njombe, Ludewa tunasema na Ludewa Makaa ya Mawe tuone jinsi gani ya kuendelea kuyakuchukua na kuendelea *ku-export*, na ule mradi uendelee kuwekewa vipaumbele vyatutoshya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, salamu nyingine kutoka Njombe hususan wanawake, wanashukuru vifo vyavya akina mama wajawazito na watoto vimeendelea kupungua. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Kengele bado eeh!

MWENYEKITI: Malizia dakika moja.

MHE. BALOZI DKT. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, wanaomba Bima kwa wote, wanapiga na magoti. Bima kwa wote itaongeza muda wa maisha, *lifespan* ya Watanzania. Bima kwa wote itasaidia, tutakuwa tuna afya nzuri, kwa hiyo, tutachapa kazi zaidi. Ofisi yangu pale Njombe nimeanza *pilot* kuwakatia akina mama Bima. Wanaishukuru sana Serikali, wanashukuru Bunge kwa kupitisha Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe wamekushukuru sana, wanaomba uje kule Njombe ufanye ziara ukiwa kama Spika kuangalia utekelezaji wa sheria mbalimbali zinazotungwa na Bunge. Kwa hiyo, wanaaulizia Sheria ya Afya kwa Wote (*Universal Health Care*) inakuja lini? Kwa hiyo, mpango huu ukizingatia, tutashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkongo hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI: Bunge linarejea.

MWENYEKITI: Ahsante.

(Bunge lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni sana kwamba tumeweza kufikia hapa tulipofika. Tunapoendelea na uchangiaji kuhusu hoja ya kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka 2022/2023, majadiliano bado yanaendelea. Leo jioni tumeweza kupata Wabunge 25, siyo haba. Naamini Jumatatu na Jumanne tukimalizia, tutakuwa tumepeata Wabunge wengi kabisa.

Nina matangazo machache. Moja, naomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mnaalikwa kesho tarehe 6 Novemba, 2021 katika *Hotel ya Royal Village* ambako kutakuwa na Maadhimisho ya Mwaka Mmoja wa Uongozi wa Mheshamiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Shughuli hiyo itaanza saa 4.00 asubuhi, hivyo mtakaokuwa na nafasi mnakaribishwa.

Pia tangazo linawakumbusha kwamba kuna semina kesho ya Wabunge wote, semina muhimu ambayo itaanza saa 3.00 asubuhi, Ukumbi wa Msekwa ambapo yale mambo ambayo tulikuwa tumekubaliana kwa kesho na kesho kutwa, mada ya kwanza itakuwa Fursa ya Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ambayo watawasilisha watu wa *UTT AMIS* na Mafanikio ya Uwekezaji kwa Njia ya Vipande, tutaelezwa pale.

Mada itakayofuata itakuwa ya kutoka kwa ndugu zetu wa *DSE* kuhusu Nafasi ya Soko la Mitaji katika Kukuza

Uchumi Binafsi wa Mbunge na mafanikio ambayo yanapatikana na hilo. Mada itakayofuata itakuwa Majumuisho Kuhusu Fursa ya Uwekezaji katika hiyo Mifuko na majumuisho kuhusu Nafasi ya Soko la Mitaji. Hiyo ni kesho. Mpaka saa 7.00 au saa 8.00 tutakuwa tumemaliza mada zote mbili; ya *UTT* na *DSE*.

Halafu keshokutwa Jumapili kuanzia saa 5.00 asubuhi; kwanza asubuhi kutakuwa na zile mbio *NBC Marathon*, lakini kuanzia saa 5.00 baada ya wenyewe kusali kutoka huko, tutaanza na Uwekezeji kwa Njia ya Hati Fungani Kupitia Masoko ya Fedha. Halafu tutakuwa na mada ya pili ya Uzoefu katika Biashara na Ujasiliamali ambapo tutakuwa na wafanyabiashara kama sita hivi ambao wataongea nasi kuhusiana na uzoefu wao binafsi katika masuala ya uwanja wa kibiashara kwa ujumla wake.

Tunaamini mada kama hizi ni muhimu, ni vizuri vile vile mkafika. Huwezi kujua unaweza ukajikuta umepata *idea* kutokana na *presentation* hizi ambazo zinaweza kukutoa kiuchumi. Tunafanya hivi makusudi ili kutoa fursa ya kuweza kusikia na kuona wenzetu huko wanafanya nini katika masuala mazima ya uwekezaji. Uwekezaji huu ni kidogo kidogo unakwenda, kidogo kidogo unakwenda, mpaka unafika mahali unakuwa na uchumi binafsi ambao ni bora zaidi.

Baada ya matangazo hayo, sasa shughuli za Mezani hapa zimekamilika. Kwa jinsi hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa 8.00 mchana.

*(Saa 1.05 Usiku Bunge lilahirisha hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 8 Novembra, 2021 Saa Nane Mchana)*